Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi – Tarehe 26 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 86

**Rasimu ya Ahadi za Serikali**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya Wabunge kuuliza juu ya utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais alizotoa wakati wa kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2005.

(a) Je, isingekuwa vema kwa Serikali ikaandaa rasimu ya ahadi zote za Mheshimiwa Rais/Serikali na mkakati wa utekelezaji wake awamu kwa awamu?

(b) Kwa kuwa, ahadi za Mheshimiwa Rais zinategemea upatikanaji wa fedha. Je, isingekuwa vizuri utekelezaji wa ahadi hizo ukahusisha hata Serikali za Mitaa kwa maana ya Mikoa, Halmashauri za Wilaya badala ya kutaka Serikali Kuu peke yake izishughulikie?

(c) Je, kwa nini Serikali isiunde Kamati ya kufuatilia ahadi hizo Wilaya kwa Wilaya na kuratibu ukweli wa ahadi hizo ili kusiwepo na ahadi ambazo Mheshimiwa Rais hakusema wazi wazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia ushindi wa mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, Serikali iliandaa orodha ya ahadi alizotoa Rais wakati wa kampeni katika kitabu kiitwacho Mwelekeo wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ahadi za Mgombea Urais wa CCM. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa ahadi hizo unakwenda sambamba na ilani yenyewe. Aidha, Wizara na Mikoa yote Tanzania Bura ilielekezwa kuandaa programu za kutekeleza Ilani ya Uchaguzi na ahadi za Rais na kuziweka katika mipango yao ya kila mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais unategemea sana upatikanaji wa fedha na baadhi zinahitaji fedha nyingi. Kwa mantiki hiyo utekelezaji wa Ilani na ahadi za Rais zinatekelezwa na ngazi zote za Serikali ambazo ni Wizara, Mikoa na Halmashauri. Ngazi hizo zote zinawajibika kutenga fedha kulingana na Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Kwa mantiki hiyo, wananchi na Halmashauri za Wilaya zina mchango mkubwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inafuatilia ahadi hizo kwa dhati. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya ahadi alizotoa mgombea wa Urais hazikuorodheshwa katika kitabu. Ofisi ya Waziri Mkuu imewasiliana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa ili waainishe ahadi zote ambazo hazikujumuishwa kwenye kitabu chenye orodha ya ahadi za mgombea. Mara baada ya kupokea ahadi hizo, zitajumuishwa kwenye kitabu kimoja na kusambazwa kwa watekelezaji na wadau wote. Hivyo basi, ushauri wa kuunda Kamati ya Ufuatiliaji wa ahadi hizi kwa sasa hautakuwa na mchango mkubwa kwani utaratibu uliopo wa uratibu wa ufuatiliaji kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Halmashauri unajitosheleza.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ni ya kuridhisha. Nina maswali mawili ya nyongeza: Kwa kuwa, katika Ilani ya Uchaguzi, ahadi nyingi zilizotolewa katika Ilanai pamoja na viongozi mbali mbali zimekuwa ni masuala ya barabara na katika Ilani hiyo ya Uchaguzi, barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga ilipewa kipaumbele na tatizo lililopo ni kwamba hakuna fedha za ndani za kuweza kuisaidia hiyo barabara. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba katika kipindi hiki ambacho tunangoja fedha za *Mellenium Challenge Corporation (MCC)* kabla hazijatolewa, Serikali itakubali kutoa angalau kiasi fulani cha fedha ili barabara hii ianze kutengenezwa? La pili, kwa sababu inaonekana katika ahadi nyingi sana ambazo zimetolewa, kipaumbele zaidi kimekuwa wananchi wakiomba barabara, kila mahali barabara. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuwa na Mfuko Maalum tena mkubwa kabisa wa kuhakikisha barabara zinapewa kipaumbele katika nchi nzima?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na barabara ya Tunduma Sumbawanga, ni kweli kabisa barabara hii iko katika Ilani na viongozi Wakuu wa nchi hii hasa wanapotembelea maeneo haya, wamekuwa wakiwapatia wananchi matumaini kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahadi hiyo, bado iko pale pale na katika mwaka huu wa fedha kama tutakavyokuja kuona katika bajeti ya Wizara ya Miundombinu, kwa hilo hilo ambalo Mheshimiwa Kimiti amelisema, angalau Serikali imetenga kifungu kidogo cha kuanza matengenezo wakati tunasubiri fedha kutoka Serikali ya Marekani. Pili, suala la kuwa na Mfuko Mkuu ambao utakidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara nchini: Mheshimiwa Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Mfuko uliopo wa Barabara, shabaha yake ilikuwa ni hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Kimiti anaisema.

Lakini, uwezo wetu wa ndani bado ni mdogo na ndio maana katika majadiliano ambayo ninyi Waheshimiwa Wabunge mmeyasema, ni nini tukifanye ili kuweza kuongeza mapato kwenda kwenye Mfuko huo? Tunashukuru sana maamuzi yenu kupitia Bajeti ya Serikali kwamba tumeangalia maeneo machache ambayo yatatunisha kidogo Mfuko huo. Lakini, bado nasema hatujafika kiwango cha kuwezesha kutengeneza barabara za nchi hii ambayo kwa *network* iliyopo sasa hivi ni bilioni 221. Mheshimiwa Spika, bado tuko chini. Lakini, mawazo ya changamoto tunayakaribisha. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ahadi za Mheshimiwa Rais ziko za aina mbili. Kuna ahadi zile ambazo ameahidi wakati anafanya kampeni, lakini pia kuna ahadi ambazo ametoa baada ya kampeni alipokwenda kwenye Wilaya mbali mbali ambazo hakuweza kufika wakati wa kampeni na akaahidi mambo ya maendeleo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atanihakikishia kwamba ahadi hizi za awamu ya pili zitaingizwa katika hicho kitabu alichokizungumzia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu katika swali la msingi, sasa hivi tunafanya tathmini kuhakikisha kwamba kile kitabu ambacho kimeorodhesha ahadi zote za Mheshimiwa Rais, kinajumuisha ahadi zote ikiwa ni pamoja na zile ambazo alizitoa wakati wa kampeni na pia zile ambazo alizitoa baadqa ya kampeni. Lakini, pia tunaangalia hata zile ahadi ambazo wamezitoa Waheshimiwa Wabunge wetu wa CCM wakati wakigombea ili kuhakikisha kwamba zile ahadi zinaangaliwa na wao wenyewe waweze kutekeleza kwa ushirikiano na Serikali. *(Makofi)*

Na. 87

**Shughuli za Wizara ya Afya Zilizoko TAMISEMI**

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) inashughulikia mambo mengi sana kwa mfano shughuli za Mikoa, Halmashauri zote nchini pamoja na Manispaa zote na bado wanasimamia shughuli za Afya:-

(a) Je, kwa nini shughuli zinazohusiana na Wizara ya Afya kama vile zahanati na hospitali za Wilaya ambazo ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zirudishwe Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii?

(b) Kwa kuwa, wakati wa kipindi cha maswali Bungeni, Waziri wa TAMISEMI anapata shida sana kujibu maswali mpaka mengine inabidi Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii achukue jukumu la kujibu kwa vile majukumu mengi yapo kwake; Kwa nini shughuli hizo pamoja na zile za magari zilizo chini ya TAMISEMI zisirejeshwe Wizara ya Afya?

**SPIKA:** Ninampongeza sana, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, kwa sababu amekuwa na bahati, maswali yote mawili ya nyongeza amekingwa na Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo inasimamia shughuli mbali mbali katika Mikoa na katika Halmashauri zote hapa nchini. Shughuli hizo siyo tu zinazohusu sekta ya Afya bali ni pamoja na sekta ya Elimu, Barabara, Kilimo, Maliasili, Uvuvi na kadhalika. Rai ya Mheshimiwa Mbunge na hakika hata Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa angefarijika sana kama majukumu haya yangehamishiwa katika sekta zinazohusika, na kwa hakika hivyo ndivyo ilivyokuwa mpaka mwaka 1982.

Mheshimwa Spika, kuanzia mwaka 1981, Serikali iliamua kwa makusudi kuanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kama vyombo vya kutekeleza shughuli mbali mbali zilizo chini ya Serikali zikiwemo zile nilizozieleza awali. Bunge lako tukufu katika kutekeleza azma hiyo lilitunga Sheria mbali mbali za Serikali za Mitaa zikiwemo Sheria Na. 7, Na. 8 na Na. 9. Azma hii ilitokana na sera za Chama Tawala za Kupeleka Madaraka kwa Wananchi kwa mujibu wa Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naamini Waheshimiwa Wabunge wamekwishakuona matunda ya utekelezaji wa Sera hiyo. Kwa hiyo, kwa sasa shughuli hizo zote zitaendelea kutekelezwa na vyombo hivyo kulingana na matakwa ya Katiba na Sheria zilizotungwa na Bunge hili.

(b) Mheshimiwa Spika, maswali yote ya msingi ambayo yamekuwa yakiulizwa na Waheshimiwa Wabunge yanayohusiana na shughuli za utekelezaji ndani ya TAMISEMI yamekuwa yakijibiwa kikamilifu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Maswali yote ambayo hayahusiani na utekelezaji yamekuwa yakijibiwa kikamilifu na Wizara za Kisekta ikiwemo Wizara ya Afya. Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa na zile za Serikali za Mitaa, Majukumu ya Serikali Kuu ni pamoja na Kutunga Sera za Kitaifa, Mafunzo ya Kitaalum na kuweka vigezo vya utendaji katika sekta husika. Haya ndiyo maeneo yanayohusiana moja kwa moja na Wizara za Kisekta.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo na kwa kuzingatia msingi wa *Colective Responsibility* ndani ya Baraza la Mawaziri, Mbunge anapouliza swali la nyongeza; narudia, swali la nyongeza, ambalo badala ya kulenga katika masuala ya utekelezaji, linagusa maeneo niliyoja ambayo ni ya kisera, ni wajibu wa Waziri yeyote kusaidia kujibu swali hilo la nyongeza. Kufanya hivyo, hakutokani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kupata shida sana kuibu maswali hayo ya nyongeza na hivyo Mawaziri wa sekta husika kulazimika kuyajibu isipokuwa ni kutokana na mgawanyo wa majukumu ndania ya Serikali.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza kwamba; ni azma ya Serikali ya Awamu ya Nne katika kipindi hiki kijacho kuanzisha ujenzi wa Zahanati katika kila Kijiji na Vituo vya Afya katika kila Kata. Kwa maana hiyo, mzigo wa matatizo utakuwa mkubwa na malalamiko kwa Wizara ya Afya. Je, bado Mheshimiwa Naibu Waziri anaendelea kuona kwamba wataendelea kumudu matatizo hayo wakiwa TAMISEMI bila kusaidiwa na Sekta ya Afya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Mheshimiwa amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya na amefanya kazi hizi kwa ushirikiano wa karibu sana na Serikali za Mitaa. Nina hakika kabisa anajua mipaka kati ya Serikali Kuu kwa maana ya Wizara za Kisekta na yale yanayohusiana moja kwa moja na Serikali za Mitaa katika ngazi ya Wilaya.

Ujenzi wa Zahanati, ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata, ujenzi wa Sekondari, uchimbaji wa Visima vya maji na kadhalika. Hivi vyote ni shughhuli zinazofanywa na wananchi katika ngazi za Vijiji, ngazi za Kata na ngazi za Halmashauri. Kama tulivyofanya kwenye shule za Sekondari na kama tunavyofanya kwenye shule za MMEM, kazi hiyo itaendelea kufanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Afya analo jukumu sasa la kusaidia baada ya ujenzi huo, kuleta wataalam, kuhakikisha analeta dawa na kuhakikisha anasimamia ubora wa utendaji kwa maana ya usimamizi wa taaluma katika Sekta ya Afya kwa watendaji wote ambao wako chini ya Wizara ya Afya. Kwa hiyo, hakuna tatizo kati ya Wizara ya Afya katika majukumu yake na yale yanayohusiana na Serikali za Mitaa katika ngazi za Wilaya. Mheshimiwa Spika, na labda niongeze; Wakati mwingine unaweza ukafanya

makosa kwa kuiona TAMISEMI kana kwamba siyo sehemu ya Sekta za Kiserikali. Ofisi hii iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni Wizara nyingine au ni Ofisi nyingine ambayo kwa pamoja na *Sector Ministries*, tunafanya kazi moja tu ya kuzisaidia Halmashauri zote katika ngazi zinazohusika. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napongeza sana majibu yote mawili ya Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, wamejibu vizuri sana. Lakini, ningependa kutoa maelezo kidogo juu ya suala la Zahanati na Vituo vya Afya. Tumelieleza katika hotuba, lakini nadhani halijaeleweka vizuri. Wale walionisikiliza, tulisema kwamba tumegundua kwamba tuna Vituo vya Afya 255 vilivyojengwa na *TASAF*. Kwa hiyo, mwaka huu kazi yetu kubwa ni kufanya *training* ili tupate watu wakuweza kwenda ku-*man* Vituo vya Afya hivyo na Zahanati hizo pamoja na kuweka vifaa. Mwaka unaofuata, 2008/2009 na 2009/2010 ndio tutaazana ujeni nchi nzima kama tulivyofanya kwa ajili ya shule za Sekondari. *(Makofi)*

Na. 88

**Ubovu wa Barabara za Mashambani Kwenda Mijini**

**MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna barabara nyingi zinazotoka mashambani kwenda Mijini ndani na nje ya Jimbo la Bukene na nchini kwa ujumla ambazo hutumika kusafirisha mazao toka mashambani kwenda Sokoni; na kwa kuwa barabara hizo ni mbovu, mfano barabara inayotoka Kata ya Ikindwa ambako mazao yao hupelekwa Shinyanga/Mwanza kupitia Mwamala, Isaka, Tinde, Mwanza:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo ili wakulima wafikishe mazao yao sokoni?

**SPIKA:** Naona leo Waheshimiwa Manaibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu wana bahati kweli, kila mmoja, kila nyongeza inachukuliwa na Wakubwa! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella – Bantu, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 685.5, kati ya hizo kilomita 192 ni barabara za Mijini, Kilomita 70.5 ni barabara za Wilaya na kilomita 423 ni za barabara za Mjazio *(Feeder Roads)*. Kati ya mtandao huo, Jimbo la Bukene lina barabara moja ya Wilaya inayotoka Bukene Mjini kuelekea Kamahamanhalanga yenye urefu wa kilomita 28.3.

Aidha, barabara za Wilaya zinazounganisha majimbo ya Nzega na Bukene ni Nzega – Karitu – Bukene yenye urefu wa kilomita 40.11 na Itobo – Mwangoye –Lusu – Choma cha Nkola yenye Kilomita 49. Kutoka kata ya Kahamanhalangakupitia Malolo *Irigation Scheme* (Kata ya Ikindwa) hatimaye hupelekwa Shinyanga/Mwanza kupitia bandari ya nchi kazu ya Isaka iliyoko Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga, kwa kupita kata za Mwamala, Mwangoye na Sigili za Jimbo la Bukene Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauri wananchi wa Jimbo la Bukene waendelee kutumia barabara ya Bukene – Itobo, Nzega – Itobo – Kahama na Itobo – Mwangoye – Choma cha Nkola katika kusafirisha mazao yao ambazo zina hali zuri ya kupitika kwa muda wote wa mwaka. Hata hivyo, Serikali itajitahidi kutengeneza barabara zake ili ziweze kupitika na wananchi waweze kusafirisha mazao yao kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa najua kwamba kuna fedha zinazotolewa kwa ajili ya kutengeneza barabara zinazotoa mazao shambani kupeleka sokoni; na kwa kuwa sehemu hii niliyotaja ina pitisha mazao mengi sana kupeleka katika sehemu nilizozitaja.

Je Serikali haioni kwamba sasa uko umuhimu wa kutengeneza angalau daraja lililopo katika kitongoji cha Sole na Kilialyoha katika Kijiji cha Malolo ili kuwasaidia wananchi hawa, wakulima kufikisha mazao yao sokoni kwa urahisi zaidi na karibu zaidi kufika Isaka kuliko kupita Nzega?

**SPIKA:** Wahandisi, mngerekebisha taa! Sasa naona imekuwa giza humu ndani!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa barabara ambazo zinapitisha mazao katika Jimbo lake. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba barabara hiyo ya *Malolo Irrigation Scheme* ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao.

Lakini, kwa sasa Serikali inawaomba wananchi wa Bukene pamoja na Halamashauri husika, waiangalie barabara hiyo, waifanyie *feasibility study* na baadaye kuleta maombi yao kwenye vyombo husika. Pili, katika Halmashauri hiyo ya Nzega, kuna fedha ambazo ni za *Local Government Transport Porgamme*, shilingi milioni 73.

Ninaomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya kuhakikisha kwamba barabara hiyo inafanyiwa upembuzi yakinifu na baadaye kuiweka kwenye mipango yao ya barabara za Wilaya.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara nyingi za vijijini ziko chini ya

Mhandisi wa Wilaya na barabara hizi nyingi ni mbovu si kwa sababu ya kwamba hazitengewi fedha, lakini pamoja na fedha kidogo kutengwa, barabara hizi zimekuwa zikitengenezwa kwa kiwango cha chini sana na mara nyingi zimekuwa zikitengenewa kwa gharama kubwa bila kukidhi viwango vinavyotakiwa na mara kadhaa kumekuwepo ucheleweshaji. Kwa mfano, katika Jimbo la Msalala, barabara itokayo Kahama kwenda Chela – Mpakani mwa Wilaya ya Kahama na Geita, barabara hii imechelewa sana kwa sababu ya matatizo ya Mhandisi.

Je, Serikali iko tayari sasa kukubaliana na malalamiko au wito ambao umekuwa ukitolewa na Waheshimiwa Madiwani kwamba ichukue hatua pale inapoona kuna matatizo kwa watendaji wake ambao ndio wanaiwakilisha Serikali katika utekelezaji wa Ilani yake kwenye Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyokiri Mheshimiwa Mbunge kwamba hela zinazotengwa kwenye barabara za vijijini ni hela kidogo sana. Lakini, kwa mwaka huu angalau fedha zimeongezeka. Nina uhakika kwamba barabara zitatengenezwa kwa kiwango kinachohitajika. Kuhusu watumishi ambao hawatimizi wajibu wao, mimi ningeshauri Waheshimiwa Wabunge, hao watumishi ambao hawatekelezi wajibu wao ipasavyo, ni jukumu la Baraza la Madiwani kuwachukulia hatua za kinidhamu pale wanapoona kwamba hawafanyi kazi wala hawatimizi wajibu wao. Sisi, kwa upande wa Wakuu wa Idara, wanashughulikiwa na Halamashauri za Wilaya zenyewe.

Lakini, kwa upande wa Wakurugenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ndio inawashughulikia katika suala la nidhamu. Lakini, pamoja na hayo, ni lazima hoja ianze kujengwa kutoka katika Wilaya husika. Kwa hiyo, nawashauri Waheshimiwa Wabunge waanze kuchukua hatua kule kule Wilayani na siyo kungojea mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ichukue hatua.

Na. 89

**Matumizi ya Mmea wa Aloe Vera**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH (K.n.y. MHE. KIDAWA H. SALEH)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni mmea mshubiri wa *Aloe Vera* umepata umaarufu mkubwa kutokana na matumizi yake katika eneo la tiba:-

(a) Je, Serikali inaweza ikatueleza mmea huo unasaidia tiba ya magonjwa gani?

(b) Je, Serikali imefanya utafiti wowote juu ya mmea huo?

(c) Je, Serikali inatoa maelezo gani kwa wananchi juu ya matumizi bora ya mmea huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mshubiri *(aloe vera)* ni jamii ya mmea ambao upo katika kundi la mimea inayoitwa *aloe* ambayo ipo takriban 250. Majani, shina na mizizi ya mshubiri hutumika katika sehemu mbali mbali duniani kama dawa ya kutibu magonjwa mbalimbali kama vile pumu, magonjwa ya ini, figo, moyo, Kisukari, vidonda vya tumbo viungo, magonjwa ya viungo, magonjwa ya ngozi. Kwa mfano, mapunje na mba, vidonda, masikio yanayotoa usaha, kuungua moto, kulainisha choo na kiungulia.

Aidha, mshubiri una madini ya chuma, *Amino Acid*, vitamin na virutubisho muhimu kwa binadamu. Kwa sababu hii, mshubiri hutumika kama sehemu ya virutubisho vya ziada kwa wagonjwa wa UKIMWI na saratani. Vile vile mmea wa mshubiri unatumika kutengeneza vipodozi mbali mbali kama vile sabuni, losheni na krimu.

(b) Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine Morogoro kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vimefanya tafiti nyingi ambazo matokeo yake yamechapishwa katika majarida mbalimbali ya kimataifa. Tafiti hizo zililenga kuthibitisha matumizi ya mshubiri katika kutibu magonjwa ya kuku kama vile mdondo na kideri.

(c) Kama nilivyosema hapo awali, tafiti zinaonyesha kuwa mshubiri unaweza kutumika kama virutubisho na tayari *juice* yake inapatikana na kutumiwa na baadhi ya wananchi. Hata hivyo kwa kuwa matumizi yake kama tiba kwa magonjwa mbalimbali hayajafanyiwa utafiti hapa nchini, ni wajibu wa kila mgonjwa kupata ushauri wa kitaalamu kabla ya kutumia mmea huu kama dawa. Aidha, kwa kuwa matumizi ya mmea huu yanayoongezeka siku hadi siku, Wizara yangu kwa kupitia taasisi ya taifa ya utafiti wa magonjwa ya binadamu inajiandaa kuanza kufanya tafiti mbalimbali kuhusu matumizi ya mmea huu katika tiba. Tunaangalia uwezekano wa kuzuia kukua kwa vimelea vinavyosababisha kuoza meno.

Na. 90

**Mpango wa Kupunguza Vifo vya Akina Mama**

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika kutimiza azma yake ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto imeanzisha mpango uitwao *Road Map*:-

(a) Je, ni Wilaya gani zimepewa kipaumbele katika kutekeleza mpango huo?

(b) Je, Serikali imefanya nini katika kuboresha mazingira ya kazi kwa watoa huduma hizo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha huduma za dharura zinapatikana vijijini kwa akina mama wanaopata matatizo wakati wa kujifungua?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hemedi Mohamed Hemedi, Mbunge wa Chonga, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, watakuwa na taarifa kwamba Tanzania ilisaini mkataba wa Umoja wa Mataifa wa malengo ya maendeleo ya *Millennium* na malengo namba 4 na namba 5 yanahusu kupunguza vifo vya watoto na kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

*Road Map* ni mpango kabambe wa kuharakisha kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi pamoja na watoto wachanga tukitilia maanani mazingira yetu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mpango huo unalenga kupungaza vifo vya mama wajawazito kutoka 578 mpaka 265 kwa vizazi hai 100,000 na vifo vya watoto wachanga kutoka 32 hadi 19 kwa kila vizazi hai 1000 ifikapo mwaka 2010. Maeneo muhimu yaliyoainishwa katika mpango huu ni pamoja na yafuatayo:-

Kuelimisha jamii kuhusu vidokezo mbalimbali vya hatari vinapotokea pamoja na kuchukua hatua za dharura kuokoa maisha ya mama, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za uzazi salama za dharura katika vituo vyote vya kutolea huduma ambayo inahusisha upatikanaji wa vifaa, damu salama, kuboresha mazingira ya kutolea huduma na dawa mwaka huu tunategemea kutoa *delivery kits* kwa kila kituo kinachotoa huduma hii kama mtapitisha Bajeti ya Wizara ya Afya, kuboresha rufaa kuviwezesha vituo kuwa na mawasiliano magari ya kuwahudumia wagonjwa, kupeleka huduma za dharura karibu na wananchi kwa kuviwezesha baadhi ya vituo vya afya kutoa huduma za upasuaji kwa wanawake wenye matatizo, kutoa mafunzo rejea ya uzazi salama kwa watumishi walio kazini na mafunzo mengine ya afya ya uzazi na kuongeza kasi ya kuajiri watumishi wenye taaluma kwa ajili ya vituo ambavyo havina watumishi na vinavyojengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mpango huu utatekelezwa katika Wilaya zote hapa nchini kulingana na rasilimali zilizopo katika Halmashauri na Serikali Kuu.

(b) Serikali inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi muhimu na kutoa mafunzo rejea kwa watoa huduma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatumia mitaala iliyoboreshwa kuelimisha jamii kuhusu kutambua viashiria vya hatari kama kutokwa damu au maji maji kwenye uke, moyo kwenda mbio, kizunguzungu, kuvimba miguu na kupata homa. *(Makofi)*

(c) Kwa kupitia utekelezaji wa mpango wa *road map*, Serikali itahakikisha huduma za dharura zinapatikana vijijini kwa kuviwezesha baadhi ya vituo vya afya kutoa huduma za dharura za upasuaji *(Emergency Obstetric Care)* kwa ajili ya akina mama wanaothibitika kuhitaji huduma hiyo. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uamuzi wa Serikali wa kutoa bure huduma za uzazi unalenga vile vile kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Je, ni kwa nini mpaka muda huu huduma hizi zinalipiwa jimboni kwangu Mwibara? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, sikupata sawa sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kajege hebu rudia na kiweke chombo katika mwelekeo mzuri ili tusikie.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uamuzi wa Serikali wa kutoa bure huduma za uzazi kwa akina mama zinalenga vile vile katika kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Je, ni kwa nini huduma hizi mpaka muda huu zinalipiwa Jimboni mwangu Mwibara?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hilo nalisikia kwa mara ya kwanza. Lakini vituo ambavyo ni vya Serikali na hata katika Hospitali Teule ya pale Bunda huduma hizi zinatolewa bure. Lakini kama kuna utendaji tofauti na hivyo ningependa tukutane ili tuweze kulifuatilia.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila mama anayezalia kituo cha afya anahitaji kupata sindano ya *egometrine* kwa ajili ya kuzuia damu. Na katika *kit* hiyo huwa kuna vichupa vitano tu vya *egometrine.* Je, Serikali inasemaje? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nisahihishe hiyo kauli. Siyo kweli kila mgonjwa anayejifungua anapewa *egometrine.* Nadhani inayozungumziwa ni uhaba wa vifaa, uhaba wa dawa, kijumla na hili nilisema katika jibu langu kwamba ni kitu ambacho tumekivalia njuga kuhakikisha kwamba tunaviongeza tusipate madhara zaidi ya kukosekana kwa hivyo vitu. (*Makofi*)

Na. 91

**Mahitaji ya Maji – Mkinga**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, matarajio ya kuondoa kero ya maji chini ya mpango wa Benki ya Dunia yalikuwa ni kuvipatia maji angalau vijiji 10 kwa kila Wilaya na kwa kuwa mpaka sasa Wilaya mpya ya Mkinga imepatiwa miradi ya maji kwa ajili ya vijiji viwili tu:-

(a) Je, kwa nini Wilaya hiyo haikupata maji angalau kwa vijiji vitano?

(b) Kwa kuzingatia uchanga wa Wilaya ya Mkinga na kero kubwa ya maji ambayo inawakabili wananchi Wilayani humo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa zaidi kwa Wilaya hiyo kwa kuongeza angalau vijiji vinane vingine chini ya mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini inatekelezwa katika Wilaya zote nchini. Wakati utaratibu huu unafanyika Mkinga ilikuwa ni Jimbo katika Wilaya ya Muheza ambapo jimbo lingine lilikuwa ni Muheza. Jimbo la Mkinga lilikuwa na watu 116,830 na la Muheza watu 182,036.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maamuzi ya kuingiza vijiji kwenye programu yalifanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Wajumbe kutoka majimbo yote mawili walishiriki katika kutoa maamuzi ya kuchagua idadi na majina ya vijiji kutoka kila Jimbo.

Kutokana na maamuzi yaliyofanywa na Halmashauri ya Wilaya tarehe 27.9. 2006 ilikubalika kuingiza vijiji vinne vya Jimbo la Mkinga na sita vya Jimbo la Muheza ili kutekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Uamuzi wa kuchagua vijiji ulizingatia idadi ya wakazi katika kila jimbo. Vijiji hivyo ni Daluni, Kibaoni, Mapatano, Kilulu Duga na Mwakijembe kwa jimbo la Mkinga na pia Kwemhosi, Mikwamba, Misongeni, Kibanda Mkumba, Kisiwani Mkumba na Ubembe kwa jimbo la Muheza.

(b) Mheshimiwa Spika, programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini itaendelea kutekelezwa hadi mwaka 2025. Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga inayo fursa ya kuongeza vijiji vingine, ikiwa itakamilisha ujenzi katika vijiji vinne vya awali. Hii itategemea uwezo na kasi ya kutekeleza miradi katika vijiji vinne vya awali. Napenda kuchukua nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya Mkinga kuhakikisha kuwa Wilaya inajenga uwezo ili vijiji vingi zaidi viweze kuhudumiwa. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu fasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani nyingi sana kwa Serikali yetu kuamua na kutangaza rasmi kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba Mkinga ni moja ya Wilaya itakuwa ni Halmashauri mwaka huu wa fedha tunaufanyia kazi. Lakini pamoja na majibu hayo napenda kuuliza maswali mawili:-

(a) Kwa kuwa vijiji hivyo vilifunguliwa chini ya mradi huu utekelezaji wake unasuasua sana mpaka sasa haujaanza. Je, Mheshimiwa Waziri, angetueleza lini utekelezaji unatarajia kuanza kwa vijiji hivyo?

(b) Kwa kuwa Serikali inaweka mkazo mkubwa sana mkakati wa kuendeleza utalii na kwa kuwa Wilaya ya Mkinga imebahatika lililokuwa pori la Mkomazi na Umba kuwa sasa Hifadhi ya Taifa na kwa hiyo tunatazamia kwamba watalii wengi watapitia. Kuna kuja ya maji kuongezwa kuweza kukidhi maji safi na salama yanayotakiwa na watalii kupitia Morogoro kutoka Kenya kwenda mpaka katika Hifadhi hiyo iliyotajwa na kwingineko.

Je, kwa msingi huo hawaoni kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza fursa za maji hasa kutegemea kwamba hii Halmashauri itachukua muda mrefu kabla haijakamilika na kutekeleza hayo na kwa msingi huo hawaoni kwamba ni vizuri viongozi wa Wizara hiyo wakaja wakasaidiana na Halmashauri na kutambua hayo. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maswali mawili marefu sana natumaini majibu yatakuwa mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miradi hii imechelewa kuanza. Lakini kuchelewa kwake ni kwa sababu ya taratibu. Ningependa kwa kifupi tu kuelezea taratibu hizi jinsi zilivyo ili kila Mheshimiwa Mbunge aweze kufahamu na kuvuta subira.

Mheshimiwa Spika, miradi hii jinsi inavyotekelezwa ni kwamba kuna taratibu ambazo zinatokana na Benki ya Dunia ili kuweza kuidhinisha fedha. Benki ya Dunia mpaka hivi sasa imefikia hatua ya mwisho. Ni kwamba taratibu zote za wakandarasi zimeanza kukamilishwa na baada ya hapo kuna taratibu ambazo kila Halmashauri itatakiwa na yenyewe iweze kukubaliana (Kuji-*commit*) kwa ajili ya utekelezaji huo. Kwa hali hiyo, kwa hivi sasa Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya TAMISEMI wameshatuma mikataba katika kila Halmashauri waweze kuishughulikia hiyo na kuisaini itakaporudi ndipo hapo hatua itakayofuatia kwa ajili ya matakwa ya Benki ya Dunia tuweze kuendelea na taratibu za kumalizia ili fedha ziweze kutoka. Kwa hali hiyo, mpaka hivi sasa hakuna Wilaya yoyote kwamba mradi huu umeanza ili kuweza kulinganisha na kusema sehemu nyingine unasuasua.

Mheshimiwa Spika, jibu la pili, kuwa sasa hivi kule ni sehemu mojawapo ya kivutio cha utalii kwamba maji yaweze kupatikana kwa wingi kwa ajili ya shughuli mbalimbali, napenda kusema ya kwamba Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri inajitahidi kwa kila njia kuongeza miradi katika Wilaya zote. Kwa upande wa Jimbo la Mkinga si miradi kumi ya vijiji ambayo kwao wanayo minne, pia kuna miradi mingine tunaita miradi ya haraka na miradi midogo midogo. Naomba miradi hiyo niweze kumtajia kwa kifupi tu ambayo iko katika Jimbo la Mkinga.

Miradi hiyo kwa upande wa Mkinga kuna mradi katika Kijiji cha Gombelo, kuna mradi katika sehemu ya Vuo, kuna mradi katika sehemu ya Machimboni na pia kuna

mradi mwingine pale pale penyewe Mjini. Kwa hiyo, miradi hiyo itasaidia kuongeza maji. Pia kuna kijiji kingine kinaitwa Sigaya na chenyewe kitapewa mradi. Kwa hali hiyo, napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba miradi tunajitahidi na miradi itazidi kuwa mingi. Pia na mwenyewe ajitahidi zaidi itakapokwisha ndipo ambapo tutaongeza mingine. (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwanza, ningependa kumshukuru Naibu Waziri, kwamba mwaka jana mapema alikubali kuja kutembelea jimbo la Mtera na kuona baadhi ya vijiji ambavyo visima vyake viliharibiwa na lile tetemeko la mwaka juzi ambalo lilitokea likatufanya hata Wabunge kukimbia Bungeni. Sasa Naibu Waziri aliwapa wananchi matumaini kwamba Serikali ingejitahidi kulishughulikia jambo hili kidharura na vijiji hivyo ni Suli, Nang'ambaku na kijiji pia kijiji cha Muungano. Hadi sasa hakuna dalili zozote zinazoonyesha kwamba ahadi hiyo itatekelezwa ingawaje nilikwenda ofisini kwake tukakaa na watalaam wake na wakanipa hayo matumaini. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anawaambia nini wale wananchi wa hivyo vijiji ambao walifurahi sana alipowatembelea na ahadi alizotoa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli niliongozana na Mheshimiwa Mbunge tukazunguka katika baadhi ya vijiji vyake vikiwemo Sulu, Nang'ambaku, Muungano na vingi vinginevyo. Ni kweli mimi mwenyewe nilishuhudia na niliona hali ilivyo mbaya kwa Kijiji cha Suli na Nang'ambaku ilikuwa ni mbali sana hatukuweza kufika kwa siku hiyo lakini ni kweli vimeathiri vibaya na tetemeko. Baada ya hapo mimi niliporudi ofisini tulikaa na wataalamu wetu tukafanya mabadiliko kuhakikisha kwamba vijiji hivyo na vyenyewe viweze kupata huduma na ambapo tulisema kwamba vijiji vyote vilivyoathirika na tetemeko tulikagua tukakuta pampu zimeharibika na tukakuta *casement* zimevunjika. Sasa hivi ni kwamba tumebakuliana na Wizara yangu hivyo vyote tutavihudumia na tumeviweka katika miradi ya *quick wins.* Ila tunapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge ya kwamba kwa sababu fedha *quick wins* ndipo sasa hivi zimefika na ziko katika utaratibu wa kuanza kutawanywa katika Wilaya mbalimbali ikiwemo na Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge kwa hiyo, naomba Mheshimiwa avute subira hivyo punde fedha hizo zitagawiwa na kazi hizo za kuweza kuhudumia hii miradi iliyoharibika iweze kuanza kushughulikiwa. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante. Kabla hatujahamia Wizara inayofuata ambayo ni Wizara ya Fedha, nilikuwa napenda kumpongeza sana Mzee Malecela kwamba leo hii vazi alilovaa na vazi la Mama Anne Kilango Malecela yote ni sare kwa hiyo ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 92

**Makato ya Withholding Tax**

**MHE. MAGRETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa *withholding tax* hulipwa na makampuni husika ambayo yana wana hisa mbalimbali.

Je, ni sababu zipi zinazosababisha wanahisa wa makampuni hayo kukatwa *withholding tax* katika mgao wa faida?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotokana na mgao wa faida (*dividend*) kwa wanahisa yanatambuliwa na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 kama mapato ya uwekezaji *(investment income).* Mapato haya yanatozwa kodi chini ya kifungu cha 9 cha sheria hiyo ambacho kinabainisha kwamba, mapato yatokanayo na uwekezaji kwa kampuni/mtu binafsi yanajumuisha pia gawio (*dividend*).

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi itokanayo na mapato ya uwekezaji *(Investment Income)* na kupunguza usumbufu kwa walipa kodi, kodi ya zuio *(withholding tax)* hukusanywa na mawakala (*agents*) ambao ni pamoja na makampuni, kwa mujibu wa kifungu cha 82 cha sheria ya mapato ya mwaka 2004. Mfumo huu unawaondolea usumbufu walipa kodi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa biashara zina tabia ya kuumwa sawa na binadamu hasa pale zinaposhindwa kukorokotoa kodi zake. Je, Serikali inavyo vituo vya kusaidia hasa wajasiriamali wadogo kukorokotoa kodi hizo katika Mikoa mbalimbali?

**SPIKA:** Laa! Haya mambo ya kitaalamu kweli.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ina ofisi kila Mkoa na ina ofisi kila Wilaya. Katika kila Wilaya au Mkoa kuna watalaam wanaohusika na masuala yote yanayohusiana na *Withholding Tax*. Vile vile kila Mkoa na Wilaya kuna hazina ndogo. Kwa hiyo, mtu yeyote ambaye anapata matatizo katika suala hili anaweza akamwona Afisa yoyote katika Wilaya au katika Mkoa. (*Makofi*)

Na. 93

**Ulipaji wa Wastaafu**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, utaratibu wa malipo ya pensheni kwa wastaafu wa Serikali kwa sasa yanafanyika kila baada ya miezi sita (6) na kwa kuwa malipo haya humsaidia mstaafu kujikimu kimaisha.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulipa pensheni hiyo kila mwezi kwa kuzingatia mkataba wa ajira?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu wake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye (a) na (b) kama ifautavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kulieza Bunge lako Tukufu, kuwa awali wastaafu walikuwa wanalipwa pensheni zao kila mwezi lakini kutokana na malalamiko ya wastaafu kuwa, gharama za kufuatilia pensheni kwenye kituo cha malipo ilikuwa kubwa kuliko ya pensheni yenyewe. Serikali ililazimika kubadilisha utaratibu wa kulipa kila mwezi na kuanza kulipa kila baada ya miezi sita. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati akiwasilisha Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/08, wastaafu wote ambao sasa wanalipwa malipo ya uzeeni na Wizara ya Fedha watahamishiwa katika Mfuko wa Pensheni ya *NSSF, PSPF, PPF* na *GEPF*. Hivyo, watalipwa pensheni kufuatana na taratibu za mifuko hiyo ambapo kwa mfano *PSPF* huwalipa wastaafu kila baada ya miezi mitatu.

(b) Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu wake zinafanyika kila hali ya uchumi inavyoongezeka kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia watalaamu wa masuala ya pensheni wanaangalia namna ya kuweza kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaafu wake wote na siyo wa Serikali Kuu tu. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu yake Naibu Waziri amesema kwamba hivi sasa kuna watalaam wanaopitia upya utaratibu wa pensheni kwa watumishi wote wa Serikali.

(a) Je, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika lini?

(b) Kwa kuwa katika majibu yake Naibu Waziri, amesema kwamba malipo ya pensheni kwa wastaafu wote wa Serikali itahamishwa kwenye mifuko. Je, ni sheria gani inatumika kuhamisha hiyo pensheni kwenye mifuko hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwanza ameuliza ni lini kazi hii itamalizika? Si rahisi kusema kwa sababu ni watalaam ndiyo watakaofanya kazi hii. Kwa hiyo, inategemea na wao na zile *data* watazihitaji na kuangalia vile vile ni wastaafu wangapi wanaohusika kwa kila sekta. Kwa hiyo, si rahisi kwa sasa hivi kusema itachukua muda gani.

Kuhusu sheria gani itatumika, huu ni utaratibu wa kufanyakazi ambao utafuata sheria zilizopo za pensheni. Kwa hiyo, hakutakuwepo na uvunjaji wa sheria yoyote katika kutekeleza hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuokoe muda. Swali linaelekezwa Wizara ya Usalama wa Raia.

Na. 94

**Wanawake Watuhumiwa kwa Kesi za Mauaji**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mahabusi wengi wa kike wanatokana na kesi za mauaji; na kwa kuwa mahabusu hao hukaa rumande kwa muda mrefu sana:-

(a) Je, Serikali inafahamu ni kwa nini kesi za Mauaji nyingi watuhumiwa ni wanawake?

(b) Je, Serikali inafahamu ni kwa nini watuhumiwa wa kesi za aina hiyo hasa wanawake wanakaa rumande muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu za makosa ya mauaji kati ya mwaka mwaka 2005 mpaka machi, 2007 zinaonyesha kwamba jumla ya matukio yaliyotolewa taarifa vituo vya polisi ni 6,115 jumla ya watuhumiwa waliokamatwa ni 5,822 kati ya hao wanaume ni 5,415 ambao ni sawa na asilimia 93 na wanawake ni 407 sawa na asilimia 7.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu hizi nilizozitoa ni wazi kuwa mahabusu wengi wa kesi za mauaji ni wanaume na sio wanawake. Wanawake ni asilimia 7 tu wakati wanaume ni asilimia 93.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu zinazoweza kusababisha mahabusu, wanaume au wanawake wenye kesi za mauaji kukaa muda mrefu rumande ni suala la mtambuka kwani linahusu taasisi za Serikali na binafsi. Zifuatazo ni baadhi ya sababu hizo:-

- Upelelezi wa kesi hizo kuchukua muda mrefu kwa sababu ya uhaba wa vifaa vya kisasa vya maabara kwa ajili ya kuchunguza vielelezo vya makosa ya jinai *(forensic laboratory),* uwezo mdogo kitaalam na idadi ndogo ya askari wa idara ya upelelezi.

- Kuchelewa kupatikana kwa taarifa za uchunguzi wa vielelezo na taarifa ya kifo *(post Mortem report)* kutoka kwa Mkemia wa Serikali na Hospitali.

- Idadi ndogo ya Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali na wa kujitegemea hivyo kusababisha mlundikano wa kesi zinazosubiri kusikilizwa.

- Mashahidi kukataa au kusita kufika mahakamani kutoa ushahidi, kukosekana kwa fedha za kuwalipa mashahidi na baadhi ya mashahidi kuhama sehemu walizokuwa wanaishi hivyo kuchukua muda mrefu kuwapata ili kufika kutoa ushahidi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Singida ni miongoni mwa Mikoa ambayo ina watuhumiwa wengi wenye makosa ya kuua wakiwemo wanawake 30 kwa takwimu nilizozipata tarehe 5 Oktoba, 2006.

(a) Je, Serikali inakubaliana na mimi kwamba kuna kila sababu sasa kujenga Mahakama Kuu Mkoa wa Singida kwa sababu watuhumiwa ni wengi wa makosa ya mauaji kuliko kutegemea Majaji kutoka Mahakama ya Kanda? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa watuhumiwa wengi wa makosa mbalimbali yakiwemo wa makosa ya kuua wanapoteza haki zao Mahakamani kwa kushindwa kujieleza ama kutokujua Sheria. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watuhumiwa wa namna hiyo wakiwemo wanawake kama wanavyofanya Shirika la TAMWA katika miji mbalimbali kusaidia akina mama na watuhumiwa wengine ili waweze kupata haki zao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia kwa majibu yake ya awali ya msingi mazuri na vile vile namshukuru Mheshimiwa Diana Chilolo kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambayo yananifanya na mimi nitoe ufafanuzi zaidi. Ni azma ya Serikali kujenga Mahama Kuu katika mikoa yote ya Tanzania na kupia mradi wetu wa maboresho ndani ya Sekta ya Sheria nafikiri azma hiyo tunaweza tukaitimiza katika miaka ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, Singida itakuwa moja ya mikoa ambayo tutaipa kipaumbele kwa sababu walizozieleza na ambazo zinajulikana kwa Mahakama ya Tanzania. Kuhusu swali la pili, ni kweli kesi za mauaji zinachukua muda mrefu kwa sababu ya unyeti wake. Ni uhalifu mkubwa na vile vile ili haki iweze kutendeka lazima upelelezi wa kutosha na kazi ya kutosha ifanywe na Mahakimu na Majaji na vile vile ni kweli watuhumiwa wenyewe wanahitaji kuwa na Mawakili ambao watawatetea endapo wao wenyewe hawawezi kujieleza vizuri ili hatimaye haki itendeke. Na ni kweli

vile vile kwamba Serikali inawasaidia watuhumiwa hawa kupata msaada wa uwakili wakati wa kesi hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wa maswali umepita na la Mheshimiwa Maida, tutalipangia siku nyingine. Naomba nitoe matangazo yafuatayo:-

Kwanza wageni, tunae mgeni kutoka Marekani Jimbo la Florida, Bwana Stan, sasa sijui ni Mussle au Musley lakini MUSSLE sijui namna ya kulitamka. Kwa sababu ingekuwa na C ingekuwa Mussle. Basi Bwana Stan ni mgeni wa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, na Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Monica Mbega. *Mr. Stan please, could you stand up. There he is, thank you very much. Welcome to Dodoma and to Tanzania, if it is your first time, we are happy to see you, and hope that you keep on coming. It is a beautiful country. (Applause)*

Naomba pia niwatambulishe kwenu Waheshimiwa Wabunge wanafunzi 35 kutoka shule ya Sekondari ya Makutopora ambao pia wamekuja na walimu wao, nadhani ni wale pale kushoto. Naomba msimame na walimu tafadhali. Karibuni sana vijana na walimu, ahsante sana kwa kuwaleta vijana kuona Bunge lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Kasembe, ameniomba niwatambulishe wanaoelekea kuwa ni ndugu zake ambao ni Merion Kasembe na Lulu Kasembe. Wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ameniomba nimtambulishe Ndugu Thomson Vedastus, mgeni wake kutoka Jimboni kwake. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao miongoni mwetu kwenye *Gallary* washiriki na viongozi wa maonyesho za asasi za kiraia *AZAKI* ambao kama nilivyosema yanaendelea haya maonyesho pale. Ningeomba viongozi na wanachama wa *AZAKI* wasimame ili Wabunge waweze kuwaona. Wale pale, karibuni sana na hongera kwa kazi nzuri mnayofanya katika jamii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Job Ndugai, Kamati ya Maliasili na Mazingira, ameniomba nitangaze kwamba leo kutakuwa na kikao kifupi katika jengo la utawala saa 6 mchana. Inasisitizwa kwamba Wajumbe wote wahudhurie bila kukosa. Saa 6 mchana ukumbi namba 428 jengo la utawala, Kamati ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, ameniomba nitangaze kwamba saa 5 asubuhi leo kwenye ukumbi namba 231 Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wanaombwa kukutana. Kamati ya Kilimo na Ardhi saa 5 asubuhi ukumbi namba 231.

Waheshimiwa Wabunge wote waliojiandikisha ili kushiriki kulenga shabaha wanaomba wakutane saa 10 jioni ukumbi namba 432. Haieleweki wanalenga shabaha ya kitu gani. Lakini nadhani wanajielewa saa 10 jioni basi wale Waheshimiwa Wabunge walenga shabaha namba 432. Natumaini yote ni kwa nia njema tu.

Waheshimiwa Wabunge leo saa saba na nusu nimearifiwa na Katibu Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kutakuwa na mkutano katika ukumbi wa Pius Msekwa saa saba na nusu Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi. Ahsante. Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, orodha yangu bado ndefu, wachangiaji waliosalia ni 79. Tutajitahidi, kwa leo tunaanza na Mheshimiwa Lucy Owenya atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo ajiandae Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga na Mheshimiwa Stephen Galinoma.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Ahsante nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza kuchangia ningependa kutoa angalizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa CCM wamekuwa na kiherehere cha kujibu hoja za Wapinzani. Ningeomba wasubiri kwanza watoe hoja zao, wapinzani watatoa hoja zao na Wizara husika itajibu hoja zetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Owenya ndiyo siasa za ushindani hizo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Sawa! Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa hotuba yake nzuri ambayo ilikuwa imefanyiwa tafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa Wizara ya Miundombinu, nitaanza na msongamano wa magari katika jiji letu la Dar es Salaam. Pamoja na Waziri Mkuu kutueleza kwamba wameanza michakato ya haraka ili kupunguza msongamano wa magari.

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba utulivu tafadhali. Naomba tutoke taratibu tu bila kelele. Mheshimiwa Lucy Owenya endelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa ku-i*ntroduce* njia tatu wakati wa *rush hours* asubuhi na jioni, bado imekuwa ni tatizo. Wale wanaopita kwa miguu wamekuwa wakipata ajali na kuna njia nyingi tu ambazo tunaweza tukapunguza msongamano wa magari Dar es Salaam, kama zile *feeder road* zitatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 65. Hili ni ongezeko la asilimia 100. Katika Wilaya ya Kinondoni wametengewa shilingi milioni 200. Hizi ni fedha ndogo kabisa kwa ajili ya kukarabati barabara. Ningeishauri Serikali iwe makini zaidi. Wajaribu kutengeneza kwanza zile barabara za ndani kwa changarawe na wazitengeneze kwa uimara zaidi badala ya kukarabati barabara kila mwaka tutakuwa tunaomba fedha kila mwaka za kukarabati barabara lakini hazitengenezeki. Kwa hiyo, wawe *more focust* watengeneze barabara moja baada ya nyingine na itatusaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kinachochangia zaidi katika kuongeza msongamano barabarani ni *traffic lights* inatia huruma unapomwona *traffic police* amesimama katikati ya *traffic lights* anajaribu kuongoza magari. Zile *traffic lights* za Dar es Salaam zimepitwa na wakati, ni za muda mrefu. Labda Serikali iangalie ni jinsi gani itakavyoweza kupata wataalam waweze ku-*up grade* zile taa zipitishe magari mengi kwa wakati mmoja na sisi tuweze kujaribu kwenda na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye kompyuta sasa hivi, tulikuwa na *Pentium One* sasa hivi tuko kwenye *Centrino* kwa hiyo Serikali nayo ijaribu kwenda na wakati. Vile vile Halmashauri za Dar es Salaam kuna sehemu ambazo taa hazipo, mfano makutano ya Uhuru na Lumumba, pale palikuwa na *traffic lights.* Tayari pale Dar es Salaam kuna Watendaji, kwa nini zile taa zisirudishwe? Kitu kingine vile vile ningependa watendaji wa Halmashauri waweze kuzingatia mitaa ya mijini. Katika miji yetu yote Moshi, Arusha hata Dar es Salaam yenyewe kumekuwa na giza usiku. Je, hata hili linasubiri viongozi wakuu wawaeleze watendaji kwamba taa za barabara zinatakiwa kutengenezwa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo sasa naomba niingie katika utalii. Awali ya yote naomba ku-*declare* kwamba mimi ni wakala wa utalii na nina *interest* katika sekta hii. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema utalii unaweza ukatuongezea mapato makubwa sana hata mimi nakubaliane naye, kama tukiwa na utalii endelevu na wenye kujali mazingira.

Waziri wa Utalii alipokuwa anachangia hoja ya Bajeti alizungumza kwamba watatangaza utalii kupitia *CNN America, CNN USA,* Australia, Newzealand na kutangaza kwenye majarida tofauti ya *Europe.* Hili jambo zuri, ni vizuri kuitangaza Tanzania, kwa sababu wenzetu wa jirani walikuwa wanajaribu kuiuza Tanzania kwa kusema *climb on Mount Kilimanjaro visit Serengeti in Kenya* lakini sasa wamekuja na *strategy* mpya wanasema *come and visit Serengeti and climb Mount Kilimanjaro or East Africa.* Kwa hiyo, tuna changamoto kubwa ya kujaribu kuhakikisha kwamba wageni wanafahamu sehemu hizi ziko Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Utalii, alivyokuwa anachangia hotuba ya *budget* ya Waziri wa Fedha alisema kwamba by the year 2010 tutakuwa na watalii wapatao milioni mbili. Hii idadi kubwa ni vizuri. Lakini ningeomba barabara za Kusini kuelekea Selous ile miundombinu itengenezwe, pamoja na wajaribu kutafuta wawekezaji ambao

wanaweza kutosha kwa kuwekeza kuweza kujenga hoteli kule Selous. Sasa hivi mimi nikiwa kama wakala wa utalii siwezi kupokea *package* ya watu 40 mpaka 50 kuwapeleka Selous. Ni vigumu sana kwa sababu kitu cha kwanza huna uhakika wa hoteli. Pili, miundombinu ya kwenda kule ni migumu. Tatu unatakiwa ukodishe ndege, ndege zenyewe zinabeba watu 10 mpaka 12.Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie ni jinsi gani ya kutengeneza miundombinu ya kwenda Kusini kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii inawezekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano katika Mlima Kilimanjaro kuna njia sita za kupanda kupitia Mlima Kilimanjaro. Katika njia moja wakati wa *pick season* njia moja inapandisha watu 200 na katika hao watu 200 wanalipa dola 650 hizi ni *none negotiable* ambazo ni *park fees* sasa dola 650 mara 200 hapo unapata dola karibu 13,000. Kwa wakati wa *pick season* ukichukua mara *at least* ule mwezi mmoja tu mwezi wa saba. Ina maana tunaweza kupata zaidi ya bilioni sita. Sasa Wizara ya Utalii ikishirikiana na Wizara ya Miundombinu inaweza ikatengeneza zile barabara za Kusini na tukaweza ku-*accommodate* hawa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea *Southern Circuit* naomba niongelee *Northern Circuit* Tarangire, Manyara na Serengeti. Katika mbuga ya Serengeti ningeomba ujenzi wa mahoteli usitishwe mara moja katika mbuga ya Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wawekezaji wanaokuja kujenga kule Serengereti wanajenga mahoteli makubwa wanajenga ma-*swimming pool* maji yatatumika mengi, maji watakayotumia yanatoka vyanzo vya maji kutoka kwenye Mbuga, hoteli zitatumia pampu kupeleka kwenye zile hoteli na bado wale wanyama walioko kule Serengeti wanategemea maji hayo hayo. *At the end of the day* wale wanyama watakimbia watarudi Masai-Mara na sisi tutabaki na Serengeti yetu bila wanyama wowote.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna mwekezaji ambaye anataka kuja kujenga kiwanja cha ndege katika mipaka ya Serengeti. Vile vile ningeshauri ujenzi wa *airport* usitishwe mara moja. Kwa sababu tayari kule Seleoue tuna kiwanja cha ndege, kama kuna mwekezaji ambaye anataka kuja kuwekeza katika kiwanja cha ndege basi aingie ubia na Serikali waendeleze kile kiwanja cha Musoma, kiweze kujengwa kiwe kikubwa zaidi, ndege kubwa ziweze kutua pale. Halafu na Serikali iangalie itatengeneza miundombinu kutoka Musoma kwenda mpaka Serengeti na *Local Tour Operators* watafaidi na utalii huu wakiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kwenye utalii, ningependa kuelewa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajumuisha, mimi kwa ufahamu wangu naelewa *Legal Tender Board* ya *Tanzania is in Tshs.* Lakini sisi kama wakala wa Kitanzania tukitaka kukata leseni tunaambiwa tulipe kwa dola. Sijui Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba tunathamini fedha zetu badala ya kuthamini dola zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza kwenye Wizara ya Utalii, naomba sasa niingie kwenye Afya. Ni jambo zuri kwa Serikali kujenga Zahanati, Vituo vya Afya pamoja na *Dispensary* kwenye Wilaya na Kata zote Tanzania. Tuna vijiji 13,000 na Kata 2,500 au zaidi kama niko sawa.

Mheshimiwa Spika, hapa tutahitaji wafanyakazi wengi sana. Ni vizuri kujenga zahanati kama tulivyojenga mashule. Lakini tukumbuke kwamba walimu wanaenda kufanya, *teaching methodology* wanarudi wanakuja kufundisha walimu. Lakini hapa tuna *deal* na maisha ya watu. Lazima Serikali iweke mikakati madhubuti kabisa ya kuhakikisha kwamba tuna wafanyakazi wa kutosha. Mfano, kituo cha Afya kinatakiwa kihudumie watu 50,000 *Dispensary* watu 10,000. Kwa haraka haraka tu kituo cha Afya kinatakiwa kiwe na *clinical officers* watatu, *midwife* 8, *nursing officers* wanne. *Medical Assistant* mmoja. *Laboratory Technician* mmoja. *Pharmaceutical Assistant* mmoja na *Dental Surgeory* mmoja. Kwa haraka haraka tu ni wafanya kazi 19. Hapo bado sijazungumzia kuhusu *dispensary.* Kwa hiyo, Serikali iangalie vyuo vyetu, je, itakuwa na wafanyakazi wa kutosha katika kuhudumia hizi Zahanati. Na vile vile kabla hawajaanza kujenga hizi zahanati *epeciallly* kule vijijini, tuhakikishe kwamba nyumba za wanyakazi zipo, na vile vile hizi zahanati zikijengwa maabara zipate vifaa vyote. Sio kwamba tunajenga tu halafu *at the end of the day* unakuta tunaki na majengo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi naomba nizungumzie kuhusu elimu. Nimefurahishwa sana na hapa napenda nikipongeze sana Chama Cha Mapinduzi pamoja na Serikali kwa kuiga Sera nzuri ya CHADEMA kuhusu suala zima la elimu. Hii hapa Ilani ya CHADEMA Mheshimiwa Spika. CHADEMA tunasema tutaongeza elimu kutoka *9% to 35%* na CCM imefanya vizuri imefika 18% iwapo hawajafika kabisa. *(Makofi)*

Pamoja na hayo yote lakini tuna changamoto kubwa. Katika suala la elimu sasa hivi tumeona walimu hawana nyumba za kuishi, *especially* kule vijijini kama nilivyoongelea kwenye zahanati. Vijijini sio rahisi kupata nyumba za kupangisha, walimu wanapata shida sana, unamtoa mwalimu kutoka mjini Dar es Salaam unampeleka kijijini anafika kule hakuna nyumba. Nafikiri kitu cha kwanza kabisa ni kuangalia walimu wanapata nyumba za kutosha na vile vile zile maabara zilizotengenezwa katika mashule ziwe na vifaa vya kutosha huko tutapata mainjinia, tupata madaktari ambao watakuja kutibu kwenye zahanati ambazo zitafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa naomba nizungumzie suala zima la matumizi mabaya ya rasilimali za Serikali. Ni jambo la kusikitisha kuna gari namba SM 1457 la *Arumeru District Council* imekaa gereji kwa miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu atueleze *inventory* ya Serikali zinaangaliwa namna gani. Kwa sababu gari hii imekaa kule kwa miaka 15 inatakiwa ilipwe laki 800,000 tu mpaka leo sijui Arumeru wameiweka kwenye sehemu gani kwamba hili gari liko wapi na linafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba kwamba Kamati Teule iundwe ili kuangalia hii hujuma ya *BOT. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa napenda nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa ndugu na jamaa kwa msiba mkubwa uliopatikana Singida kwa ajali ya *bus* la Mohamed *Trnas,* pamoja na ajali ya *Land Cruiser* ambayo alikuwemo Mbunge wa zamani marehemu Stephen Kazi. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa bajeti nzuri aliyoiwasilisha wiki iliyopita. Kwa kweli naomba uniruhusu niseme Zakia oyee! *(Makofi)*

**MBUNGE MMOJA:** Oyee!

**MHE.DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo sasa niingie kwenye hotuba iliyo mbele yetu ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni kweli hotuba aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na hotuba za Wizara ambazo chini ya Wizara yake kwa kweli ni nzuri sana imeonyesha dira na mwelekeo wapi tumetoka, na vile vile imeonyesha dira na mwelekeo wapi tunakwenda ambayo ni nia thabiti ya kujiletea maendeleo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo sasa, naomba nijikite katika mambo kadhaa ambayo nimenuia kuyachangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naanza na suala la gari la zimamoto kwa Manispaa ya Singida.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima Serikali hii kwa Watanzania mwaka 2004 niliomba gari la zimamoto hapa hapa Bungeni. Kwa mapenzi makubwa ya Serikali kwa wana Singida tulipewa gari la zimamoto kwa kutengewa fedha kwa awamu mbili.

Awamu ya kwanza mwaka 2005 tulitengewa shilingi milioni 200 awamu ya pili 2006 tukatengewa shilingi milioni 165. Kitu cha kushangaza kuna watendaji ambao wana tabia ya ajabu kabisa, kwa kutaka kuidhalilisha Serikali yetu yenye mwelekeo mzuri, yenye kupenda watu wake, mtendaji alichukua hela milioni 165 akatumia kwa shughuli ambazo hazikulengwa na Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Matokeo yake mpaka sasa hivi gari la zimamoto Singida hatuna. Hebu niambie juzi hapa ajali ya *bus* la *Mohamed Trans* hivi kweli tungekuwa na gari la zimamoto tungeshindwa kweli kuokoa Watanzania waliopoteza maisha wote hao 25?

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alifika mapema kwenye tukio baadhi ya watu walikuwa hata hawajakata roho, wanapiga kelele wanamlilia, Mkuu wa Mkoa awaokoe.

Mkuu wa Mkoa kwa uchungu mkubwa alidondosha machozi kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kuwasaidia abiria hao waliokuwa wanaungua humo ndani.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Serikali yetu tutaendelea kuipaka matope mpaka lini kwa Watendaji wa *design* hii ambao wanachukua madaraka mkononi, wakati wanaelewa kabisa kabisa taratibu za fedha, wanatumia pesa bila hata vikao halali vya Halmashauri.

Naiomba Serikali iwatazame kwa macho mawili watendaji wa namna hii kwa sababu wanachelewesha maendeleo yetu, wanarudisha nyumba huduma za Serikali kwa tabia ambayo wanaifanya kwa maslahi yao binafsi. Naomba sana sana kwa shilingi milioni 200 zilizobaki benki huko Singida ninaiomba Serikali ifanye kila liwezekanalo watuongezee pesa tuweze kununua haraka gari la zimamoto. *(Makofi)*

Kwa sababu matukio ya zimamoto Mkoa wa Singida sasa yamekuwa mengi. Tuliunguliwa Ofisi ya CCM Wilaya, tukaunguliwa *Stand* yetu, leo *bus* la *Mohamed Trans* tuliunguliwa nyumba kubwa ya mfanyabiashara yote haya ni matukio ya kutisha ambayo yanahitaji yatazamwe kwa jicho la huruma kabisa kabisa ili tuweze kupata gari la zimamoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hilo sasa, naomba niongelee suala la ujasiriamali. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa jinsi anavyowajali wajasiriamali mpaka akaamua kupeleka bilioni 1 kwa kila mkoa.

Lakini hivi huu usiri wa mabenki yetu unatoka wapi? Kwa nini mara zote wanakuwa wakikiuka taratibu ambazo waliwekeana mkataba na Serikali? Hata Mkuu wa Mkoa akiomba taarifa ya wajasiriamali ambao tayari wamekwishakopeshwa anaambiwa hii ni siri kubwa. Ma-*DC* wakiomba wanaambiwa hii ni siri kubwa. Ni siri gani hiyo? *(Makofi)*

Tunataka kujua ni wajasiriamali wangapi wamekopeshwa katika mikoa yetu na Wilaya zetu ili angalau hata sisi wana siasa tunapohubiri kwenye majukwaa tutoe mifano halisi kwamba kwa sasa *SACCOS* fulani na fulani tayari imekwishakopeshwa.

Tunashindwa kutoa hata mifano. Kila tukiongea tunaambiwa hakuna aliyekopeshwa, inawezekana kweli ziko *SACCOS* ambazo zimekopeshwa lakini takwimu hatunazo. Tunaomba sana sana tena namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa na jitihada kubwa ya kuitisha hawa Mameneja wa Benki hizi kujadiliana nao mara kwa mara.

Ninaomba basi waheshimu yale majadiliano wanayojadiliana na Serikali ili hili zoezi la kutoa mikopo kwa wajasiriamali liweze kwenda vizuri, watu waweze kupata huduma, angalau tujue kwamba kelele za wanasiasa kwenye majukwaa kuhimiza wajasiriamali limefanikiwa kwa kiwango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea hilo naomba nizungumzie suala la kugawa Wilaya za Mkoa wa Singida. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Singida ametueleza kwamba Mkoa wa Singida kiuchumi ni wa mwisho kati ya Mikoa yote 21 Bara. Nimekaa natafakari, nakosa majibu, kulikoni Mkoa wa Singida uwe mkoa wa mwisho. Kuna sababu gani za msingi zinazopelekea Mkoa wa Singida uwe wa mwisho kiuchumi?

Lakini ukitazama sana wana Singida ni wakulima wazuri, ni wafugaji wazuri, ni wafanya biashara wazuri, lakini kinachokosekana hapo ni maelekezo ya watendaji wetu wa Serikali, Singida ni kubwa. *(Makofi)*

Watendaji wetu, hata ukimchukua Mtendaji wa Kata, unakuta Kata ina kilometa za eneo 1,500 hana hata baiskeli unategemea Mtendaji huyu atazunguka kuhimiza maendeleo, au bwana shamba, atazunguka kuelimisha wakulima wake walimeje? Ninaiomba sana Serikali, Singida ni Mkoa wenye wakazi wasikivu kabisa, wana nidhamu. Na wanaitii Serikali yao.

Ninaomba sana sasa, kwa kuwa Wilaya za Singida toka enzi ya uhuru mpaka leo haijagawanywa, naomba ipewe kipaumbele, ninaamini Wilaya hizi zikigawanywa, hata watendaji wataweza kumudu kuelekeza wananchi, wataweza kutembelea wananchi kwa sababu watakuwa na maeneo madogo. *(Makofi)*

Nikitoa mfano mdogo tu, Kata ya Rungwa peke yake ukubwa wa Kata ya Rungwa ni sawa na Wilaya ya Siha, hivi kweli jamani mnatutendea haki? Kuna haki hapa? Wilaya ya Manyoni peke yake ni sawa na Mkoa wa Kagera, hivi kweli mnatutendea haki?

Ninaomba sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu tunaipenda, tunaithamini, na ndiyo maana tulimchagua Mheshimiwa Rais, kwa kishindo. Mtutazame wana Singida kwa jicho la huruma. *(Makofi/Kicheko)*

Wilaya ya Manyoni igawanywe iwe wilaya mbili. Kwa maana ya Manyoni na Itigi. Singida nayo hivyo hivyo, tuwe na Wilaya mbili, kwa maana ya kila jimbo kwa maana iwe na Wilaya yake kadhalika Wilaya ya Iramba. Mkifanya hivyo, mtatusaidia kuinua uchumi wa Singida, watendaji wataweza kufanya kazi zao vizuri kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana katika Bajeti, kilimo kimepewa kipaumbele, napongeza sana na vile vile ndani ya kilimo cha umwagiliaji kimeainishwa humo ndani, na sisi Singida tumeainsha *scheme* za umwagiliaji 22 toka mwaka jana, tulitengewa fedha za *scheme* kama tatu. Ninaomba sana katika *scheme* hizi tulizoainisha na sisi tukumbukwe tutengewe pesa za kutosha, nina amini *scheme* hizi endapo zitafanyiwa kazi itakuwa ni chanzo ama ni chachu ya kuinua uchumi wa Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea hilo, niongelee habari ya barabara, Manispaa ya Singida ina barabara fupi na ndogo tatu tu pale mjini kati, wafanyabiashara wetu wamezungukwa na barabara za vumbi. Biashara zao zinatimuliwa vumbi kwa sababu hakuna barabara zenye kiwango cha lami, naomba sana, kwa sababu hakuna barabara zenye kiwango cha lami, naomba sana Manispaa ya Singida ikumbukwe kutengewa fedha kwa ajili ya kuweka barabara za lami angalau zile tatu zilizobakia pale mjini kati, ili angalau hadhi ya Manispaa ionekane na siyo barabara tu, hata taa. Ukiingia Mjini Singida usiku ni giza nene, wale Watanzania wenye tabia mbaya wanajifanyia shughuli zao bila wasiwasi kwa sababu tuna taa mbili tu ukitoka kwa Mkuu wa Mkoa barabarani mpaka hospitali ya Mkoa, mji mzima ni giza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba haya kwa heshima kabisa kwa huruma zote tukumbukwe na tufikiriwe ili na sisi Manispaa ifanane na jina la Manispaa.

Baada ya kuongelea hilo naomba nionglee kuhusu posho za Madiwani, naipongeza Serikali kwa kutambua hilo, napongeza sana, Serikali imeongeza kutoka shilingi 30,000 mpaka 60,000. Lakini mimi naona hata hiyo sitini bado ndogo angalau ifikie laki, angalau Diwani anapoenda kuchukua akunjiwe hata laki moja apewe, pamoja na maombi kuongeza kufika laki vile vile Serikali mnaoneja kama hili jukumu la kutoa posho za Madiwani lingebebwa na Serikali kwa kutoa ruzuku. Ni Halmashauri ngapi zenye uwezo hivi nikiangalia Singida, Iramba, Manyoni na Manispaa hivi wataweza kutoa hata hii sitini kweli?

Naomba Serikali itazame hii madhali imeshaonesha huruma kwa Madiwani, basi ione pia huruma kwa Halmashauri zetu ambazo hazina uwezo basi muone uwezekano wa kutoa hizi posho za ruzuku ili Madiwani hawa wasije wakapata shida Wakurugenzi wataanza kulaumiwa kwa sababu watashindwa kutimiza lengo la Serikali. *(Makofi)*

Lingine ni kuhusu Makaimu Wakuu wa Idara, mimi kwenye Kamati ya *LAAC* niliona Halmashauri nyingi wakuu wa idara unawaambia ni kaimu, mfano Daktari Kaimu, Mhandisi Kaimu sijui bwana nani Kaimu, hivi tutafanya kazi na Makaimu mpaka lini? Mtendaji ana Kaimu mpaka miaka mitatu, mitano, hivi kama kweli tumeshaona ana uwezo sasa asithibitishwe kama ana sifa na kama hana sifa kwa nini msimuondoe mkampeleka kuwa Mkuu wa Idara, nina hakika hizi Halmashauri zinazoendeshwa na Makaimu, Kaimu zinachelewesha maendeleo, kwa sababu Makaimu siku zote hawana hakika ya nafasi hiyo, anajua kabisa kiti hiki sio changu, ni kesho nitaondolewa. Naomba sana Serikali tuwaondoe Makaimu, kama wana uwezo tuwathibitishe ili waweze kufanya kazi kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *value for money,* ni kweli Serikali inaendesha miradi ya maendeleo inapeleka pesa nyingi lakini si miradi yote inayotekelezwa kwa kiwango kinachofanana na pesa iliyopelekwa, naiomba Serikali, itazame utaratibu mzuri wa kufuatilia miradi hii, ili watendaji waweze kuitelekeza kwa kiwango kinachotakiwa. Miradi mingine inatekelezwa kwa viwango vya chini, unakuta

jengo limejengwa, ukigusa hivi linapukutisha mchango, unakuta mfuko mmoja wa sementi unafyatua matofauli 50.

Mheshimiwa Spika, wakati utaratibu ama kiwango kinachotakiwa sio hicho naiomba Serikali ikifanya hivyo miradi yetu yote ya maendeleo kwa wanayopewa wakadarasi ama tunayofanya sisi wenyewe itakuwa ya kiwango na itatumika na itadumu kwa miaka mingi. Si vizuri miradi hiyo hiyo kurudia rudia kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya napenda nitumie nafasi hii kuunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda kutoa pole kwa wale wote waliopata ajali ya *Mohamed Trans,* na kupoteza maisha yao, naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Aminn.*

Pili napenda kutoa pole kwa wale wote waliopata ajali kwenye gari ya *Land Cruiser,* akiwemo Mbunge Mstaafu Mheshimiwa Steven Kazi, napenda Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi na wafiwa awepe subira. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi napenda kuchangia katika eneo la ujenzi wa Taifa, ni kweli kabisa Serikali imewaeleza wananchi tusaidiane kwa kutumia nguvu za wananchi katika kujenga shule, kujenga zahanati na kujenga mabweni. Lakini kitu ambacho kinanipa wasiwasi, ni pale watendaji wanapochangisha michango hii kwa kutumia risiti ambazo hazina nembo ya Serikali au ya Halmashauri husika, je, pesa hizi zina uhakika upi, kwamba pesa hizi zinazochangwa na wananchi zinafika mahali husika na wana uhakika upi, kama hawa watendaji hizi risiti wanazotumia ambazo hazina nembo ya aina yoyote ile zinafikisha pesa hizi za wananchi katika michango hiyo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hilo ningependa Serikali itueleze ni kwa nini fedha hizi zisichangishwe kwenye risiti zenye nembo ya Halmashauri ya Mji au nembo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa juhudi zake zote anazozifanya ana haki ya kushukuriwa na kusifiwa. Lakini kuna baadhi ya watendaji Wilayani wanamuangusha Waziri huyu, unakuta mtoto amechukuliwa kutoka Wilaya nyingine Dodoma, amechukuliwa kutoka Arusha anapelekwa Mkoa wa Kagera au anapelekwa Mkoa wa Kigoma, lakini wale watendaji kabisa wazi kwamba hawa watoto wametoka Wilaya mbalimbali na nyumbani kwao na sasa hivi wanahitaji kupata mshahara wakati husika. Lakini ukija kumuuliza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anahangaika sana na kutaka kuwasiliana na watendaji.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Serikali kupitia kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamsaidie Mheshimiwa Waziri huyu kufuatilia ni kwamba pesa za mishahara ya watoto hawa inakwama wapi na hasa watoto wa kike sasa hivi wanakuwa hawana msimamo, tunalalamika hapa watoto wanapata mimba zisizo za msingi, lakini kichocheo kimojawapo kama mtoto umemtoa mbali na kwao na umempeleka kufanya kazi eneo la mbali na amekubali katika mazingira hayo. Ni vipi mtoto huyo na mshahara wake umeshatumwa, asipatiwe kwa wakati muafaka? Tunaiomba Serikali ili imsaidie Mheshimiwa Waziri huyu na juhudi yake iendelee ikionekana machoni kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine, ambapo suala hili limeongelewa na Wabunge wengi, ni mikopo, uwezeshaji. Huu mfuko wa uwezeshaji kama ulikuwa hauna mpangililio maalum ni bora usinge toka kwa wakati huu, wangeendelea kuuboresha ukatoka wakati ambapo kila mmoja angeweza kufanya shughuli za kupata mkopo huu bila malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianzia kwa mfuko huu kabla sijawalaumu watu wa mabenki, ninaanzia kwa Watendaji wa Kata, wanawake wamekwishaunda vikundi au vijana, wanawake wamejikithiri mitaji yao wakaieleta na kusema watengeneze Katiba, watoe pesa za usajili wasajiliwe. Lakini watakapofikisha kwa Mtendaji wa Kata, ataanza kuwazungurusha, atawaambia hii Katiba sio rudini mkatengeneze. Wanarudi wanakwenda wanatengeneza nyingine, anawaambia leteni mchanganuo, wanapeleka mchanganuo anawaambia huu mchanganuo sio mwnde mkafanye mchanganuo mzuri zaidi. Wanakwenda kwa wataalamu, akinamama hawa au vijana wanakwenda kufanyiwa mchanganuo wakija wanauliza mmefungua akaunti, tumefungua, tunaomba haya mwende mpaka kikao cha Madiwani kitakapokaa mwezi ujao. Sasa hii inaonesha hali halisi ya huyu mama ambaye umemwambia kwamba unataka kumuondole umaskini, ni kiasi gani ambavyo unampa usumbufu na anaona hata ile pesa yake angeiingiza kwenye hiyo michanganuo, asingeingiza kwenye Katiba ni bora ile pesa yake angeendelea kuifanyia mtaji kidogo kidogo ingemzalishia, kuliko usumbufu huo anaoupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa Kata, katika hii ya mikopo wamekuwa kama miungu mtu, lakini utashangaa mtu mwingine anaandika maombi yake leo na anapeleka barua lakini baada ya wiki moja ameshajadiliwa amepewa, tunajiuliza kuna nini hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alitupa muongozo wa kwenda kusimamia mikopo hii na akatuambia Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe kwa muongozo huu wananchi wanapata mikopo hiyo. Lakini ni kwamba hajatusaidia ni kwamba sasa tumekuwa tunachonganishwa Wabunge na wananchi, wananchi wanatuambia Wabunge mnajua hizi pesa zimekwenda wapi. Wakati huo tukisema kuingilia kujaribu kwenda kuwaulizia wahusika kuhusu hii mikopo hatuwezi kutoa mikopo kwa sababu haina mdhamana, tutatoa mikopo kulingana na sheria za benki.

Sasa hapa kuna mambo mawili, tungeomba tueleweshe kwa sababu sisi ndio watetezi wa wananchi, kama vile Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alivyosema Wabunge tukasimamie wananchi wapate mikopo. Mtueleze kwa sababu watu mikopo hii hawajapata mpaka leo wengi, walio wengi kwa sababu nimezunguka mkoa mzima wa Mwanza tatizo ni hili, kila unapofika wanakwambia mikopo hii kapewa nani? Kila unapofika wanakwambia tunaomba utueleze ni nani anayeshughulikia mikopo hii kwa sababu tumeshasumbuliwa na Watendaji mpaka tumechoka. Lakini kulingana na hoja ya Mheshimiwa Grace Kiwelu, jana leo nimepata jibu ambalo Mheshimiwa Grace Kiwelu alisema kwamba mikopo hii imetolewa kisiasa. Tunapofikia kwenye mambo ya maendeleo ya jamii au mambo ya maendeleo ya watu tusiangalie itikadi za siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema amepewa kura hata na Wapinzani, kama Mheshimiwa Rais amewatambua Wapinzani ndio walimpa kura, je, hawa watendaji kwa nini wanabagua kwa itikadi za siasa? Hilo pia tungeomba tueleweshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninarudi katika suala la afya, labda kwa mawazo yangu mimi binafsi mimi ninaona sasa hivi kufikia huu mwaka 2008/2009 ni mapema sana tumewahisha kujenga zahanati yaani kujenga zahanati kila kata, kwa sababu moja, sasa hivi tunajenga shule za sekondari kwa nguvu za wananchi kushirikiana na Serikali. Wananchi hawa hawa tunawaambia tena tujenge maabara kwa kushirikiana nguvu za wananchi na Serikali. Wananchi hawa hawa tunawaambia tujenge hosteli kwa kushirikiana na nguvu za wananchi na Serikali, kwanza tujiulize wananchi wetu wa Tanzania wanakipato gani? Tukijiuliza na tukajua wananchi wetu wa Tanzania wana kipato gani tutapata jibu ni wapi Serikali iwasaidie au ni wapi Serikali ibebe jukumu zima bila kumshirikisha mwananchi.

Sasa tutakaposema tuanze kujenga zahanati, kwa sababu katika Kata moja ya Jiji la Mwanza, Kata ya Nyamanyoro, Mtendaji angalau wa Kata kidogo ameweza kupanga hata kwa mwananchi aweze kulipa taratibu hii pesa ya kujenga sekondari na anasema pesa hii italipwa kwa miaka miwili ina maana mpaka mwaka 2008/2009 pesa hii itakuwa bado wanaendelea kulipa. Sasa utakapokuja kumwambia tena achangie kitu kingine wakati kile hajakimaliza, inakuwa kwa kweli ni ngumu zaidi na wananchi wetu tunafahamu tunasema Tanzania ni nchi maskini, na maskini na wananchi wetu ni maskini pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tungeomba kwa suala hili la Zahanati lijidhatiti kwanza isijekuwa kama shule za sekondari ambazo shule za sasa hivi shule zimejengwa, wanafunzi wapo, walimu hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kurudi katika hali ya siasa, pamoja na kwamba wamesema kuna uwiano mzuri wa hali ya siasa na pia kuna matarajio mazuri ya hali ya siasa na siasa ikikaa sawa uchumi utaimarika na watu wataendesha shughuli zao. Lakini kwa hili mimi niko pembeni, hali ya siasa tunaielewe, pamoja na kwamba Chama Tawala ni CCM lakini hali kisiasa tunaielewa.

Mheshimiwa Spika, ni pale Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya au wa Mkoa anakuwa ni Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, suala hili linanipa wasiwasi sana, kwa sababu ulinzi wote ndani ya Kamati yake Jeshi la Wananchi wanamwakilisha, Jeshi la Usalama wa Raia wanamwakilishi, Magereza yumo, yaani vyombo vyote ambavyo vinalinda ulinzi na usalama mpaka Maafisa Usalama wa Taifa wamo ndani ya kikao hicho cha ulinzi na usalama na wote wako chini ya Mwenyekiti ambaye ni Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa.

Kwa hiyo, taarifa zote za mkoa anakuwa nazo yeye na yeye kwa sababu tumeelezwa wazi kwamba Mkuu wa Mkoa ni kada wa CCM hapa wa tunajenga siasa iliyo na uwiano? Na ni kwa nini Serikali sasa isitafute hivi vyombo vya ulinzi vya mkoa vikawa chini ya taasisi havijihusishi na siasa kama Jeshi la Wananchi au Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukienda hivi tutakuwa hatufiki pale tunapohitaji usawa na tutakuwa tukifika pale ambapo wengi wa wanachama tawala wanasema watatawala milele kwa hali hii ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nilimsikia Mbunge mzoefu akisema kwamba Wabunge wote ni sawa na wana haki sawa. Lakini ni kitendo cha kushangaza wakati mimi binafsi nikiwa na viongozi wangu wa chama na baadhi ya Wabunge tukiwa tumekaa tunaongea na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tunduru aliingia Mbunge mmoja wa Chama Tawala kwa mabavu yote na akataka kusema kwamba sisi hatuna haki ya kuwa kwa Mkuu wa Wilaya na kwa haki ya kuwa kwenye Kamati ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka amefikia Mbunge huyu kusema kudharau viongozi wa Vyama vya Upinzani, hii kwa kweli tunaona haifurahishi wala haileti maana, wala haileti mantiki, kama Wabunge wote ni sawa na yeye ajione ni sawa kama Wabunge wa *CUF* wa CCM, CHADEMA, *TLP, UDP* wote tuwe sawa na tuwe na uwiano sawa. Ila nafikiri ndio litakuwa wazo la busara kwa Mbunge mkongwe jana nimemsikia akiongea kitu kama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchangia suala moja, jana nimeuliza swali la kuhusu nyumba za milimani katika Jiji la Mwanza, jibu nililopewa na Naibu Waziri sikuridhika nalo. Ameniambia wale watu wamepewa namba, ni kweli wale watu wamepewa namba na zile namba walizopewa ni kwa ajili kulipia majengo yao. Sio zile namba walizopewa ni kwamba wako kihalali kabisa kwenye lile eneo na watakapotakiwa kuhamishwa ni lazima wafidiwe.

Sasa ningeiomba Serikali iliangalie upya suala hili na iweze kuwarasimisha kwa sababu imeshasema haiwabomolei, iliangalie upya suala na iweze kuwarasimisha kwa sababu imeshasema haiwabomolei, iweze kuwarasimisha wenye nyumba hao waliojenga kwenye miinuko ili hata kama Serikali itakapokuja kuamua kuwahamisha iwalipe malipo

yanayolingana na uhamishwaji wao, lakini si namba kwa ajili ya kulipia majengo hayo, ile namba ni kwa ajili ya kulipia majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba Serikali iangalie upande wa Mahakama kwa sababu katika kitabu cha Waziri Mkuu kimeongelea maeneo ya Mahakama. Ningeomba Serikali iangalie upande wa Mahakama na hasa mahakama za nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Nyumba kwa kuwa hazipitiwi mara kwa mara zimeshakuwa na ukiritimba na kesi bandia ambazo zinatoa hukumu bandia. Unakuja kukuta hukumu imetoka kwenye Mahakama ya Nyumba inapelekwa Mahakama ya Wilaya na inatolewa *order* ya kwenda mtu yule kutupiwa vyombo nje, wakati hakuitwa, hakupewa *summons* na wala hakupewa kitu chochote kile ili mradi tu anayemshitaki ni mtu mwenye uwezo au ili mradi anayemshitaki ni kigogo fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika sheria hizi na hasa nitamuomba Waziri wa Katiba na Sheria aingalie upya sheria ya Mahakama ya Nyumba ili iweze kutoa muongozo hata kwa maskini ambao pia wanahitaji kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa niongelee suala lingine katika maliasili, pale ambapo Serikali inapiga marufuku kitu fulani au inapiga marufuku misitu au inapiga marufuku kuchoma mikaa, hatukatai, kweli ni uharibifu wa mazingira lakini pale inatoa mianya kwa wale watendaji kufanya mambo wanayoyajua wao. Kwa sababu pale unapopiga marufuku kitu fulani, yule uliyemwambia kwamba asifanye kitu kile ili afanye inabidi kwanza aanze kutumia rushwa kuanzia chini huku anakokwenda kulifanya jambo hilo. Nitatolea mfano walipopiga marufuku ya kuchoma mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Mwanza, gunia moja la mkaa ni shilingi 35,000/= mpaka 30,000/= ukilipata kwa bei nafuu kidogo ni 28,0000/=. Baada ya kupiga marufuku ndio hiyo bei ilipanda kiasi hicho lakini kabla ya hapo gunia la mkaa lilikuwa linanunuliwa 16,000/=. Hebu tujifikirie huyu mwananchi wa chini aliyepigiwa marufuku ataweza kununua gunia la mkaa shilingi 30,000? Je, hii nishati mbadala tunauhakika gani Serikalini kwamba imefika mpaka huku kijijini au imefika kwa wale wananchi maskini wa hali ya chini. Wanatuambia tutumie gesi, mtu anatumia nyumba juu nyasi, chini nyasi atatumia gesi? *(Makofi)*

Sasa hivi Serikali tunaposema maisha bora kwa kila Mtanzania ni kila Mtanzania aweze kujimudu maisha, aweze kula, aweze kufanya shughuli zake na aweze kusomesha watoto wake. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie katika suala hili kwa kuwa nishati mbadala haijafika maeneo mengi ya nchi hii hata wakazi wa mijini na hata wakazi vijijini, tungeiomba basi izuie yale magogo na mikaa inayokwenda nje, ili wananchi wetu wenye kipato cha chini, wananchi wetu maskini waweze kujikimu kwa maisha yao. Kwa kweli wanasema tutumie umeme lakini umeme hautumiki. Mwananchi wa kawaida una taa moja, unawasha taa yako chumbani unaletewa bili ya umeme shilingi 30,000/= kwa taa moja hujaweka jiko hilo la kutumia umeme! Bado hujasema watoto wamekesha wanasoma, kwa hiyo katika hili mimi ningeona Serikali pia pamoja na kwamba watu wanaharibu mazingira izuie zaidi yale magogo yanayokwenda nje, kuliko kuzuia

matumizi ya ndani, kwa sababu nishati ya mbadala ya mkaa haijapatikana vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lililopita niliongelea hii sheria ya malezi ya watoto ambapo baba na mama wanaachana, na nikamuomba Waziri wa Katiba na Sheria ajaribu kurekebisha sheria hii mapema. Lakini mpaka leo tunaingia Bajeti ya pili tumemaliza mwaka sheria hii haijarekebika, jana nimemsikia Naibu Waziri anajibu kwa wale watoto wa ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wapo na pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana naona kengele imelia ya pili.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Ili nisije nikasahau mbele ya safari toka mwanzo kwamba ninaunga mkono hoja ya Waziri Mkuu moja kwa moja. Kwa maana hiyo naunga mkono taarifa au maoni ya Kamati ile ya Katiba, Sheria na Utawala Bora nikiwa mmoja wa wajumbe. *(Makofi)*

Napenda nichukue nafasi hii ya mwanzo kumpongeza Waziri Mkuu na viongozi wote Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wengine wote walioshiriki katika kutengeneza hotuba hii ambayo ni fasaha na ina kina cha kutosha kabisa na ni pana na mtu ungeweza kuzungumzia muda mrefu kwa sababu mambo yake ni mengi sana. *(Makofi)*

Sasa kabla sijachangia nilichotaka kuchangia ningependa nirejee hoja aliyozungumzia Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Pascal Degera, jana kuhusu barabara ya Iringa, Dodoma, Manyoni kuweka lami. Katika hatua hii mimi sitapenda kusema maneno mengi, kwa sababu nadhani, Waziri wa Miundombinu atakuwa labda na maelezo ya uhakika na sahihi wakati wa hotuba yake baadaye mwezi ujao.

Kwa sasa naomba tu Serikali iweke uzito wote katika suala hili si la jana wala juzi ni zaidi ya miaka 12 tunahoji suala hili, lakini kumekuwa na danadana na jibu siku zote upembuzi bado, sijui mimi sijaona upembuzi unaochukua miaka yote hiyo upembuzi yakinifu.

Sasa mimi naomba jibu wakati hotuba ya Wizara ya Miundombinu itakapotolewa na kwa sasa naomba Wabunge wenzangu wa Mikoa hii ya kati, mikoa ya ile nyanda za juu, Mikao ya Kusini wote tutafaidika kama barabara hii itawekwa lami. Ningeomba sana katika michango yenu iwe ni hotuba hii ya Waziri Mkuu iwe hotuba za Mawaziri wengine wote, tusemee jambo hili na napenda Serikali ifahamu kwamba hakuna Mbunge

anayebisha suala hili katika mikoa yote niliyoitaja. Hebu tilieni maanani tupate barabara hii, si kwa faida ya sisi Wabunge tu lakini kwa faida ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitazungumzia mambo kadhaa yanayotokana na utekelezaji lakini nitajikita zaidi katika mambo mawili, kwanza nitazungumzia kile ninachokiona ni udhaifu katika mfumo wetu ambacho kinakinzana na dhana yetu ya kwenda kwa kasi zaidi katika maendeleo na pili nitazungumzia mambo ambayo yanaendelea hivi sasa yanayokwaza *speed* hiyo, tumesema na nashukuru Waziri Mkuu ametukumbusha jana kwamba sisi tunapaswa kukimbia badala ya kutembea. Sasa kuna vipengele fulani fulani nitakavyovitaja ambavyo vinakaza kasi hiyo tunayokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze na udhaifu katika mfumo wetu, kwanza niipongeza Serikali kukubali kutuhusisha sisi Wabunge katika mchakato wa Bajeti ulioanza mwaka huu. Nafikiri hili ni jambo nzuri sana na kwa kweli lilikuweko siku za nyumba wakati tulipokuwa tunageuza Bunge likawa *planning commission* wakashiriki katika mchakato mzima. Sasa tumerudia huko mimi nafikiri ni vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba Serikali ikamilishe mchakato huu katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, sisi huku kwenye Bunge kwenye ngazi ya Kitaifa mmeturuhusu kushiriki, lakini huko Wilayani kuna matatizo kwa sababu ya *sealings, budgeting sealings* kuchelewa kupelekwa Wilayani, kuna ucheleweshaji mkubwa sana kiasi kwamba sisi Wabunge tunashindwa kushiriki kule kwa sababu ni kipindi kile kile tunatakiwa kuwa hapa. Mimi nashauri Serikali itazame upya kwa lengo la kuhakikisha kwamba ushiriki wa Wabunge unaanzia huko tunakotoka ili tunapofika huku tuwe katika hali ya kuweza kutetea kile tulichoanzisha kule Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali iliyopo sasa hivi mambo mengi tunayakuta hapa na yanatoka hapa na yanatoka kule kule kwetu kwa sababu nini hatukuhusishwa, hatukuhusishwa kwa sababu ya mwingiliano wa hizi ratiba. Kwa hiyo, nashauri kwanza kabisa *sealings* ziwe zinatolewa mapema zaidi halafu iwe ni lazima *mandetly* kwa Wabunge kushirikishwa katika ngazi ya Wilaya na isiwe jambo la hisani kama ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya mfumo ambao mimi kwa maoni yangu nadhani unakwamisha kasi ya maendeleo, ningependa kusemea machache, kwanza naipongeza Serikali kwa kitendo cha kupeleka madaraka mikoani, rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa anasema *D by D means Decentrolization by devolution.* Hiyo ndiyo ilikuwa dhana ya Serikali kwa muda mrefu toka mwaka 1972 na najua hili kwa sababu mimi ndiyo niliyeongoza utekelezaji wa *decentralization* ndiyo ilikuwa dhana, lakini imeyumbayumba hapo katikati imesuasua, imebidi kufanya marekebisho hapa na pale na katika kufanya marekebisha hayo kuna sehemu imesahauliwa nayo mfumo wa pale mkoani.

Pale mkoani tumeunda kitu hakieleweki, tumefuta *defectal* kwa maana kwamba hatukutengeneza sheria, hatukufanya maamuzi lakini tumefuta wakuu wa idara,

tumewafuta tumewaita washauri. Sasa utekelezaji wake umekuwa mgumu sana na kwa kweli mimi nadhani ni wa kienyeji, chukua mfano *Regional Education Officer*, huyu kazi yake inatawaliwa na sheria ya elimu lakini utaratibu huu mpya unaomfanya awe mshauri na hatajwi katika sheria ya elimu utekelezaji wake unakuwa hauna msingi wa kisheria na kwa kweli ni wa kienyeji. Vivyo hivyo, wakuu wengine wa idara unamkuta Mshauri wa Shirika yeye katika Sheria ya Ushirika hakuna kitu cha namna hiyo, *DALDO* hivyo hiyo, *Regional Livestock Development Officer* hata *Regional Medical Officer* ni mshauri. Hawa wote hawana nguvu ya kisheria katika nafasi zao kama washauri.

Mimi nashauri kwamba kwa kuwa hii inaleta utatanishi na isitoshe kana kwamba hii haitoshi ni kwamba kumekuja utaratibu mwingine wa *cluster* yaani wanakusanywa baadhi ya hawa wakuu wa idara katika kundi moja sijui kwa lengo gani inaitwa *cluster*. Sasa hawa kwa sababu na wao wako katika mtindo uleule inakuwa ni utatanishi wa moja kwa moja.

Kwa hiyo, nashauri hasa kwa vile hakuna *link* kati ya hawa washauri na Serikali zetu za Mitaa hakuna *linkage,* haiwezi kuvuka mpaka aende kusaidia Wilaya. Kwa hiyo, mimi nadhani iko haja ya kutazama upya utaratibu huo mzima kwa sababu kama ninavyosema washauri hao hawana uhalali kisheria kutenda kazi zao na Serikali za Mitaa zina wataalamu wa taaluma mbalimbali sioni kwa nini hawa wasifanye kazi zao kama inavyotakiwa bila haja ya kuwa *linked* mahali pengine. Vile vile mfumo huu wa *cluster* mimi ningeshauri uondoke, hausaidii chochote bali ni mzigo tu na kwa kweli unaleta utatanishi zaidi. *(Makofi)*

Kuhusu mambo ambayo yanakwaza Mikoa katika utekelezaji wake, kwanza nina tatizo na mfumo huu wa kuwa na Kanda. Sisi kule Iringa tuko chini ya Mkoa mwingine Kikanda kwa hiyo tukitaka jambo fulani sharti tusafiri au tuwasiliane na hiyo Kanda kule Mbeya. Kwa hiyo, unaweza kutafsiri kwamba kuna Mikoa ambayo labda ni *super* kuliko mingine na kuna Mikoa ambayo ni ya kawaida, sasa hii Mikoa isiyokuwa na Kanda Makao Makuu ni lazima iende kwenye Kanda ambapo mara nyingi tunatakiwa tulipe gharama za malazi, usafiri na gharama za hao wtaalamu kuja kufanya kazi katika Mikoa yetu. Mimi nafikiri hii inaleta usumbufu licha ya kwamba inatuongezea gharama ambazo ni za ziada na Mikoa mingine haina. *(Makofi)*

Mimi naushauri mfumo huu uondolewe, kila mkoa uwe na *full compliment* ya raslimali watu, rasilimali fedha na ifanye mambo yake kikamilifu bila haya ya kutegemea Mikoa mingine ambayo mimi napenda kuiita ni ubaguzi ambao mimi nafikiri siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikiendelea na vikwazo hivi lakini kikwazo kingine ambacho ningependa kukitaja najua muda wangu umekwishapungua ni ucheleweshaji wa fedha kupelekwa Wilayani. Fedha ziwe za Bajeti yetu ziwe za nchi za nje sawa, lakini zinachelewa sana kwa sababu ambazo mimi sijazifahamu. Kwangu huko nina uzoefu, kuna fedha ambazo zimefika miezi miwili au mitatu iliyopita yaani mwezi mmoja au miwili kabla ya *financial year* sasa utekelezaji wake utafanyika saa ngapi?

Mimi nashauri Wizara yetu inayoshughulika na mambo haya ya Serikali za Mitaa ijiimarishe ili kusudi iwe na uwezo wa kutupelekea fedha. Kwanza ihakikishe upatikanaji wa fedha kwa wakati huko zinakotoka kama ni za nje au kama ni humu humu zipatikane haraka.

Pili ni kwamba wakishazipata ziletwe Wilayani bila kuchelewa kama ilivyo hivi sasa mfano mmoja mzuri labda kama muda utaniruhusu. Fedha za MMES kwa mfano zitoke Wizara ya Elimu, zije kule Hazina Ndogo, Hazina Ndogo hawawezi kutoa bila barua ya *REO* halafu zikitoka zinakwenda kwa Shule Mlezi sasa ukianza kufuatilia hii utachukua muda mrefu sana na maana yake ni moja tu kwamba utekelezaji unachelewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninafikiri kwamba iko haja kubwa sana ya TAMISEMI kujenga uwezo wa kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali na vile vile kujiimarisha kuhakikisha kwamba zinapofika pale hazichelewi tena.

La mwisho, nadhani ikiwa muda utaniruhusu ni kwamba kuna Kata nyingi ambazo hazina Madiwani hivi sasa na katika Wilaya yangu nina Kata mbili ambazo ni wazi kwa sababu ya vifo vya Madiwani walioshika nafasi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kata ya Ifunda na Kulanda pia zimekaa muda mrefu bila Madiwani, mimi naomba Wizara hii ichukue hatua za haraka sana kuhakikisha kwamba uchaguzi mdogo unafanyika chini ya kifungu cha Sheria yaani *Election Act*. Juzi juzi hapa tumepitisha Sheria ya kusema chaguzi hizi zifanyike ndani ya siku 20 hadi 50, tukiendelea namna hiyo itakuwa ni uvunjaji wa Sheria ambayo sisi wenyewe tumeitunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono kwa mara nyingine tena, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa sasa ni zamu ya Mheshimiwa Profesa Philemon Mikol Sarungi, atafuatiwa na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, wakati huo huo Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi, ajiandae.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na TAMISEMI. *(Makofi)*

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusoma hotuba yake kwa umahiri na kwa *speed and accuracy* kama ilivyo kawaida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni Bajeti ya utekelezaji ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ni Bajeti ya kazi imeandaliwa vizuri sana na inakidhi matarajio ya wapigakura wetu ambao wametuwezesha kuingia ndani ya Bunge hili na ninaomba tuipitishe kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja ya Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika Bajeti hii ni kutoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya itakayoanza rasmi mwaka ujao wa fedha. Napenda kutoa salamu na shukrani kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa kwa wananchi wa Rorya aliyoitoa mwaka 2005/2006 kuwa Rorya itakuwa Wilaya. Wananchi wa Rorya wamempa jina la mkombozi wa wananchi wa Rorya, wana imani naye, wana imani na Serikali yake, wana imani na Chama cha Mapinduzi, wana imani na Sera za Chama cha Mapinduzi. Wananchi hawa wameahidi kuwa raia wema na kwamba watatii na kuheshimu sheria za nchi, wataulinda Muungano wetu, watauliza Muungano wa nchi yetu na Umoja wa Taifa letu. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afikishe salamu hizi kwa Mheshimiwa Rais kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Rorya wanamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoshughulikia mchakato mzima wa uanzishaji wa Wilaya mpya ya Rorya kwa kufuata falsafa ya Serikali ya awamu ya nne kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Wamempa jina la bwana wa vitendo yaani yeye hana maneno mengi anafanya kazi yake kwa vitendo. Nasema ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaomba uendelee kuwa mlezi wa Wilaya changa ya Jimbo la Rorya. Wilaya hii ni kitinda mimba kati ya Halmashauri za Wilaya 11, ndiyo mtoto mchanga na wanakuomba uendelee kulea Wilaya yao kwa kushiriki katika harambee mbalimbali kama kawaida yako kwa kuchangia miradi ya Wilaya na watakukaribisha katika *harambee* hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waziri Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Naibu Waziri, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, wamefanya kazi nzuri sana na wamesimamia zoezi hili bila kuogopa na bila kuyumbishwa na kwa kufuata Sheria na walisimamia Sheria na Kanuni. Wamefanya kazi nzuri sana pale ambapo wengine hawakuelewa wamekuwa walimu na wameelimisha.

Lakini kama tunavyomfahau Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ni mtu wa kanuni, hataki kuyumbishwa yumbishwa. Walitokea wachache waliotaka kuleta maoni yao nje ya utaratibu ili maoni yao Mheshimiwa Mizengo Pinda aweze kukubali, hawa hawakuwa wawakilishi wa watu walikuwa ni watu wachache lakini nafurahi na wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya wanashukuru sana aliwatamkia neno moja *stop* na akawaambia wengi wamepewa ninyi wachache nimewasikiliza, nampongeza na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya pia wanamshukuru na kumpongeza Dada yao na mwanamama shujaa Mheshimiwa Celina Kombani amefanya kazi kubwa sana katika zoezi hili na wanamkaribisha aje aone Wilaya mpya ya Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya kumpongeza sana Mkuu wetu wa Mkoa,  Bwana Isdory Shirima na pia kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Manyoni ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Tarime, Ndugu Pastory Mabiti na Mkuu wa Wilaya wa sasa Ndugu Stanley Kolimba kwa kusimamia zoezi hili kwa ujasiri mkubwa na wananchi wa Rorya, wanathamini sana mchango wao na wameahidi kuwapa ushirikiano wote ili tulee Wilaya yetu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,  pamoja na kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Halmashauri na ofisi zake, wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya wanaomba yafuatayo, kwanza, wanaomba sana kuwa pamoja na ujenzi wa majengo ya Halmashauri ya Wilaya ujenzi wa hospitali mpya pia ianzishwe mara moja. Tulikuwa na hospitali moja katika Wilaya ya Tarime, wananchi wanaoishi Kibui, Nyamagaro, Sota, Kirongwe walikuwa  wanateseka sana kufuata huduma katika Hospitali ya Wilaya, wengine walikuwa wanapitia nchi jirani kutokana na ubovu wa Barabara kwa hiyo ujenzi wa barabara uanzishwe sambamba na ujenzi wa Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wanaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanakufahamu na wanakuheshimu, ulipokuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Maji uliwasaidia sana kupata malambo sita na bado wanakumbuka sana na wanajua utawasaidia, wanaomba magari ya *Ambulance* ya kuwahudumia wagonjwa. Najua unaweza uwezo wako ni mkubwa, angalau hata moja basi. Kituo cha afya ya Kinisi hakina gari, Nguga pia hakuna gari sasa Halmashauri ya Wilaya mpya pia haina gari na haitakuwa na gari, wanakuomba ili tuokoe uweze kuwapatia magari hayo matatu na kama haiwezekani angalau hata moja ili tuweze kuokoa maisha ya akina mama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi ambalo pia nataka niweke kwa Waziri Mkuu na kwa Serikali ni kuhusu ujenzi na ukarabati wa barabara 15 za Wilaya na barabara 12 za vijiji. Ombi hili na zoezi hili mpango huu upewe upendeleo maalumu, natoa shukrani kwa TAMISEMI  kwa kazi kubwa waliyoifanya katika ujenzi wa barabara lakini kazi bado ni kubwa kwa hiyo ni matumaini ya wananchi wa Rorya ujenzi wa barabara hizi 15 za Wilaya na 12 za vijiji itakamilishwa pamoja na ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi pia wameomba kuwa miradi inayoendelea kwa sasa ambayo ameshaanza na ambayo ataanza miradi kama ya maji, umeme, mabwawa, malambo, majosho, kilimo cha umwagiliaji na MMES kwa kuwa Wilaya yetu ni mpya miradi hii isimamiwe vizuri na ipate msukumo mpya na upendeleo wa pekee.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wananchi wa Wilaya ya Rorya wanaomba kwamba zoezi litakapoanza wataajiriwa watumishi wapya wanaomba zoezi hili katika kuwaajiri watumishi wapya lifanywe kwa uangalifu mkubwa na kama ikiwezekana hata wastaafu wenye uzoefu waajiriwe ili waweze kuweka msingi imara. Maana tukianza vibaya na watumishi ambao hawatamudu tutakuwa tumejichimbia kaburi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema leo ni siku ya furaha wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya wakati wananiona wanasherehekea kweli kweli. Mwaka 2006 tuliomba

tupatiwe Wilaya, mwaka 2007 tumepata Wilaya ni ndoto na miujiza. Kwa hiyo, kwangu ni furaha, sina maneno mengi ya kusema na nitachangia kwa maandishi baadhi ya mambo yaliyomo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini kwa leo narudia kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais mkombozi wa wananchi wa Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Chacha Wangwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, wakati huo huo Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii hoja ya Waziri Mkuu na pia natanguliza shukrani kwa ofisi hiyo ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe na Mawaziri wake kwa jinsi ambavyo wameelekeza macho yao katika Wilaya ya Tarime kipindi hiki. *(Makofi)*

Mimi najiunga na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi kuipongeza Serikali kwa kutupatia Wilaya nyingine katika Tarime na kutupunguzia mzigo mkubwa tuliokuwa nao kama Halmashauri maana yake tuko moja ya Halmashauri kubwa sana hapa nchini yenye Madiwani 60 ambapo hata mjadala ulikuwa hauendi, tunaishia kugombana sana, lakini sasa nashukuru Tarime itakuwa na Halmashauri yake yenye Madiwani kama 20 ambacho ni kiwango kizuri kwa mjadala. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kutoa pole kwa wale wote waliopatwa na ajali huko Singida mara mbili, pia Mbeya na Arusha kwa kweli inatisha sana jinsi ambavyo viwango vya ajali vinaongezeka hapa nchini, lakini ningependa kutoa ushauri kwa Serikali ya kwamba tatizo kubwa ni barabara. Barabara zetu ni finyu sana ukiangalia hata barabara ya Dar es Salaam – Dodoma ni barabara nzuri lakini ni finyu mno, malori makubwa, mabasi, punda, mikokoteni, baiskeli na hata gari ndogo, kwa hiyo, barabara za aina hii ni lazima zilete ajali na kwa hiyo, tungeomba Serikali ipanue barabara na pia kuimarisha barabara za kati ya nchi kama ile ya Singida ili sisi wengine tusiwe tunazunguka nchi za jirani kuja hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukalaumu wapiga debe, madereva na vile vile mpaka hata polisi, lakini mimi nadhani tatizo kubwa ni kwamba barabara ni nyembamba mno. *(Makofi)*

Tatu naendelea kuipongeza Serikali kwa kuchukua hatua dhidi ya wale Askari Polisi waliofanya mauaji kule Tarime na lile tukio limepongezwa sana na wananchi na ninafikisha salamu zao kwamba kwa mara ya kwanza sasa Serikali inaanza kushughulikia tatizo hilo ambalo ni kubwa sana, lakini hii ni nzuri isipokuwa wanahoji ya kwamba kwa nini wasipelekwe Mahakama ya kawaida mpaka wapelekwe Mahakama ya Kijeshi. Ingawa mmoja amelala mbele na wawili wamekamatwa lakini hii ni ishara nzuri sana na polisi watajua ya kwamba kuna Sheria na Sheria ni msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuendeleza mchezo wa soka kwa kweli kipindi hiki kumekuwa na juhudi kubwa sana kwa upande wa Rais wetu na Serikali na Wizara hiyo ili kuhamasisha wananchi washiriki katika soka na vijana kufanya bidii. Isipokuwa kitu ambacho mimi sikuelewa sawasawa ni kwa nini ilibidi ya kwamba mpaka hiyo Timu ya *Taifa Stars* iletwe Bungeni kwa ajili ya kupongezwa wakati ambapo hawajaleta Kombe. Sisi tulikuwa tunatarajia walete Kombe kwanza lakini lile goli moja basi sawa ile nadhani inabidi waongeze bidii. Mimi siyo shabiki sana wa soka, mimi napendelea ngumi, kupiga ngumi na wale wa michezo mingine kama ngumi vile vile waangaliwe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi mimi naelekea sasa kuzungumzia suala la kiutendaji hapa Bungeni, kwa kweli mimi ni mfuasi wa sera ya Spika ile ya *Standards and Speed* kwa sababu hiyo ndiyo sera inayotumika dunia nzima na kwa sababu sasa hivi ni *speed age* kwa hiyo, katika watu kufanya *speed* nadhani ya kwamba hapa Bungeni kuna *confusion* kidogo katika *standards*. Tunapokuwa tunazungumzia Ilani kwa sababu Ilani mimi naona kila wakati Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanaongelea Ilani, kila mahali Ilani. Lakini Ilani jinsi tunavyoifahamu ni kitu kinachoitwa *Election Manifesto* inatumika tu wakati wa uchaguzi na itazungumziwa wakati wa uchaguzi mwingine, kinachotakiwa kizungumziwe hapa ni *policies* yaani tuzungumzie sera kwamba sisi kama Wabunge tunafanya mijadala ya kuboresha sera za Serikali wananchi wafaidike lakini kila wakati wakisimama Waheshimiwa Wabunge wa CCM wanaongelea Ilani, Ilani. *(Makofi)*

Lakini ile Ilani pamoja na kwamba inaabudiwa zaidi ya Mungu, mimi sioni ya kwamba ina umuhimu sana kuzungumziwa hapa Bungeni. Kwa hiyo, kwa viwango vya Bunge nadhani wangepunguza haya masuala kwa sababu kama Chama cha Mapinduzi kinatawala nchi kila mtu anajua kwamba ndicho kinachotawala. Simba akiingia kijijini wale wanakijiji wanajua Simba yupo hapa kijijini siyo lazima azunguke aseme mimi ndiyo Simba. Kwa hiyo, inaonyesha kwamba wana hofu na hofu yenyewe inatokana na kwamba mambo mengine ambayo tunayafanya hapa siyo yale ambayo wananchi wametutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sisi Wabunge wa upande wa Upinzani kwa mujibu wa Katiba hamuwezi mkatuzuia tukaingia hapa Bungeni wala hamuwezi kutuzuia kuzungumza, ni wajibu wetu kwa hiyo, siyo kwamba mpaka mtushambulie sana ili tukitaka kusema ukweli mnatushambulia kabisa kwa jazba. Lakini kule wananchi wanaona, wanaona ya kwamba sisi tunafanya kazi yao. Kwa hiyo, angalieni sana hili suala litakuja kuwagharimu huko mbeleni kwa sababu wananchi wanaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi mimi ningependa kurudi sasa katika kuzungumzia suala la hii hotuba ya Waziri Mkuu, ni kweli amezungumzia mambo mengi lakini nadhani kimsingi Bajeti nzima kuna kasoro ambazo ni za msingi hasa, nimeshawahi kuzungumza na Mheshimiwa Aggrey Mwanri akanijibu hapa kwamba Serikali hii inafuata mfumo wa kijamaa. Lakini nadhani kuna *confusion* katika kitu kinachoitwa *model of production,* hii ni muhimu sana tuangalie kwa sababu kuna mifumo ya uchumi duniani inayojulikana kama ni mfumo wa ujamaa lengo lake ni *production* yaani uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni mfumo wa kibepari vile vile ni *production,* sasa katika *production* mimi naona Bajeti yetu haijazungumzia suala la kuinua uzalishaji na tunavyofahamu ni kwamba sekta kubwa hapa ni sekta ya kilimo lakini sekta ya kilimo haijaangaliwa kwamba *production* iongezeke ili tuweze kuuza zaidi na wale wanaofuata mfumo wa kibepari wanaelewa kwamba kuna *balance of payments* na katika *balance of trade*. Sasa tuangalie uwiano kwamba tunazalisha vitu ili tuuze zaidi nje halafu tu-*import* vitu vichache, lakini kama tume-*import* vitu vingi kwa gharama kubwa na uzalishaji wetu ni mdogo mno kiasi kwamba hata nchi kama Mauritius inatuzidi na ukiangalia kilimo chote sasa hivi kime-*collapse* tunategemea tu zile zinazoitwa *Extractive Industries* yaani Viwanda vya Kukwangua kama vile Madini na Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini na huu ndiyo mzigo mzito ambao wananchi wa Kanda ya Ziwa wanalia nao na wanatafakari na ni lazima watachukua hatua katika uchaguzi ujao kwamba sisi tunachangia uchumi wa Taifa kwa kiwango cha 47% hayo ni madini ya Dhahabu, Almasi na kadhalika na Samaki zinakuja kama 58% yaani watu wote Tanzania sasa wanakula juu ya migongo yetu, watu wa Kanda ya Ziwa. Sasa hii inaonyesha wazi kabisa kwamba tunaumizwa sisi kwa sababu sisi ndiyo tunaolisha hili Taifa lakini ndiyo ambao hatupati mgao wetu unaostahili yaani hatuna barabara, shule na hata hospitali kwa hiyo, ni lazima tutahoji kwamba sasa mbona hakuna uwiano wa kugawana mapato ya Taifa? Hii inatokana sasa na kwamba *planning* ina tatizo.

Mimi katika mipango sijui kama kweli watu wako *serious* kwa sababu kama tungeongeza juhudi za kuinua uzalishaji hii ingeenda sambamba na kutengeneza barabara ili uchukuzi uwe rahisi kwa sababu masoko ya ndani yapo na yanazidi kukua na masoko ya nje vile vile.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Wilaya yangu kwa mfano kuna Kampuni ya kuchimba dhahabu wao hata kuku wanatoka Ulaya na hata nyanya zinatoka Afrika Kusini wakati watu wa pale pale wana uwezo wa kuweza kuzalisha vitu kama hivyo. Lakini nadhani *planning* katika suala la uzalishaji ndiyo lingeangaliwa ili sasa hii Bajeti ambayo tumeipitisha hapa isije ikawa ni Bajeti kama ile ya kuzalisha au kuku-*inflation* kiwango cha kule Zimbabwe. Ile *system* ya Zimbabwe mnafahamu sasa hivi tatizo kubwa jinsi ambavyo imekuwa lakini pamoja na ukali ni kwamba *inflation* ikiisha kuwa kubwa na bei ya vitu ikaongezeka wananchi watazidi kuumia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba ya kwamba katika hoja hii ya Waziri Mkuu atusaidie kuangalia hili suala la kwamba tutaongezaje uzalishaji kule vijijini na tunawezaje kuongeza uzalishaji bila kutengeneza miundombinu ya barabara ambayo ni kwamba uchukuzi uweze kuwa mzuri wa kupeleka mazao kule yanakohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kugusia ni kuhusu ile michango. Michango ile ambayo imekuwa sasa ni ya lazima mimi nadhani Serikali inawajibika kuchukua kodi na kuitumia katika maendeleo, awamu ya kwanza ilikuwa inafanya hivyo, awamu ya kwanza ilikuwa inahimiza wananchi vijijini lakini pia ilikuwa inatoa shule na kusomesha watoto hata sasa hivi watoto wamekuja hapa kutoka vyuo mbalimbali wako hapo nje wanasubiri kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge

wamezuiliwa kufanya mitihani. Sasa hii inaonyesha ya kwamba Serikali haijatimiza wajibu wake wa kuchangia maendeleo kwa kutumia kodi katika kujenga shule, hospitali na kadhalika. *(Makofi)*

Sasa hizi fedha za michango ya lazima ambazo zimejenga shule 1,084 tunataka ya kwamba kwenye hii Bajeti zionekane ya kwamba hizo fedha kwa sababu zimehimizwa na Serikali. Kwa hiyo, tuone ya kwamba hao ni wahisani wa ndani kwa hiyo, kama wahisani wa nje wanatoa 42% basi hawa wa ndani nao tujue kwamba wametoa kiasi gani kwa sababu ni mabilioni yamechangwa na mengine yamefujwa na sasa tunasema huo mpango utakuwa endelevu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ina maana kwamba wataanza kujenga hospitali, sasa Serikali imeacha mzigo wake kabisa, imeuweka kwa wananchi. Kwa hiyo, tuelewa kwamba hao wahisani wakishalipa kodi, maana kodi wameshalipa kwa mpango wa *VAT* na kila mtu analipa, lakini sasa wanazidi tena kuambiwa wajenge vitu ambavyo ni wajibu wa Serikali kuvijenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili lieleweke wazi kwamba ni kiwango gani sasa ambacho kimechangiwa tayari cha hizo fedha, kwa sababu siyo fedha za Serikali ni fedha za wahisani wa ndani. Halafu kama ni wahisani wa ndani sasa wao hiyo ni kodi au kama siyo kodi basi ieleweke kwamba wametoa msaada kwa Serikali na Serikali kama imeshindwa sasa kufanya juhudi zake cha kufanya ni kujiuzulu ili wananchi wachague Serikali nyingine. Kwa sababu Serikali imeshindwa kutimiza wajibu wake.

La mwisho, ningependa kuzungumzia kuhusu kashfa ya *BOT,* sisi tutaendelea kuizungumza na tutawaelimisha wananchi pamoja na kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine wakongwe hapa wanakuwa wakali. Lakini hiki ni kitu ambacho kimeonyesha wazi kwamba Serikali imeshindwa kusimamia matumizi yake, fedha zinafujwa ovyo na hizo fedha inaonekana kabisa kwamba njia yake ndiyo hiyo, imeonekana wazi, dunia yote inajua, angalia hii *e-mail* hata mimi nimetumiwa kutoka huko Ulaya sijui. *(Makofi)*

Sasa angalia kuna *group* la watu hapa ambao wanaonekana kama wao ndiyo wameajiri Baraza la Mawaziri. Inaonekana kabisa kwamba Baraza la Mawaziri sasa wao wanawasikiliza hao Wahindi au tuseme wananchi ambao wengine siyo Watanzania, lakini wana asili hiyo ya Kisia, sasa ndiyo wanaendesha hii Serikali. Hili suala tutaendelea nalo na watu vile vile watatusaidia kutupa majibu. Halafu ningewashauri Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wawe wakweli, tunafahamiana hapa kwa dhamira, mnapenda haki. Lakini hii ya kusema asilimia fulani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, hakuna ushahidi wowote wa Serikali yetu kuendeshwa na hao unaowaita Wahindi. Naomba ulifute hilo. Inawezekana kuna watu wanakula rushwa, lakini kusema Serikali inaendeshwa na watu fulani, hilo siyo sahihi. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, haya naliondoa ili lirudi katika eneo la utafiti. Kwa sababu mimi ni hisia yangu ilikuwa lakini naliondoa. Ahsante kwa kunipa huo mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ila ningependa pia Serikali yetu iangalie mambo ya utawala bora. Lile suala la kutumia ubaguzi Katiba inakataa, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wote, eti wote wanatoka Chama cha Mapinduzi. Halafu Katiba inakataa kwamba tusibaguliwe ukiisoma, hakuna kubagua Mtanzania yeyote. Sasa hii inaonyesha kwamba suala la ubaguzi hapa tunakiuka Katiba kama tunapendelea kwamba hao watokane tu na Chama cha Mapinduzi. Kuna wananchi wangeweza kutoa hata michango yao kwa njia nyingi za utawala bora hapa nchini. Lakini sasa na ile Kamati inayoitwa Kamati ya Ulinzi na Usalama haiko Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunajenga Serikali ya Kijeshi ndiyo maana Wakuu wa Mikoa wengi mpaka wawe wanajeshi. Sasa sijui kama tunatarajia vita hapa na ni kwa nini wote wawe wanajeshi tu? Halafu baadaye Kamati ambayo inachukua maamuzi mazito ya kisheria na Kikatiba na wakati ile haiko Kikatiba ni kama sungusungu fulani hivi. Kwa hiyo, hilo nalo pia naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini naomba niwahakikishie kwamba hakuna CCM ya Zimbabwe na wala wana-CCM hatuna kiherehere, ila tunafanya kazi zetu kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa pole za rambirambi kwa wenzetu wote ambao wamepoteza ndugu zao kwa ajali mbalimbali ambazo zimetokea katika kipindi hiki cha Bunge. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mimi sina la kupinga kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo mengi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweza kuyazungumzia na yanagusia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na hatutasita kusema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza kwa kweli Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, sina tatizo nao na wananchi wa Jimbo langu wanafahamu hiyo. Lakini nachukua nafasi hii ya pekee kumpongeza Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celine Kombani, kwa kazi anayoifanya, ni nzuri sana. Kwa kweli tunamsifu, kwa muda mfupi ambao ameweza kujiunga na Bunge na kupata nafasi ya Unaibu Waziri ameweza kuhimili na kujibu maswali kwa uhakika na wala bila kubabaisha na Waheshimiwa Wabunge wote wanakiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe, kwa kweli kwa kazi ambayo umefanya kwa kipindi hiki tangu tumekuchagua na kwa lengo lako nzuri la kufanya

Waheshimiwa Wabunge waweze kuwa Wabunge wa Kimataifa na Bunge la kujitegemea. Inaonyesha wewe mwenyewe ni shahidi katika mjadala uliopita wa Bajeti na sasa Waheshimiwa Wabunge wanachangia kwa kujiamini na wala bila kujali itikadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, mimi nilikuwa na mambo ya kusema kama matatu. La kwanza ni kwa upande wa mikopo. Serikali imekuwa na lengo zuri tu kabisa la kuwawezesha wananchi na hata ikaamua kutoa hiyo shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Lakini lazima tukubali kwamba kuna tatizo kubwa sana katika utekelezaji wa hizo fedha shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wake umekuwa ni mgumu na haugusi moja kwa moja kama dhamira ya Mheshimiwa Rais alivyotaka kwa maana ya wale ambao wana kipato cha chini. Sana sana ni wale wenye anwani ambao tayari wana biashara ndiyo wameweza kunufaika na mpango huo mzima.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu tumewasikiliza wenzetu wa *NMB,* wenzetu wa *CRDB* na sisi Waheshimiwa Wabunge tunatoka kwenye hizo sehemu ambazo hao wajasiriamali wapo na wale watu wa kipato cha chini wapo. Tulifikiri kwanza Serikali ingeweza kutathmini fursa ambazo zipo kwa kila Wilaya na hatimaye kutoa agizo kwa hizo benki ambazo zinahusika ili ziweze kuwakopesha waweze kuzitumia fursa zao.

Mheshimiwa Spika, sasa inaonekana moja kwa moja kwa kweli *NMB* wanafanya biashara, tukubali na *CRDB* wanafanya biashara, si rahisi wakamkopesha mtu ambaye hawana uhakika kwamba atarejesha mkopo huo na hawamfahamu kwa ukaribu. Ndiyo maana wamekuwa wakisita sana kukopesha watu ambao shughuli zote zinagusa kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa na pendekezo moja kwamba kwa sababu tumesitisha na Awamu ya Pili inakuja taasisi pekee ambayo ingeweza kutusaidia ukiondoa *SACCOS* ni taasisi ya *SIDO.* Shirika la *SIDO* limeenea katika kila Mkoa na lina uwezo wa kutoa elimu kwa kila Wilaya mpaka kufika kwenye vijiji. Wanatoa elimu na wanatoa mikopo ya vifaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tungewapa nafasi kama Waziri mwenye dhamana ya shughuli ya Uwezeshaji Wajasiriamali angeshirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa maana ya *SIDO* ili waone kama fedha nusu wazipeleke kupitia *SIDO* na fedha nyingine ziendelee kuwa upande wa Benki. Kwa sababu *SIDO* wanatoa mikopo ya vifaa na tunaelewa ilipotangazwa hiyo mikopo kila mtu alikuwa na hamu ya kwenda kuchukua mkopo kabla hajajua ni jambo gani atafanya. Lakini *SIDO* watawasaidia kuibua miradi, watasaidia kuwakopesha vifaa ambavyo watavitumia katika miradi hiyo na hatimaye watawaelekeza ni jinsi gani ya kufanya miradi hiyo. Kwa hiyo, hili lilikuwa ni pendekezo langu ili iwaguse wale ambao kabisa Mheshimiwa Rais anahitaji kuwasaidia na hatimaye waweze kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwa upande wa kilimo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana na mimi limekuwa likinisumbua sana hili suala la kilimo. Mpaka nashangaa na najiuliza sana tangu nimeingia kwenye Bunge hili, Bajeti

ya Kilimo imekuwa ikiwa kubwa sana na imekuwa ikiongezeka ukilinganisha na sekta nyingine zote. Lakini *impact* kwa mkulima mmoja mmoja haionekani wala haiwagusi. Sasa najiuliza tatizo liko wapi? Mawaziri waliowekwa huko, *turnover* ya Mawaziri katika Wizara hii imekuwa ni kubwa, anaweka huyu, anaweka huyu na wote ni watendaji wazuri sana wa kazi.

Sasa mimi nafikiria huko ndani ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuna nini? Basi ifanyike *reform* ndani ya Wizara yenyewe ya Kilimo labda kuna matatizo ya watendaji wetu, hawataki kwenda na kasi ambayo Serikali ya Awamu ya Nne inataka iende na kasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa pembejeo kwamba Mikoa ambayo ni *the Big Four* wapate mbolea, ufuatiliaji wake umekuwa ni tatizo sasa hatuelewi ni nini? Nani asijue kwamba Mheshimiwa Stephen Wasira, anafanya kazi sana, Mheshimiwa Charles Keenja alikuwa ameweka kipaumbele sana kwenye kilimo cha umwagiliaji. Lakini ukienda huko kwenye taasisi na *scheme* hakuna kinachoendelea na kipato cha mwananchi hakijaongezeka kwenye kipato chake. Lakini tunaamini ajira kubwa ni kilimo, sasa huko Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuna tatizo gani? Kwa nini kusifanyike tathmini nzuri tu, kama wenzetu wamekaa sana ndani ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika basi wabadilishwe waje wengine wenye kasi mpya na ari mpya ili tuweze kusonga mbele na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo nilitaka kulisisitiza kwamba tumechoka. Mimi juzi hapa niliuliza swali hapa la *scheme* ya Madibira ambao umeigharimu Serikali shilingi bilioni 24 kwa mkopo, nikawa nauliza ule mradi unazidi kuzorota, je, bado unasimamiwa na Serikali au unasimamiwa na wanaushirika wanaolima pale? Jibu alilonipa Naibu Waziri na wenyewe walivyosikia wananchi huko inaonekana hawajafanya utafiti.

Mimi nikamsamehe Naibu Waziri kwa sababu ndiyo kwanza alikuwa ameingia kwenye hiyo Wizara, lakini jibu limeandikwa na wataalamu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wanaandika kumfurahisha Waziri. Sasa hayo kwa kweli yanakuwa yanatugusa sana lazima kitu kifanyike huko ndani ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika badala ya kuleta majibu ya hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni maeneo ya utawala. Mkoa wa Mbeya una eneo kubwa na umekaliwa na Wakuu wa Mikoa wengi sana na wengine wako humu ndani ni Mawaziri, lakini maeneo yake hayajawahi kufikiriwa kwa muda mrefu. Wilaya tatu, kama Mbozi, Chunya na Mbarali zina maeneo makubwa sana. Sasa ni lini na sisi Mbeya tutafikiriwa kugawanywa ili tupate Wilaya ambazo zinaweza kuwa rahisi kutawaliwa?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwa upande wa Wilaya yangu ya Mbarali ilianzishwa mwaka 1995 na ina Tarafa mbili tu, ina ukubwa wa kilomita za mraba 16,000, Tarafa mbili, Kata 11. Mkikaa ndani ya *full council* mna Madiwani 16, eneo mnaloliongoza ni kubwa mno, tumefuata taratibu zote za kupitia kwenye *council*, za kupitia kwenye *RCC,* na ninaamini *RAS* wetu wa Mkoa wa Mbeya ameweza kuwasilisha

mawazo yetu na mapendekezo yetu ya kugawa Tarafa na Kata kwa Wilaya ya Mbarali hata Jimbo. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atusaidia haraka iwezekanavyo ili kuweza kutusaidia kugawa ikiwezekana kuanzia Jimbo, Tarafa na Kata ili ziweze kutawaliwa kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwa upande wa kipato kwa Waheshimiwa Madiwani, mimi naipongeza na kuishukuru Serikali imewafikiria, lakini kipengele ambacho kimewekwa cha kusema kwamba watazingatia uwezo wa Halmashauri hilo kwa kweli linatugusa sisi wote. Ni afadhali ingesemwa kwamba Halmashauri zote ziongeze hiyo posho kutoka shilingi 30,000 mpaka 60,000 bila kuweka hicho kipengele. Hata tulipo sasa tunatofautiana sana Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikao cha Madiwani wengine wanapokaa kwenye vikao wanalipwa shilingi 10,000 kwa kikao na hiyo shilingi 30,000. Lakini utasikia Halmashauri nyingine wanalipwa 30,000 au 50,000 kutokana na uwezo wa Halmashauri. Sasa hiyo shilingi 30,000 yenyewe ilivyo inatugusa ni kidogo sana kwa Diwani kwa kazi ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika Mbarali anajua na Waziri wa TAMISEMI amefika huko, Kata moja ni sawa sawa na Jimbo moja labda la Zanzibar au la Jimbo moja la Mkoa mwingine. Huyo Diwani anatembea kwa miguu, wafugaji walikuwa wametapakaa huku na huku, kwa hiyo, Diwani alikuwa anazunguka kwa miguu au kwa kutumia baiskeli, akifika lazima avue sharti aoge ndiyo aende kwenye mkutano, lakini jibu lake anapata shilingi 30,000 kwa mwezi na kwenye kikao anapata shilingi 10,000. Sasa hilo lingeweza kuzingatiwa. Wafikiriwe vile vile na posho za vikao na hata zile fedha za kujikimu. Lakini pili, yaangaliwe na maeneo ya utawala, hao Madiwani wanatofautiana. Sasa kama Halmashauri haina uwezo maana yake Madiwani wake wataendelea kupata hiyo shilingi 10,000 na hiyo shilingi 60,000. Sasa hicho kigezo ningeomba Waziri mwenye dhamana akiangalie kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwa upande wa Mbarali naipongeza Serikali kuweza kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mbeya na Mbarali kwa upande wa eneo la Ihefya, ile sehemu oevu na ninawapongeza wafugaji wote waliokuwa wameingia pale Ihefya na wananchi wote kwa jumla waliweza kuitikia wito wa Serikali kwa mmoja mmoja. Walitoka ndani ya Ihefya na ile Ihefya sasa inapendeza; na ukienda kwa kweli imerudia hali yake ya awali. Nakumbuka wakati najiunga na Bunge hili mwaka 2000 swali langu la kwanza lilikuwa kuhusu Ihefya. Kabla hata wafugaji hawajaingia wengi. Niliomba Serikali inisaidie kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mbarali ili kuweza kuwatengea maeneo wafugaji ambao walikuwa wameingia Mbarali. Lakini ilisuasua mpaka juzi tulipoona athari sasa zimetokea.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nawapongeza Mawaziri wote waliokuja na Serikali kwa jumla kuweza kuwaondoa wafugaji ndani ya eneo lile. Lakini sasa kinachofuata ni kwamba hilo eneo sasa linapandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa na litachukua karibu kilomita za mraba 4,500, mpaka 5,000 kutoka 80,000. Kuna Kata moja ambayo itatakiwa iondoke na vijiji saba. Sasa Mkoa na Wilaya tulifanya ziara na

kuwahamasisha wananchi na wananchi wamekuwa hawana matatizo wameitikia kuhama. Tangu mwezi Septemba, 2006 mpaka sasa tathmini imekuwa ikifanywa na wameambiwa wasifanye shughuli zozote za maendeleo kwenye hivyo vijiji saba, maana yake shule hakuna kujengwa, nyumba za kudumu hazitajengwa itakuwa mwisho tarehe 30 Juni, mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa nilichokuwa nakiomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au Waziri mwenye dhamana kuwa kuna vijiji ambavyo viko tayari kuhama mapema iwezekanavyo. Wanachosubiri ni hiyo fidia ili waende huko wakaendelee na maendeleo yao. Kwa sababu shule zitapaswa kuhamishwa, miradi mbalimbali ambayo wanayo itabidi wahame nayo, mashamba inabidi yakaandaliwe. Nina mfano halisi kabla sijaja kwenye kikao hiki kuna kijiji kimoja Kata ya Madibira Ikonga waliniambia Mheshimiwa Mbunge tunahama lini? Maana yake wamesitisha kila kitu cha kuwaletea maendeleo wanasubiri waende huko na maeneo ya kuhamia wameishayaainisha. Sasa kwa sababu tumeshalichoka hilo na *mind set* za wananchi ziko tayari kuhama.

Nafikiri ni wakati muafaka kabisa kwamba haya mambo yangeenda haraka haraka badala ya kutulia. Halafu baadaye tusije tukaibua ikaja ikawa kero tena kwa wananchi. Kwa sababu tayari wameishaandaliwa na wako tayari kuhama. Ningeomba wakati Waziri Mkuu anahitimisha hoja yake nijue mpango wa Serikali uko vipi ili kuhakikisha kwamba hao wananchi hawatapata usumbufu tena hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na jambo moja ambalo ninataka kuipongeza Serikali kwa upande wa uwezeshaji wa wananchi. Mimi nimejifunza jambo moja zuri sana la stakabadhi za mazao ghalani. Nilitaka nilichangie na wenzangu kwamba ni kitu pekee ambacho kimewafanya wakulima wa Mbarali waweze kuondokana na umaskini kwa haraka. Kwa sababu imekuwa ni changamoto pekee kwanza ya kusaidia kupata mikopo, lakini pili, kupata bei nzuri ya mazao na tatu, Serikali inakuwa inajua Wilaya hiyo ina mazao kiasi gani kwa ajili ya kutafuta soko. Kwa sababu ni Wilaya chache tu ambazo wameanzisha utafiti kwamba huu mpango ni mzuri sana kwa Wilaya nyingine zote ambazo zina mazao ya nafaka au ya chakula. Kwa sababu inawasaidia wananchi hao kutafuta soko bei ikipanda.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa ninavyoongea kasi ni kubwa sana, tatizo tu ni ma-*godown*, maandalizi ya ma-*godown* yale hayatoshi, unakuta mazao yamewekwa mpaka nje na wanaweka maturubai, kitu ambacho ni hatari. Sasa huu mpango uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ningeomba wataalamu watusaidie kuhakikisha kwamba yale ma-*godown* mengine yaliyokuwepo ya zamani yakarabatiwe ili wananchi tena wasipate athari za kuharibikiwa na hayo mazao. Kwa hiyo, hilo nalisisitiza na nawashawishi wenzangu kwamba mpango huu ni mzuri kwa ajili ya kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni pongezi kwa upande wa MMEM kwamba inaendelea. Utaratibu uliokuwepo ulikuwa ni kupeleka fedha kwa kuangalia kasi ya kila Wilaya. Mpango ule wa Awamu ya Kwanza umeisha mwaka jana. Sasa tayari kulikuwa na magofu mengi yapo yalikuwa bado hayajaezekwa. Ningeomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atoe mkazo kwa Maafisa wa Elimu wa Wilaya kila mmoja alete

tathmini ya yale majengo ambayo hayakukamilika kwa wakati ule, kwa sababu watu walikuwa wanajenga kwa kasi wakitegemea fedha za MMEM zitakwisha na mpaka sasa majengo mengine yameishia nusu ili kwanza majengo yale ambayo yalikuwa hayajakamilika, yakamilike wakati muafaka. Ni vizuri wakaleta hiyo tukakamilisha ndipo tukaanza mpango mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu bado ni kubwa, wenzangu wamelichangia, nisingependa kulirudia, lakini tatizo kubwa sana ni kwa sababu shule ni nyingi na mazingira yale ya mbali usipokuwa na walimu maana yake wanafunzi hawatapatikana wengi wa kufaulu kwenda shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kwa upande wa mpango wa fedha hizi za UKIMWI, niseme shughuli nzima za UKIMWI. Mimi niko kwenye Kamati ya *PAC,* sasa wakati ule tumehudhuria kwenye semina pale walipokuwa wenzetu wa ule Mpango wa Mheshimiwa Rais, utakuta kila Wizara imepewa fedha za maendeleo nyingi sana *billions*, lakini ukiuliza unaambiwa ni fedha za UKIMWI. Hizo fedha za UKIMWI zikija zinachelewa kwa hiyo, unaona kwamba Wizara fulani imepewa fedha za maendeleo nyingi kumbe fedha nyingi ni za UKIMWI na UKIMWI mwenyewe ni kwa ajili ya kuleta elimu tu. Sasa hatujui ni kigezo gani kinatumika ili kuhakikisha kwamba Wizara zote na Taasisi zote zinapata fedha za UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuendelea kuwepo katika siku ya leo ili niweze kushiriki katika Bajeti hii. Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wote Mawaziri, Manaibu, Watendaji kwa ajili ya shughuli nzito walioifanya ya kutayarisha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wananchi wa Wilaya ya Bukombe kwa kuendelea kuniamini, lakini pia kwa jitihada kubwa walizozifanya hasa katika mabadiliko ya Idara ya Elimu kutoka shule za sekondari tano mwaka 2005 hadi shule za sekondari 21 kwa sasa hivi ninavyoongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha natoa pole kwa wale wote waliopatwa na misiba mbalimbali katika nchi yetu ya ajali na ya aina nyingine ya magonjwa. Lakini tunajua Mungu wetu ni mwaminifu na Mungu wetu ni mwema na tena Bwana alitoa na Bwana ametwaa na jina la Bwana libarikiwe. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niongelee suala la utawala bora. Najua hata Waheshimiwa Wabunge wengine wameliongelea suala hili hasa Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuongea sasa hivi. Lakini ninapoongea suala la utawala bora ninazingatia sana eneo la Wilaya ya Bukombe. Bukombe ina ukubwa wa

kilomita za mraba 10,482 ambazo ni sawa na asilimia 20.6 ya eneo lote la Mkoa wa Shinyanga yenye ukubwa wa kilomita za mraba 50,781. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sensa ya mwaka 2002 ukiangalia Kata moja ninayoishi mimi Kata ya Ushirombo ilikuwa na idadi ya watu 87,807 ikiwa na vijiji 18 na matawi 27 ya Chama cha Mapinduzi. Lakini Tarafa moja ya Siroka katika sensa hiyo mwaka 2002 ilikuwa na idadi ya watu 214,900 na kitu, vijiji zaidi ya 50. Kwa sasa hivi Wilaya ya Bukombe ina idadi ya watu 525,746 na hii inasababishwa na ongezeko la asilimia 7.4 kwa mwaka katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika hali halisi utawala bora kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe inawezekana ikawa ni mgumu sana, ugumu wake unatokana na ukubwa wa maeneo ambayo viongozi wetu wanayasimamia. Fikiria labda Mtendaji wa Kata kusafiri kwenda kufika kwenye kijiji kimoja inabidi pengine atumie siku nzima. Wale wananchi wa kule hawatapata haki zao za kimsingi za kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Madiwani tulikaa tukaazimia kwamba tusajili vijiji vipya, tuongeze Kata, tuongeze Tarafa, tuongeze na Majimbo kwa sababu maeneo ni makubwa mno. Kwa mfano, kipo kitongoji kimoja kinaitwa kitongoji cha Kherimchele kutoka Kata ya Uyovu kina Kaya 627 hicho ni kitongoji. Kitongoji ndani ya vitongoji vipo saba, siyo kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hali yoyote utawala bora na *D by D* na suala ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza katika ukurasa wa 40 wa kitabu chake cha hotuba linawezakana likawa gumu pamoja na nia nzuri ya Serikali iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka labda Serikali isaidie kunieleza kwa sababu sisi upande wetu ngazi ya Wilaya tumeshamaliza maazimio yetu ya kuomba usajili labda Serikali itawasaidia wananchi wa Bukombe wajue kuna hatua gani imefikiwa ili nao wafurahie matunda mazuri ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Serikali kwa sababu tayari imesajili vijiji 48, nilijaribu kupitia nikafikiri labda ndiyo ya kwangu, lakini wako wengi wenye matatizo kama hayo. Wilaya zimeongezwa kwa kweli ni jambo jema. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali itusaidie hasa kujua ufafanuzi wa Wilaya ya Bukombe hitaji tulilolisema limefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika, lakini ushauri wangu, naishauri Serikali iharakishe kutoa usajili wa vijiji hivyo, Kata, Tarafa na Majimbo inawezakana Kata na Jimbo ikawa ni vigumu kwa sababu itahitaji uchaguzi mwingine, lakini tunaweza tukasajili vijiji kwanza, tukasajili Tarafa na baadaye kadri uchaguzi utakavyokuwa unakaribia tukamilishe na maeneo mengine yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Kata hizo zina viongozi wa Kata na viongozi wa Tarafa katika maeneo hayo na Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Kata, Waratibu wa Elimu wa Kata, Maafisa wa Kilimo na Mifugo wa Kata kutokana na ukubwa wa

maeneo niliyoyasema wanapata shida sana katika utekelezaji wa Ilani wa Uchaguzi. Nilikuwa pia naishauri Serikali ikiwezekana hao viongozi wetu wakopeshwe vyombo vya usafiri ili waweze kuzunguka vizuri katika maeneo hayo na kurahisisha shughuli zao na kuwatendea haki wananchi walioko mbali na Makao Makuu ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa na ombi na ushauri kwa Serikali hasa nafikiri itakuwa ni ombi kwa Waratibu wa Elimu ya Kata, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji wana shughuli nyingi sana wanazozifanya katika uandishi, kwa sababu ni ombi au labda mimi nisaidiwe nimeshindwa kulielewa vizuri. Nashindwa kujua hao watu wanapata wapi ruzuku ya kuendeshea ofisi zao. Inawezekana hao watu hawana mafungu rasmi. Nilikuwa naangalia kwenye kitabu kikubwa tulichopewa cha utekelezaji wa ahadi za Serikali katika Bunge ninaona ni zile fedha zinazorudishwa kijijini au kwenye Kata kutokana na mapato ya Halmashauri. Lakini sijaona hao viongozi wa ngazi ya Kata na Vijijini kule wanapata wapi ruzuku ya kuendeshea ofisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana tusipowaangalia hao watu tunaweza tukachangia na kuhamasisha kuendelea ulaji wa rushwa katika maeneo yao. Naomba uangaliwe utaratibu wa ruzuku kama pengine ni Halmashauri zinaagizwa au kama ni Serikali Kuu basi utaratibu ule ueleweke ili na sisi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani tufahamu kwamba Ofisi za Mtendaji wa Kata, Ofisi ya Mratibu wa Kata, Mtendaji wa Kijiji wanapatiwa fungu kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, ninaongelea suala la utawala bora katika Idara ya Polisi au Idara ya Ulinzi na Usalama hasa niseme katika Idara ya Polisi na Sungusungu. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika ukurasa wa 137 kwenye Ulinzi na Usalama inasema hivi nanukuu: "Kuwahamasisha wananchi ili waendelee kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao na kuhakikisha usalama wao na wa mali zao." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, sungusungu wanasaidia sana ulinzi katika maeneo yetu hususan katika Kanda ya Ziwa na hao sungusungu ndiyo wanasaidia sana katika juhudi za kuwasaidia polisi kwa sababu tunaamini polisi ni wachache. Kwa mfano, nilipata taarifa kwamba katika Wilaya pekee ya Bukombe ina upungufu wa askari wengi sana. Lakini sungusungu wametapakaa katika kila kijiji. Hao sungusungu wanasaidia ulinzi, shida inapotokea inawezekana kwa sababu mila na desturi zinazotumiwa na askari wetu wa Jeshi la Sungusungu ni kwamba wanakuwa na siku zao maalumu pengine za kutawazwa, sijui itakuwa ni lugha sahihi, lakini wanasema ni lugha ya kutawazwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku hiyo wanapotawazwa wanaona kabisa fulani ni mhalifu katika eneo letu anatusumbua. Wanamtoza faini ya kutoa labda mbuzi mmoja ambaye atwaliwa na wanajamii pale. Mtu huyo anatoka anakimbia kwenda polisi akifika polisi anakwenda kusema maneno nimepigwa, nimefanya nini na anasingizia anaunda maneno yatakayoweza kulidhalilisha jeshi la sungusungu. Jeshi la polisi kwa sababu wameambiwa kwamba nimepigwa na sheria ya nchi hairuhusu kufanya hivyo hawa sungusungu wanakwenda kukamatwa wanawekwa ndani, wanapelekwa Mahakamani,

sasa matokeo yake tutadhoofisha sungusungu. Labda nipende kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa Brigedia Jenerali Mstaafu Dr. Balele, amesimamia kweli sungusungu katika maeneo yetu. Lakini tunaomba basi Serikali iwape ulinzi wa kisheria ili watambulike kisheria, wanapofikishwa Mahakamani wanasema hawaelewi lolote. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, upande wa polisi, katika Wilaya ya Bukombe kipo kituo cha Masumbwe, wale polisi ukifika pale utawahurumia na nilikuwa naomba Waziri wa Usalama wa Raia akipata nafasi aje kule na Mkuu wa Mkoa amfikishe Masumbwe. Kile kituo kinavuja na mvua ikinyesha inabidi watoke nje. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kituo wakiangalie lakini pamoja na kutupatia gari la polisi kwa ajili ya upelelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la miundombinu. Katika kitabu cha Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ukurasa wa 47 kifungu kidogo cha 67 alieleza kwamba wanaangalia ukarabati wa barabara katika mikoa sita ili waweze kuchochea ukuaji wa maendeleo katika maeneo hayo. Nashangaa na naomba Serikali iniambie ni kigezo gani imetumia kuuacha Mkoa wa Shinyanga katika mikoa sita inayotakiwa kuchochea maendeleo kwa vile Mkoa wa Shinyanga uko nyuma, barabara zake ni mbovu lakini haiko katika mpango huo, ninaomba Serikali iangalie. Kama walivyomaliza kusema wazungumzaji wengine madini yapo kule, wawekezaji wanapitisha mali zao katika barabara mbovu na Serikali haijaangalia. Wilaya ya Bukombe peke yake barabara haziridhishi, naomba hili tuliangalie na hatimaye tuweze kupewa maelezo kwamba wametumia vigezo gani kuiacha Wilaya na Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la nishati na madini, lakini najua nitaomba nafasi nichangie hasa kwenye Wizara husika. Tuna tatizo la umeme katika Wilaya ya Bukombe na siasa ya Bukombe sasa hivi ni umeme. Balbu moja tunalipa shilingi 8,500 kutoka kwa wafanyabiashara wenye *generator* ili tuweze kuendesha uchumi wetu, hatuwezi tukafanikiwa pasipo umeme. *(Makofi)*

Naomba umeme Bukombe tuwashiwe umeme lakini nitaomba nichangie kwenye Wizara husika kwa sababu muda hapa haunitoshi. Upande wa madini niliongea hata mwaka jana suala la watafiti wanaokaa kwa muda mrefu na suala hili bado nitaendelea kulisema. Wako watafiti katika eneo la Nyakafuru wamekaa zaidi ya miaka kumi na nitaendelea kulisema labda mpaka Serikali itakapotoa jibu la kuridhisha, walisema mkataba wao unaisha, lakini sasa hawa watu sijaona faida wanayokuwa nayo katika eneo lile.

Katika mgodi wa Tulawaka sehemu kubwa ya wafanyakazi wake wote wanapata huduma katika kituo cha afya cha Uyovu, lakini sijaona mchango wowote unaotolewa na mgodi huu kwenye kituo kile. Sasa tunajaribu kuangalia na ule mgodi huko Biharamulo kituo cha Uyovu kiko Bukombe kutoka kwenye mgodi kuja pale Uyovu ni chini ya kilomita 20 lakini je, wanawasaidiaje? Naiomba Serikali ituangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kufukuzana na muda kama utaniruhusu nitaongelea suala la kilimo. Sekta ya kilimo ni muhimu sana katika nchi yetu. Umuhimu wake ni kwa sababu ya mchango wake katika Pato la Taifa lakini sababu ya pili ni utoaji wa ajira, ni sehemu pekee inayotoa ajira. Lakini nchi yetu haijaweza kuzalisha chakula cha kutosha kwa ajili ya matumizi yake katika nchi yetu. Hili tatizo linatokana na hawa wananchi wakulima kwa sababu ni wadogo wadogo hawawezeshwi kupata mikopo, hawakopesheki.

Nilikuwa nashauri Serikali iweze kuwakopesha wakulima hawa kupitia Halmashauri zetu kwa sababu kwenye Mabenki hawakopesheki. Kama Serikali inaweza ikaunda utaratibu pesa ikapitia kwenye Halmashauri, Halmashauri iweze kuwawezesha watu kadhaa itakuwa ni nzuri sana. Lakini namshukuru Mheshimiwa Mbunge aliyekaa kwa utaratibu aliousema stakabadhi au nini ya mapato nimefurahia ingawa sijaujua vizuri inawezekana nitatamani nijifunze tuweze ku-*implement* katika Wilaya ya Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pamba. Pamba ni asilimia 60 inatoka katika Mkoa wa Shinyanga, lakini pia inatoka katika Kanda ya Ziwa. Lakini wananchi na wakulima wa Kanda ile wanapata shida. Mbunge mmoja siku moja alisema hapa wao wanafanana na mshumaa. Tunaomba kuna matatizo na huko kwenye Wizara labda ndiyo maana hata Bunge wanasema kuna nini, kuna tatizo la pembejeo. Dawa hazifiki kwa wakati, zikifika dawa hata wakinyunyuzia wale wadudu utafikiri wamepakwa mafuta.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ili suala la pembejeo hasa dawa libinafsishwe, wapewe wafanyabiashara binafsi wanunue walete dawa kule, mwananchi aende akanunue kule. Kwa sababu hata ule utaratibu wa *passbook* hauwasaidii. Inawezekana wako tu kundi la watu wachache wanaonufaika na *passbook*. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iwaangalie hawa ili tuweze kuboresha uchumi wetu na tuweze kuwaondoa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami pia niweze kutoa mchango wangu katika hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliopita kwanza kwa kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo naomba kusema mimi binafsi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Musoma naiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda uliopo ni mfupi naomba niende kwenye hoja moja kwa moja. Kati ya hoja ambazo ningependa kuzizungumza zingine zinahitaji tu maelekezo kwa sababu wakati fulani zinaendelea kuleta kero kwa wananchi wetu ambao hasa ndio wametuchagua. Mojawapo ya kero ambayo inahitaji tu kuzungumziwa mara moja na ikaondoka ni pale ambapo Serikali kwa maana watendaji wetu wakati mwingine wanasababisha vitendo ambavyo vinakera wananchi pasipo sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano leo unakuta hawa watu wa daladala hizi za kawaida zinazopiga *town trip* wanashikwa kwa sababu ya kwamba magari yao hayana vidhibiti mwendo. Sasa wanashikwa na wakati huo huo wanatozwa faini. Sasa ukiangalia vidhibiti mwendo vyenyewe havipo, lakini hayo magari yanazunguka hapo hapo mjini na wanaambiwa kwamba magari hayana vidhibiti mwendo, wakishashikwa baada ya hapo wakishatozwa faini wanaachiwa. Kwa hiyo, nadhani hilo ni suala ambalo Serikali linahitaji tu litolewe tamko tofauti na hapo ili vidhibiti mwendo viweze kuletwa ili tatizo liweze kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nilidhani ni vizuri nikalizungumza ni suala ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alishalizungumza katika kikao kilichopita, lilikuwa linahusu mambo ya mirathi pamoja na mafao ya wastaafu na hao wanaoshughulikia mambo ya mirathi. Bahati nzuri alishalitolea tamko kwamba ni vizuri wananchi wale wote wenye matatizo ya mirathi pamoja na mafao waende kwenye Ofisi za Wabunge wakajiandikishe. Naomba kusema hivi zoezi hilo tumelifanya na tumeshalimaliza, tunasubiri tu maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nini kifanyike kwa hawa wananchi ili waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo bahati nzuri leo limejibiwa hapa ni suala linalohusu mahabusu kuchukua muda mrefu Mahakamani. Tunashukuru kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia amesema wazi kwamba kwa kweli suala la vifaa, uwezo na Mahakimu linachangia mahabusu kuchukua muda mrefu. Lakini basi kwa kweli ni vizuri Serikali ingeliangalia kwa mapana na marefu zaidi maana mimi nilipokuwa jimboni nilibahatika kutembelea Gereza la Musoma Mjini. Lakini cha ajabu ambacho nimekutana nacho kule kwa kweli mahabusu wanachukua zaidi ya miaka 9 Gerezani.

Ukiangalia basi huyu mahabusu ambaye anachukua zaidi ya miaka 9 ni kwamba bado yuko katika tuhuma na kama yuko katika tuhuma kweli pale na matatizo yaliyopo ya uwezo wa kifedha, pamoja na matatizo yaliyopo ya ufuatiliaji kuwa na taabu lakini kwa kweli kipindi cha miaka 9 ni kipindi kirefu mno na ni vizuri Serikali ingelipa kipaumbele ione kwamba haya matatizo itayapunguzaje ili ule muda wa kusubiri Mahabusu wanakaa miaka 9 kwa kweli ni muda mrefu sana walau kipindi hicho kipunguzwe vizuri zaidi ili haki zao ziweze kupatikana maana yawezekana kuna wengine hawana makosa lakini wako mle wanakaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuwa nimezungumza hilo kwa ajili ya muda naomba nizungumze masuala mawili ya mwisho kama ifuatavyo, suala la kwanza linahusiana na Halmashauri zetu. Ni kweli kama tunavyofahamu Halmashauri kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii nayo ni Serikali kama zilivyo Serikali zingine. Ni kweli kwamba kuna matatizo makubwa ambayo yako ndani ya Halmashauri zetu na leo tunaipongeza TAMISEMI kwa juhudi kubwa ambayo imeendelea kufanya katika kupunguza matatizo makubwa yaliyoko katika Halmashauri. Mojawapo ya matatizo hayo ni pamoja na watumishi. Tunawapongeza TAMISEMI kwamba imejitahidi sana kusukuma au kupeleka watumishi wengi katika Halmashauri zetu. Lakini bado utendaji

wa kule wote tunakubaliana kwamba haujawa mzuri. Sasa mimi nilidhani yako baadhi ya mambo mawili wakati baadhi ya mambo ambayo Serikali inahitaji kuyatilia mkazo. *(Makofi)*

La kwanza ushauri wangu katika Idara zote na katika maeneo yote kuna labda ni kama Wizarani kuna Waziri au Naibu. Kama ni Katibu kuna Katibu Mkuu na kuna Naibu Katibu Mkuu, kama ni Halmashauri kuna Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, lakini sasa kulingana na wingi wa shughuli za Halmashauri unakuta Mkurugenzi ni mmoja na hakuna Kaimu Mkurugenzi au Naibu Mkurugenzi. Sasa matokeo yake kulingana na shughuli za Halmashauri zilivyo nyingi kila siku Mkurugenzi yuko safari na kila siku Mkurugenzi yuko kwenye vikao na anapoondoka ni hiari yake amkabidhi nani nafasi yake ya ukaimu. *(Makofi)*

Katika hali hiyo sasa leo anamkabidhi huyu, kesho anamkabidhi huyu matokeo yake sasa mwendelezo wa ile mipango yote ambayo imepangwa katika kuendeleza inatofautiana siku hadi siku. Ningeishauri Serikali kwamba hebu sasa ni wakati muafaka kila Halmashauri iwe na Mkurugenzi lakini vile vile iwe na Naibu Mkurugenzi. Tunadhani kwa kufanya hivyo mambo mengi yanaweza yakaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa ni kweli kwamba ili Halmashauri iweze kuendelea na hili limetamkwa wazi jukumu kubwa la Serikali Kuu ni kuijengea Serikali ya Mtaa uwezo wa kuweza kujiendesha yenyewe. Katika kujijengea uwezo mimi ninavyofahamu tunaijengea uwezo kwa namna mbili, namna ya kwanza ya kuijengea uwezo ni katika rasilimali watu na ndiyo maana kama nilivyosema katika hoja yangu ya msingi kwamba kwa kweli katika hilo tunaipongeza TAMISEMI, imeendelea kufanya kila iwezalo kuhakikisha watendaji wengi au watumishi wengi wanapatikana katika ngazi za Halmashauri. Lakini basi kigezo cha pili, ni rasilimali fedha. Sasa pamoja na kazi kubwa na nzuri ambayo imefanyika huko lakini kwa kweli Halmashauri zetu hazina rasilimali fedha. Kwa kuwa hazina rasilimali fedha utendaji wake siku zote unakuwa ni wa kusuasua, ushauri wangu kwamba ni wakati muafaka badala ya Serikali kuwa kila siku inaongezea Manispaa fedha, ni vizuri Serikali ingejikita zaidi kwenye kuijengea Halmashauri uwezo ili ziweze kujiendesha zenyewe. Itakapojijengea uwezo ziweze kujiendesha zenyewe maana yake zitaweza kumaliza hayo matatizo mengi ambayo yanayotokana na Halmashauri hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo, bahati nzuri katika maeneo ambayo nimeyatembelea baadhi ya nchi mwaka juzi nilibahatika kwenda Afrika ya Kusini. Afrika ya Kusini nchi ile Halmashauri zake zinajiendesha kwa asilimia 98, kwa maana asilimia 98 zenyewe zinalipa watumishi wake mishahara, zenyewe zinatengeneza miradi yake ya maendeleo.

Lakini katika nchi yetu leo ukiiachia Halmashauri sidhani hata kwa asilimia 20 inaweza ikajiendesha na ndiyo maana haya matatizo mengi yanajitokeza. Kwa hiyo basi, ningeishauri Serikali ni vizuri ingekuwa hata na chombo kidogo ambacho kingejaribu kuangalia kuna matatizo gani kule katika Halmashauri zetu na iweze kuwa kama *area programme* za kusimamia kule katika baadhi ya Halmashauri zetu ziweze kuhakikisha

kwamba vyanzo vilivyopo Halmashauri zile zinakusanya mapato. Lakini tatizo lingine kubwa kule kwenye Halmashauri mapato yanayokusanywa kule ni ya majadiliano. Lakini kwenye Serikali Kuu ni wajibu wa walipa kodi waweze kulipa mapato. Kwa hiyo, kama hilo lingeangaliwa basi tatizo hilo lingeweza kukamilika. Lakini tatizo lingine kubwa ni tatizo linalohusiana na maslahi ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukiniangalia mimi kama Mheshimiwa Mbunge kazi yangu kubwa ni uwakilishi wa mwananchi, Diwani ni mwakilishi wa wananchi katika eneo lake. Mimi ni msimamizi wa kuisimamia Serikali na Diwani anaisimamia Halmashauri yake kule. Mimi kama Mbunge nina jukumu la kupitisha Bajeti hali kadhalika kwa Mheshimiwa Diwani. Mimi ni mhamasishaji mkubwa wa maendeleo kama Mbunge, Diwani ana jukumu hilo hilo na ndiyo maana Mbunge tunamwita ni Diwani. Hivi kweli ule uwiano wa shilingi 30,000/= kwa kazi kubwa anayoifanya Diwani kwa kweli ni vizuri Serikali ikaliangalia upya. *(Makofi)*

Leo tunashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ametamka wazi kwamba sasa Madiwani watalipwa kati ya shilingi 30,000/= mpaka 60,000/= ni vizuri angetamka kabisa kwamba Diwani walau kwa kuanza alipwe shilingi 60,000/= kuliko tutakapowaachia kwamba kulingana na uwezo wa Manispaa au uwezo wa Halmashauri. Kwa hiyo, hilo ni vizuri lingeangaliwa, lakini marupurupu yake mengine ambayo ni pamoja na haki zake za msingi Diwani kama mhamasishaji mkubwa tungeomba sasa ni wakati muafaka Serikali iweze kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la *bodaboda.* Suala la *bodaboda* bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema wakati anaahirisha Bunge kwamba tutakapokutana katika Bunge hili sheria italetwa na ifanyiwe marekebisho, lakini katika hotuba yake hakuna mahali ambapo nimelisikia. Suala la waendesha baiskeli au waendesha pikipiki kwa kweli yawezekana sisi kama Watanzania hatujalitazama katika uzito wake. Leo kuna maeneo mengi ambayo tumejenga shule zetu za sekondari pamoja na shule zetu za msingi pamoja na maeneo mengine, lakini wote tunakubali kwamba kote huko usafiri wa magari haufiki. Kama hivyo ndivyo basi kwamba hakuna usafiri unaofika kule kwa sasa kuna usafiri mbadala wa baiskeli pamoja na pikipiki za *bodaboda. (Makofi)*

Leo katika tatizo kubwa tulilonalo katika nchi yetu ni tatizo la matumizi ya muda. Sasa yale maeneo ambapo magari hayaendi ambapo ni kama kilomita 5 leo tunawakataza waendesha baiskeli na pikipiki hivi tunatarajia kuleta maendeleo endelevu. Kwa hiyo, tunadhani ni wakati muafaka sasa kama Waziri Mkuu alivyoahidi sasa ni vizuri sheria hiyo ikaletwa Bungeni ili tuweze kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda kwenye nchi za wenzetu ambao zimeendelea. Leo nenda India wanatumia mpaka usafiri wa punda, leo nenda hata kule Uingereza kutoka kule vijijini kwao kuja mjini wanaendesha baiskeli akifika pale anaweka baiskeli anaingia kwenye *tube* kwa maana ya treni akifika mjini anaendelea na kazi zake, hata ukienda kule Sweden. Hivi leo kwenye nchi changa kama Tanzania ambayo bado

inahangaika sasa kunakuwa na kigugumizi gani kwamba hata usafiri wa baiskeli unaonekana kwamba si usafiri unaopaswa kutumika katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunadhani sasa ni wakati muafaka kabisa suala hili liweze kushughulikiwa na baada ya kuwa limepata ufumbuzi sasa baiskeli pamoja na pikipiki ziweze kuruhusiwa. Kinachotakiwa pale ni kazi kidogo tu, wale waendesha baiskeli na pikipiki zitambulike na wao wasajiliwe wapewe mafunzo, wawe na vitambulisho basi tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo watakuwa wametusaidia zaidi na vile vile wao watakuwa wamejipa ajira kuliko hivi sasa badala ya trafiki kuangalia ajali za magari zinazotokea barabarani kila wakijisikia leo wanazoa baiskeli wanazipeleka huko, kesho wanazitoza faini ambayo badala ya kuleta tija inaendelea kuleta kero.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisingependa kugongewa kengele nasema naunga hoja mkono asilimia mia moja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza natumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Babati Mjini na napenda nitambue mchango wao hasa baada ya kuwasiliana nao na wale walionipigia simu pamoja na wale ambao nilipata nafasi ya kuzungumza nao. Nataka niwahakikishie kwamba hoja zao zote zitafika na kwa sababu leo nimepata nafasi kuchangia hoja ya Waziri Mkuu nitaanzia hapa. *(Makofi)*

Lakini hoja zingine ambazo hawatazisikia basi zitakuwepo katika hotuba za Mawaziri wengine na kama hazitakuwepo kwenye hotuba za Mawaziri tutahoji kwenye vifungu na kama kwenye vifungu hatutaona vile vile tutapata nafasi ya kuongea na Waheshimiwa Mawaziri nje ya ukumbi huu. Kwa hiyo, niseme nafasi ipo ya kuwawakilisha hoja ya wananchi wangu wa Babati Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia katika maeneo manne. Moja ni usimamizi wa kazi za Serikali, pili, nitazungumzia utekelezaji wa kazi za Serikali vile vile nitagusia matumizi ya kazi za Serikali na ahadi za Serikali. Ubadhirifu mwingi wa fedha za Serikali unatokana na eneo la ununuzi wa vifaa, ununuzi wa huduma na kazi za ujenzi au ukandarasi.

Sasa wote tunafahamu kwamba asilimia 70 ya matumizi ya fedha za Serikali ni ununuzi wa bidhaa hizo nilizozisema, vifaa, huduma na ujenzi kwa matumizi ya kawaida. Kwa matumizi ya ujenzi asilimia mia moja yote yanahusika kabisa na ununuzi wa vifaa, huduma pamoja na ujenzi. Eneo hili lisipopata usimamizi wa kutosha ndani ya Serikali basi tutajenga barabara ambazo ni hafifu, tutajenga majengo ambayo ni hafifu na kila kitu kitakuwa kwa kweli hafifu; eneo hili linahitaji usimamizi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hatoshi kuainisha mambo yote haya kwa sababu kazi yake kubwa kwa kweli ni kuona kama taratibu zimefuatwa. Lakini tunacho chombo cha kudhibiti ununuzi wa umma kwenye vifaa (*Public Procurement Regulatory Authority).* Mamlaka hii ya udhibiti ni muhimu sana, tukiimarisha Mamlaka hii ikaja mpaka kwenye mikoa mpaka kwenye Wilaya udhaifu utajitokeza. Ni kwa kupitia Mamlaka hizi tu ndio maovu yanaweza yakafichuliwa tofauti kabisa na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kwa hiyo *PPRA* naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aimarishe utendaji wake wa kazi na iweze kuja mpaka Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa twende Manyara na naomba nitumie kwa ruhusa yako niende kwenye *Vote 95* ambao ni Mkoa wa Manyara. Kwa ruhusa yako naomba niseme kwamba Mkoa wa Manyara unajenga jengo la Ofisi ya Mkoa, jengo hili sasa limetumia muda mrefu na gharama ni kubwa. Kutokamilika kwa jengo hili kunazuia maendeleo mengine kufanyika ndani ya Mkoa wa Manyara. Kwa sababu jengo linahitaji fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri wa Mkoa ilipendekezwa kwamba hili jengo liishe basi Mkoa unahitaji shilingi bilioni 2.485 na sina hakika kama fedha hizi zitatolewa lakini nataka niipongeze Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ameainisha kwenye ukurasa wake wa 16 kwamba Mkoa wa Manyara umepewa shilingi 885 milioni kwa Bajeti ya mwaka huu. Lakini amesema kuna shilingi 1.6 bilioni zimehamishwa kwenye mradi huo na kufanya fedha zote kuwa shilingi 2.485 bilioni. Nataka taarifa hizi zithibitishwe sasa vizuri ili Mkuu wa Mkoa wa Manyara anapoondoka hapa ajue fedha hizi kweli anazo. Kwa sababu kwenye kitabu hiki cha 4, kinaonyesha tu kwamba Mkoa umepewa hizo shilingi 885 milioni. Sasa hizi ambazo zimehamishiwa huko ningependa kujua sasa zipo wapi ili tuwe na uhakika kabisa kwamba zipo kwenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Mheshimiwa Rais alipokuja Babati kushukuru wananchi aliombwa fedha karibu bilioni moja ili jengo lile liweze kusogea na kukamilika. Sasa kama na fedha hizo zimetolewa kabla ya Bajeti hii mpya basi pengine ndiyo tunaweza tukafikia fedha hizo, vinginevyo sioni fedha hizi ziko wapi? Nashukuru Kamati imesema lakini kwenye vitabu sioni, kwa hiyo, ningependa kujua kwamba fedha hizo kweli zipo ili tuwe na uhakika, Mkuu wa Mkoa anakwenda kumaliza ile ofisi ili watumishi wahamie kule na hili tuweze kugeuka katika miradi mingine. Ningependa kupata ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa nichukue nafasi hii hapo hapo kwenye *Vote 95.* Sasa hapa nasikitika kwa sababu hotuba ya Waziri wa Fedha imesisitiza ukarabati wa hospitali za Mkoa. Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 35 amezungumza ukarabati Hospitali za Mikoa 11.

Lakini nasikitika kwamba hajasema tunakarabati lakini na kujenga hospitali moja Manyara, huo ndio Mkoa ambao hauna Hospitali ya Mkoa na ndilo jambo zito kabisa

kwa Mkoa. Ungewauliza leo wananchi wa Babati pale kwamba je, fedha hizi ambazo bilioni 2.485 ziende kumalizia jengo lile au zianze Hospitali ya Mkoa wangesema jengo lisimame na Hospitali ya Mkoa ianze kwa sababu ndio jambo la msingi. Lakini kwa sababu ni mradi ambao umeanza basi tunaomba fedha hizi zitolewe huu mradi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusitikitisha kwamba katika Bajeti ya mwaka jana zilitolewa fedha shilingi 100 milioni kuanza ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Manyara pale Babati. Leo hakuna fedha iliyowekwa ni sifuri, nataka maelezo ya kutosha kwenye eneo hili. Hakuna fedha maana yake ujenzi wa Hospitali ya Mkoa usiendelee, sasa maana yake ni nini? Imesisitizwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu naye mwenyewe ametaja lakini hakuna Hospitali ya Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna fedha maana yake ujenzi wa Hospitali ya Mkoa usiendelee, sasa maana yake nini nini? Imesisitiziwa kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye mwenyewe ametaja, lakini hakuna Hospitali ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, hospitali za mikoa mingine kwenye ukarabati zimepewa shilingi milioni 600, zingine milioni 500. Lakini hii ambayo ni muhimu ujenzi wake haijapewa hata senti tano. Nataka maelezo ya kina wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anafanya majumuisho ya Makadirio ya Ofisi yake. Nataka niunganishe hapo hapo na Hospitali ya Wilaya ya Babati ambayo ilikuwa Kituo cha Afya wakati Wilaya ilipoanza na kabla ya hapo ilikuwa Zahanati tu, hospitali ile sasa imezidiwa. Kabla hata haikumaliziwa ili iwe na hadhi ya Hospitali ya Wilaya tukapata Makao Makuu ya Mkoa, kwa hiyo, sasa hivi inabeba Mkoa, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alitembelea Hospitali hii na nina hakika aliyoyaona atakuwa ameieleza Serikali. Hospitali hii haina hata mahala pa kuhakikisha walau wale wagonjwa mahututi wanapokelewa na kuwekwa, hakuna *ICU*. Kama ni chumba basi wote hapo hapo, iwe akina mama, na kadhalika, ni hapo hapo. Hili ni tatizo kubwa, hakuna *ICU*!

Hospitali ina chumba cha kuhifadhi maiti tangu ilipokuwa Kituo cha Afya, chumba hicho ni kidogo kabisa, hakuna hata jokofu wala kitu chochote. Lakini hapa hata kwenye ukarabati haijawekwa, lakini vituo vya afya vingine na Hospitali nyingine za Wilaya zimewekwa, sasa tutaelwa nini. Wodi zina msongamano mkubwa kwa sababu ya Babati kupata Makao Makuu ya Mkoa, kwa kweli watu wamekuwa wengi sana. Sasa nashauri kwamba basi walau Serikali itafute fedha za kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Mkoa lakini vilevile katika fedha hizo za ukarabati hizi ambazo zinatolewa kwa baadhi ya Hospitali za Mikoa na Wilaya katika maeneo mengine basi fedha walau shilingi milioni 500, 600 zipelekwe pale kwenye hospitali ya Wilaya ya Babati tukarabati eneo la walau tupate jengo la *ICU*, chumba cha kuhifadhia maiti tupate majokofu hata mawili matatu.

Mheshimiwa Spika, zamani tulipokuwa Wilaya ni kwamba marehemu waliweza kuchukuliwa mapema zaidi na kwenda kuhifadhiwa. Lakini leo tuna Mkoa watu wamekuja pale. Tatizo likipatikana pale ni lazima maiti ihifadhiwe ili iweze

kusafirishwa. Kwa hiyo, ningeomba Serikali itusaidie basi kupeleka fedha pale ili tuweze kukarabati hospitali ile walau katika kipindi hiki ibebe huo mzigo wa Mkoa mpaka hiyo ya Mkoa itakapojengwa; na kama nilivyosema ningeomba sasa kujua mipango hii ya kujenga Hospitali ya Mkoa tungependa kufahamu kwamba sasa ikoje kati ya sasa na 2010. Serikali inaweza kufanya nini, vinginevyo wananchi hawatatuelewa kwamba wataona tunajenga mahekalu ya ofisi lakini tunasahau mambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno ya kutosha kwenye eneo hilo, nimalizie kwenye eneo hilo hilo kwamba Halmashauri ya Mji wa Babati ilipewa shilingi milioni 120 kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji ambayo hakuna. Lakini mwaka huu nayo imepewa sifuri, ningependa vilevile kupata maelezo. Lakini hapa nataka tujue kama ni Halmashauri ya Mji imetumia vibaya fedha hizo tuambiwe.

Nimeona kwenye *Vote* 82 ya Mkoa, nadhani wa Ruvuma nao walipewa shilingi milioni 120 lakini sasa wamepewa milioni 300. Lakini Babati mwaka jana ilipewa shilingi milioni 120, lakini sasa imepewa sifuri, nataka kujua katika maeneo haya je, kuna tofauti ya matumizi? Kama ni Halmashauri ya mji wa Babati imefanya ubadhirifu basi tuambiwe lakini wananchi wasipate shida bure wakati ambapo kama kuna mtu aliyekosea basi hao ndiyo waandamwe, lakini wananchi wasipate shida. Tunahitaji kuwa na Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Babati. Hapo vilevile tungenda tupate maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, naona muda umekimbia kweli kweli labda sasa niongelee kuhusu Kilimo. Gharama ya Kilimo imekuwa kubwa, mimi nimepiga hesabu heka moja kwa zao la mahindi ni zaidi ya shilingi 15,000. Lakini ukiuza kwa bei ya kawaida ya shilingi 17,000 ambayo *SGR* mwaka jana ilitupa, kwa kweli unapata shilingi 170,000. Kwa hiyo, mwananchi anaondoka na faida ya shilingi 20,000, hivyo Kilimo hiki hakilipi. Tunaomba bei ya mazao ya wakulima iongezwe, na *SGR* iweze kuwa na uwezo mkubwa wa kununua mazao ya wananchi ili tuhifadhi. Nchi jirani ya Zambia hapa *SGR* yake inahifadhi mpaka tani milioni mbili. Lakini ya kwetu hapa ni tani 150, inaonekana tatizo ni sheria. Basi i badilisheni hii sheria ili nchi iwe na hifadhi ya kutosha, tununue chakula cha kutosha sio tunaishia tani 150, haitusaidii na ndiyo maana tukipata tatizo basi tunashindwa namna ya kusaidia wananchi. Kwa hiyo, kama ni sheria tunaomba ibadilishwe.

Mheshimiwa Spika, eneo la barabara, barabara ya Minjingu- Babati Singida pamoja na Dodoma-Kondoa-Babati na kwa upande huu kwenda mpaka Iringa, miaka yote tangu miaka ya 1980 lugha ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mpaka 2004. *(Makofi)*

Mwaka 2004, tuliambiwa mikataba inaweza ikasainiwa Julai, 2005 kwa barabara ya Minjing -Babati-Singida, hakuna kilichotokea. Sasa nataka kujua lugha ya sasa ni nini? Basi nadhani tutasikia kama si kutoka kwa Waziri Mkuu mwenyewe basi kwa Waziri mhusika. Lugha ni nini? tunataka kujua. Muda umekwisha ahadi ndiyo hiyo mpaka 2010, ni kesho kutwa, imebakia bajeti hizi tatu mnazosema, sasa sijui pamoja na kuanza na nini sijui kama itaanza!

Tungependa kujua lugha ya uhakika ni nini, tupate safari hii. Barabara hizi zimeshindikana hata mngepeleka fedha za matengenezo na namna gani haziwezekani.

Babati-Minjingu ina magari mengi, nadhani sasa yanafikia zaidi ya 400 kwa siku, haiwezekani barabara ile kuendelea kuwa ya changarawe. Magari ni mengi ya mizigo, kwa hiyo, haiwezekani kabisa, sasa tujue lugha ni ipi ili tuendelee kufahamu kama tunaendelea na usanifu na upembuzi yakinifu wa kina. Kwa kweli nadhani lugha hii sasa ibadilike tupate ratiba kamili safari hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Babati, aliongea na wananchi kuhusu matatizo yao, yapo matatizo ya wananchi wa Haraa ambao kahawa yao iliathirika na dawa ambayo waliinunua kutoka kwenye Kampuni mmoja ya *Burton*, aliwasikiliza yeye mwenyewe, inachukua muda mrefu, wananchi wale sasa wanataka kujua hatima ya matatizo yao.

Kwa kuwa aliwasikiliza yeye mwenyewe, mimi sina haja ya kulizungumzia, nadhani mwenyewe atajua namna ya kuhakikisha kwamba wale wananchi wanapata ufumbuzi wa matatizo yao. Vilevile aliwasikiliza wananchi pale Babati na alipata hisia kwamba zipo Idara ambazo wananchi hawana imani nazo, Idara za Serikali na yeye alisema ataangalia upya mambo haya. Kwa hiyo, tunaomba yale mambo ambayo aliwasikiliza pale Babati na kadhalika basi ni vizuri akapata kweli majibu.

Mheshimiwa Spika, zipo ahadi za Serikali ambazo zimeandikwa kwenye kitabu, tunataka kujua na zile ahadi ambazo zinatokana na majibu ya maswali yetu kitabu chake kiko wapi?

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana, naunga mkono. (*Makofi*)

**MHE. JAMES D. LEMBELI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa heshima kabisa, napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kahama kwa kuniwezesha leo hii kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Huu ni mchango wangu wa kwanza tangu niingie katika Bunge hili, nawashukuru sana na naahidi kwamba nitatekeleza yote yale ambayo Chama cha Mapinduzi kimewaahidi na mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Wabunge wenzangu ambao wamempongeza Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri. Ni hotuba ambayo kwa kweli inalenga katika kukidhi matarajio ya wananchi kuhusu maendeleo ya nchi yetu. Kwa sababu hiyo na kwa sababu wengi wamezungumza, mimi nitachangia kidogo katika sekta nne zifuatazo: Sekta ya Utalii, Sekta ya Madini, Miundombinu na mwisho Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii napenda nikiri wazi kwamba mimi ni mdau katika sekta hii kwa sababu karibu ya nusu ya utumishi wangu Serikalini nilikuwa katika Sekta ya Utalii. Naipongeza Serikali kwa mikakati ambayo sasa imeanza kuhakikisha kwamba utalii unachangia kikamilifu katika pato la taifa. Jitihada ambazo sasa hivi zinafanyika za kutangaza vivutio vyetu katika nchi mbalimbali duniani kwa nguvu na

kwa kasi, nasema hilo ni wazo zuri. Lakini mimi nilikuwa na wasiwasi katika Mkakati mmoja ambao umekuwa ukisisitizwa mara kwa mara hapa Bungeni; kwamba Balozi zetu zitumike katika kutangaza utalii wetu katika nchi ambazo wanawakilisha.

Mheshimiwa Spika, mimi ninawasiwasi. Katika uzoefu wangu wa zaidi ya miaka kumi na tano kutangaza utalii wa Tanzania sikuwahi kuridhika na kazi ambayo inafanywa na Balozi zetu kutangaza utalii wa Tanzania. Biashara ya utalii ambayo ni *specialized* lakini pia ni nyeti. Inahitaji watu wenye Elimu inayohusu masuala ya biashara ya utalii.

Ukiangalia watumishi wengi waliopo katika Balozi zetu, taaluma zao si biashara ya Utalii. Wengi taaluma yao ni Diplomasia na hata maelezo wanayatoa kwa watu wanaofika katika Balozi zetu kuulizia maeneo ya vivutio vya utalii Tanzania wengine hawajawahi kufika. Mtalii anafika katika Ofisi ya Ubalozi anataka kujua habari ya Gombe, utakuta Afisa anayemuhudumia hajawahi kufika Kigoma; hajawahi kufika Gombe, kwa hiyo unategemea nini? Ni dhahiri mgeni huyo anaweza kuwa na taarifa nyingi zaidi kuliko ofisa wetu wa Ubalozi aliyopo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine wana wawakilishi katika nchi mbalimbali, naiomba Serikali iangalie maeneo ambayo Tanzania inapata watalii wengi tupeleke watu na walipwe kwa kazi hiyo. Bajeti ya mwaka huu ya *TTB* ni kubwa, hivyo wanaweza kupeleka watu kwa mfano Marekani, Ujerumani, Uingereza na kwingineko. Ni kwa kufanya hivyo tu tutaweza kweli kuitangaza nchi yetu kikamilifu. Vinginevyo kutumia Balozi zetu ni tatizo kubwa. Nitatoa mfanoa mmoja:-

Miaka sita iliyopita mimi nilikwenda Sweden na pale Ubalozini licha ya kuwapelekea Makabrasha yenye habari za karibuni za Tanzania bado walikuwa wanaendelea kugawa makabrasha ya miaka 20 iliyopita ya *TTC.* Sasa mambo kama haya yanaendelea kufanyika. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali ijaribu kuliona hili na kuwapeleka wananchi katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini. Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya hapa nchini ambazo zina madini mengi na hususan dhahabu. Kahama dhahabu inapatikana karibu kila mahali . Hivi karibuni nimesikia redioni kwamba mgodi mpya wa madini ya dhahabu unaitwa Buzwagi utaanza kujengwa nje kidogo ya mji wa Kahama kilomita kama tano. Kwa kutumia Ilani ya Uchaguzi mimi nimeshiriki kikamilifu kuhamasisha wananchi kujiandaa na ujio wa mgodi huu.

Kinachosikitisha ni kwamba nimesikia tayari mkataba baina ya Serikali na Kampuni itakayochimba dhahabu hiyo tayari umeshawekwa. Lakini wananchi wa Kahama wamekuwa wakipiga kelele husasan wale wa maeneo ambako mgodi huu unajengwa hivi sasa wananchi wa Mwendakulima, Mweme na Chapulwa. Kila siku wanalalamikia juu ya fidia zao, hakuna mtu anaweza kuwaeleza kikamilifu kwamba Serikali inasema nini watalipwa kiasi gani na kadhalika. Matokeo yake sasa hivi ni vurugu tupu mpaka inalazimika Mkuu wa Wilaya anakwenda na Polisi kuwajaribu kuwazuia wananchi wenye hamaki wasiwashambulie wale ndugu zangu wa *Barricks*.

Sasa hili naliona ni tatizo kubwa. Mimi niliamini wazi kuwa Mkataba huu utakuwa tofauti na mikataba ile ya nyuma; na kama umefanyika kwa nini umefanyika kwa siri siri hata mwakilishi wa wananchi wa eneo hilo Mbunge, hana habari. Kinachosikitisha zaidi nimewahi zaidi ya mara mbili kuomba Waziri wa Nishati au Naibu wake aje Kahama azungumze na wananchi wa eneo hilo Kata ya Mwendakulima kuhusu haki zao baada ya mgodi huu kuanza kufanya kazi. Mpaka hii leo hakuna na wanategemea mimi Mbunge niende pale nizomewe halafu ndiyo waje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni hatari sana kwa nchi yetu, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe kwamba Waziri wa Nishati anafika Kahama na si kwenda Blyanhulu, anakuja Buzwagi kuzungumza na wananchi wa Kata ya Mwendakulima.

Lipo tatizo, bado makampuni haya pamoja na kuahidi kwamba yatalipa dola laki mbili kwa Halmashauri ambako wanafanya kazi, nasikitika mpaka jana *Barricks* walikuwa hawajailipa Halmashauri ya Kahama dola laki mbili. Na sasa wameanza ujanja, barua na maulizo mbalimbali wakati jambo hili ni lipo wazi. Hela hizi zilitakiwa zitumike kwa maendeleo ya wananchi wa Kahama katika mwaka huu wa Fedha unaokwisha, mpaka leo pesa hizo hawajalipa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sekta ya miundombinu. Mkoa wa Shinyanga, Mwanza, Tabora na Singida tangu uhuru wamekuwa wakililia barabara hii inayotoka Dodoma, Manyoni, Singida mpaka Shelui. Kwa bahati nzuri sana wananchi wa maeneo haya hawana uzoefu wa kupiga kelele, lakini ukimya ukizidi kishindo ni kikubwa. Tunataka barabara hii sasa ya kutoka Dodoma kwenda Manyoni, Singida mpaka Shelui tupewe maelezo ya kutosha lini itakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka hapa Bungeni kila kikao Waziri anayehusika alikuwa anatoa taarifa kuhusu maendeleo ya ujenzi wa barabara hizi. Mwaka huu sijawahi kusikia, siamini hata hiyo pesa iliyotengwa kwa ajili ya kukamilisha barabara hizi kama kweli itapatikana na kuweza kuona kwamba barabara hizi zinapitika.

Mikoa hii ndiyo inayozalisha pamba kwa wingi; mikoa hii ndiyo yenye madini mengi lakini bado mazao yao ukipita Sekenke pale; na wewe mwenyewe umepita, ni hatari tupu! Watu wanapoteza maisha yao. Nikiwa mdogo wakati nakwenda shule ya Sekondari Njombe miaka 30 iliyopita, Sekenke iko hivyo hivyo, tatizo ni nini? Wakati huo huo tunawahamasisha wananchi limeni pamba, limeni mazao ya chakula, watayafikisha vipi Dar es Salaam? Ubovu wa barabara hii unasababisha mateso makubwa sana kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Magharibi. Maendeleo hayawezi kupatikana kama barabara na reli haitapitika hivyo kuweza kufikisha bidhaa katika maeneo haya na zikapatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atupe *time plan* ya kumalizika kwa barabara hizi. Maeneo mengine tumesikia hapa watu wamepiga kelele barabara zao zimekamilishwa na sisi safari hii tungependa kusikia kwenye Bajeti hii tunaambiwa ni lini barabara inayotoka Dodoma kuunganisha mikoa ya Magharibi na Kanda ya Ziwa zinakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sitachukua muda mrefu, nimalizie kwa Sekta ya Mifugo. Kama nilivyoanza kuzungumzia kwenye Sekta ya Madini, Mkoa wa Shinyanga umebahatika kuwa na rasilimali nyingi. Rasilimali watu, maliasili, madini na mifugo. Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa idadi ya ng'ombe Tanzania nzima. Napenda niishukuru Serikali kwa kuwezesha kupatikana kwa mwekezaji ambaye atawekeza katika kiwanda cha nyama kilichopo pale Shinyanga. Naishukuru Serikali kwa sababu hii itawarahisishia wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kupata soko la uhakika la ng'ombe wao. Robo ya ng'ombe wote wanaochinjwa Dar es Salaam wanatoka Shinyanga na wewe mwenyewe ni shahidi. Malori yanayopita hapa yote yale yanatoka Shinyanga. Sasa wananchi wa Shinyanga kwa hakika wataishukuru Serikali kwa kuwawezesha kuwa na soko la uhakika sambamba na Serikali kuwawezesha kupata mwekezaji wa kiwanda cha nyama. Nilikuwa naiomba Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kwamba kiwanda cha maziwa kinajengwa Shinyanga. (*Makofi*)

Kwa hili ningependa kiwanda cha maziwa kijengwe Kahama kwa sababu Kahama ni mji unaokuwa kuliko miji yote ya Mkoa wa Shinyanga. Sambamba na kiwanda cha maziwa, kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga una idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi na kondoo ingekuwa busara kujengwa kiwanda cha ngozi pale mkoani Shinyanga. Hii itawasaidia wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kupata soko la uhakika la zao la ngozi.

Mheshimiwa Spika, ngozi inayopotea mkoani Shinyanga, Mwanza, Tabora , ni kiasi kikubwa sana ambacho kweli kingeweza kupatiwa soko la uhakika, ingeweza kuongeza pato la taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nisingependa kengele ilie wakati nikizungumza, naomba nihitimishe kwa kusema ninaunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda uliosalia wa dakika saba hautuwezeshi ku mwita anayefuata kuchangia. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo Saa Kumi na Moja jioni. Samahani niseme tu kwamba ataanza, Mheshimiwa Katagira, atafuatiwa na Mheshimiwa Shibiliti na baada ya hapo Mheshimiwa Joyce Masunga.

*(Saa. 6.57 Mchana Bunge Liliahirishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*(Hapa Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Alikalia Kiti)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Waheshimiwa Wabunge, habari za Jioni! Ninaomba sasa nimwite Katibu ili atuongoze katika shughuli tunayoanza nayo sa hizi.

## HOJA ZA SERIKALI

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu katika kipindi hiki cha jioni. Kama alivyosema Mheshimiwa Spika, wakati akisitisha shughuli zetu mchana kwamba msemaji wetu wa kwanza saa hii atakuwa Mheshimiwa Katagira, atafutiwa na Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Joyce Masunga ajiandae.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika hoja hii. Wapiga kura wangu waliniomba na kunielekeza kwamba nitumie muda mwingi kutetea suala moja ambalo ni muhimu kwao. Lakini kabla ya suala hilo, kwa muda mfupi naomba nijielekeze kidogo kwa masuala mawili ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Madiwani: Tunashukuru na tunafarijika kwamba Serikali sasa imetambua umuhimu wa madiwani na imeweza kuongeza posho yao maradufu kutoka shilingi 30,000/= kwenda shilingi 60,000/=. Tunashukuru Serikali. Lakini bado kuna tatizo moja lingine kubwa ambalo linawakabili Waheshimiwa Madiwani, nalo ni suala la usafiri. Sisimami hapa katika Bunge hili kusema kwamba Waheshimiwa Madiwani wapewe magari, la hasha! Sisimami kusema kwamba Madiwani wakopeshwe magari, la hasha! Wala sisimami kusema kwamba madiwani wapewe pikipiki, hapana! Lakini naomba Serikali ianzie kwa suala dogo tu. Itoe idhini kwa Halmashauri ili ziweze angalau kuwadhamini madiwani wanapotaka kukopa vifaa vya kusafiria kama pikipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wilaya zetu ni kubwa na pia Kata zetu ni kubwa sana na Mheshimiwa Diwani yeyote anatarajiwa atembelee vijiji, atembelee vitongoji, ahudhurie mikutano na pia aweze kwenda kuhimiza maendeleo hasa ujenzi wa shule, zahanati na kadhalika. Kama hana chombo cha kusafiria huwa anajikuta katika hali ngumu kabisa. Kwa hiyo, naomba kwa dhati kabisa kwamba Serikali iruhusu Halmashauri ziweze kudhamini madiwani katika kukopa vyombo vidogo vidogo vya usafiri hususan pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la *Ware House Receipts*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amelitaja nadhani katika ukurasa wa 14. Kweli huu ni utaratibu mzuri, ni mpango mzuri unaosaidia wakulima waweze kukaa na mazao yao na kuyauza wakati bei ikipanda. Tatizo moja ambalo linajitokezza ni la riba za Benki zinazotoa mikopo ya ku-*facilitate* huu utaratibu wa *Ware House Receipts*.

Benki hizi zinatoa riba ya juu na kwa hiyo zinafanya ile faida ambayo ingepetikana kusaidia wakulima iwe ndogo. Mimi nafarijika kwamba Serikali mara hii imeona suala la riba na katika kujitahidi imetuahidi kwamba katika mwaka huu wa fedha, haitakopa katika Benki za humu ndani. Ni mategemeo yangu kwamba hakika zoezi hilo litafanya riba zishuke angalau kidogo.

Kwa hiyo, mimi naiasa Serikali iweze kuangalia namna ya kusaidia mpango huu wa *Ware House Receipts* angalau Benki ziwapatie riba ambayo ni tofauti na inavyo-*charge* katika shughuli zingine za biashara zake kwa sababu hii ni kuwasaidia wakulima, ni kuwasaidia watu ambao wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze katika suala muhimu ambalo nimeelekezwa na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kyerwa kwamba niliongelee kwa kirefu kabisa. Suala hili ambalo ni muhimu ni ombi la wananchi wa Wilaya ya Karagwe hususan Jimbo la Kyerwa kuomba kwamba Wilaya ya Karagwe igawanywe katika Wilaya mbili; Wilaya ya Karagwe na Wilaya ya Kyerwa. Wilaya ya Kyerwa ikiwa ni maeneo ambayo ni Jimbo langu la Uchaguzi, Jimbo la Kyerwa, sasa liwe Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu nyingi za kuomba Wilaya hii igawanywe. Kwanza, Ukubwa: Wilaya ya Karagwe ni Wilaya kubwa sana. Katika Wilaya nane ambazo zinaunda Mkoa wa Kagera, ndio Wilaya kubwa kuliko Wilaya zote hizo. Lakini pia Jimbo la Kyerwa ambalo naomba litengwe liwe Wilaya ya peke yake, ni kubwa sana. Jimbo hili lina Kata 11, lakini ukichukua Kata 3 peke yake; chukua Kata ya Nkwenda, Kata ya Mabila, Kata ya Kamuli, ziunganishe pamoja zinazidi kwa ukubwa wa eneo baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kagera. Kata hizi tatu zinazidi Wilaya ya Chato, Wilaya ya Misenye, hizi Wilaya na Wilaya ya Bukoba Vijijini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karagwe ina idadi ya watu wapatao karibu nusu milioni. Lakini pia Jimbo la Kyerwa ambalo wananchi wanaomba ligawanywe kama Wilaya ya Kyerwa, lina mbuga za kuhifadhi wanyama (*Game Reserves)* mbili kubwa. Lina *Ibada Game Reserve* na *Rumanyika Game Reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni kwamba Jimbo la Kyerwa linapakana na mataifa mawili: Taifa la Uganda kwa upande wa Kaskazini, Taifa la Rwanda kwa upande wa Magharibi. Sisi tunasema kwamba hizi ni baraka kwa sababu tuna majirani, tufanye nao biashara tuendelee. Lakini pia mipaka hii ina matatizo yake. Baadhi ya majirani zetu wamekuwa na hulka ya vita kwa miaka mingi. Kwa hiyo, utakuta kwamba mipaka hii ina- *facilitate* ujambazi *(Cross Border Banditry).* Mipaka hii ina–*facilitate* uingizaji wa silaha. Ninapoongelea silaha, siongelei bastola, au *Rifles*, ninapoongelea silaha, naongelea silaha za kivita, *Sub-Machine Guns, Machine Guns, Grenades*. Lakini pia hii mipaka ina-*facilitate* wizi wa mifugo na uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoomba Wilaya ni mategemeo yetu kwamba tukishapata Wilaya, basi vyombo vya Serikali vitakuwa karibu na sisi na vitaweza kushughulikia kikamilifu masuala haya ya ujambazi, uingizaji silaha, uhamiaji na uwizi wa mifugo kwa karibu zaidi. Kwa mfano, kama tuna Wilaya yetu sisi wenyewe, ina maanisha tutakuwa na *OCD* wetu. Kama kila wiki mbili akipiga *patrol* sehemu za mipakani na vijana wake, nina hakika kwamba watu wanaokuwa wanapanga mipango ya kuingiza silaha, kuiba mifugo, kufanya ujambazi, ziara za namna hii zitakuwa ni

*deterrent* (Mzungu anasema) na zitafanya masuala haya yasitokee kwa wingi kama yanavyotokea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya Wilaya ya Karagwe kuwa kubwa, huduma kwa wananchi ziko mbali nao. Kituo cha Polisi Kikuu cha Wilaya kiko mbali, Mahakama ziko mbali. Wako wananchi ambao wanaishi vijiji ambavyo ni zaidi ya kilomita 200/220 kutoka makao makuu ya Wilaya.

Mwananchi kama ana madai na inambidi ahudhurie kesi katika Mahakama ya Wilaya, inabidi alipe shilingi 20,000/= kwenda na kurudi. Lakini kama kesi inachukua siku tano/sita, inabidi sasa atafute *Guest House* ya kulala, atafute hoteli ili awezwe kuhudhuria kesi. Inakuwa mbaya zaidi ambapo kesi inahitaji mashahidi watano/sita, wote inabidi wasafirishwe waende kwenye Mahakama hiyo, walipiwe gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukipata Wilaya, na Hakimu wa Wilaya atakuwa karibu na wananchi. Vyombo vya Utawala vitakuwa karibu na wananchi, maofisa Elimu, maofisa kilimo na kadhalika. Wananchi wa Jimbo la Kyerwa, wanayo sababu kabisa ya kuomba watengewe Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijiuliza kama wataamua kutenga ziwe Wilaya mbili je, uchumi utahimili kuendesha Wilaya hizi, nakuhakikishia kwamba katika Mkoa mzima wa Kagera, Wilaya ya Karagwe inaongoza katika uzalishaji wa kahawa na maharage. Maharage ya Karagwe yanaliwa Bukoba, Rwanda, Burudi, Kahama, Geita, mpaka Dar es salaam. Tunazalisha ndizi kwa wingi, mifugo kwa wingi. Hii ni sababu tosha ya kugawanya Wilaya ya Karagwe zikawa Wilaya mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongea na watawala, ukiongea na Serikali, sababu moja kubwa wanayotoa ni kwamba gharama za kuanzisha Wilaya zitakuwa kubwa. Nakuhakiishia kuwa katika kutenga Jimbo la Kyerwa likawa Wilaya, hakutakuwa na gharama za ajabu. Kwa nini? Kwa mfano, hospitali ya Wilaya, tayari tuna Kituo cha Afya ambacho tumekiendeleza sisi wenyewe wananchi tukishirikiana na Halmashauri yetu na hiki Kituo k imekwishafikia kiwango cha kuweza kuwa Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe alitupa heshima ya kuja kufungua *Theatre* yetu ya upasuaji na hata akauliza ni kitu gani kinakosa kukifanya Kituo hiki kisiwe hospitali kamili. Kwa hiyo, suala la hospitali, tayari lipo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi: Tayari tuna Kituo cha Polisi kizuri na kikubwa ambacho kina hadhi ya kuwa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Kituo hiki kilijengwa na *UNHCR* wakati wa ujio wa wakimbizi. Tukijiuliza majengo ya Utawala yapo baadhi ya majengo tayari. Lakini wapiga kura wangu wamenihakikishia kwamba tamko likitoka kwamba tunapata Wilaya, katika ujenzi wa Jengo la Utawala (*Administration Block)*, wananchi watajitolea vifaa vyote ambavyo siyo vya Kiwandani. Wataleta mawe, kokoto, mchanga. Hivi ninavyoongea tayari nina *offer* ya matofari ya kuchoma nusu milioni ya kujenga *Administration Block*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadiriki kusema kwamba ombi la wananchi wa Jimbo la Kyerwa kupata hadhi ya Wilaya ni dogo. Wananchi wanaomba ruhusa toka Serikali ili waweze kushirikiana na Serikali na kujisogezea maendeleo yao wenyewe. Nikiwa na imani kwamba Serikali italiangalia suala hili kwa huruma kabisa, nasema ninaunga mkono hoja hii na pia nakushukuru tena kwa kunipa wasaa huu wa kuchangia katika hoja hii. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kutoa pole kwa ajali ambayo kwa kweli ni ya kutisha, karibu watu 58 wamefariki ndani ya wiki mbili hizi kutokana na ajali mbali mbali. Lakini, pole za pekee nizielekeze kwa wanaushirika, nikianza na Mzee Buberwa ambaye ni Mwenyekiti wetu wa *KCU* kule Kagera ambaye mtoto wake amefariki kwenye ajali ya Basi la Mohamed *Trans*, alikuwa anakwenda kwenye *field* kule *TANICA* na Mwenyezi Mungu akamwita kwa njia hiyo. Pili, nitoe pole kwa wanaushirika wa Mkoa wa Shinyanga *(SHIRECU)*, ni juzi tu Mwenyekiti wetu wa *SHIRECU*, Sitta Matagulwa naye amefariki dunia kutokana na ugonjwa uliomsibu akiwa Dar es salaam kufuatilia masuala ya wanaushirika wa Shinyanga. Na hii ya juzi tu ambayo wanaushirika wenzetu wa Mkoa wa Mwanza watatu wameitwa na Mwenyezi Mungu kwa hali ambayo ni ya kutisha, basi tumwombe Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi, Amin!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba ambayo kwa kweli ameiandaa vizuri, si yeye tu, lakini ni pamoja na watalaamu wake wote wakiwemo Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara yake. Nampongeza sana, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu! Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu bila kuwasahau watendaji wake wakuu ambao wanamsadia sana, Wakuu wetu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri, wanafanya kazi kubwa sana.

Baadhi yao wako hapa, si rahisi kuwataja wote kwa sababu amekwishawataja Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya wale tunaowafahamu kuwa ni wachapa kazi: Mheshimiwa Kandoro yupo, Mheshimiwa Babu, Mheshimiwa Said Kalembo, Mheshimiwa Shirima na Ndugu yangu ambaye tulikuwa naye kwenye Kamati ya Ushirika, Mheshimiwa Tarimo ambaye sasa hivi yuko Kusini. Hongera sana kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu ni nzuri imegusa Wizara nyingi. Kwa kipindi cha mwaka mmoja amefanya kazi nzuri sana. Yapo mengi, ukiangalia tu hivi utaona kwamba huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli ifike mahala tukubali kwamba kazi inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu kwanza nigusie kwa *data* hali ya barabara yetu kutoka Dodoma-Singida–Shinyanga–Mwanza. Nimeona katika kitabu chetu hiki cha Maendeleo kuna shilingi bilioni 28.1 kwa Dodoma – Manyoni, kuna shilingi bilioni 11.2 kwa Singida–Manyoni, lakini kuna shilingi bilioni 10.6 kwa Singida-Shelui. Haya yote

ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kinachotakiwa hapa, sana sana ni kwamba Umma uelewe kwamba haya mamilioni yatatekelezwaje? mipango ikoje? Tutaanza lini na tutakamilisha lini ili angalau wananchi waweze kuelewa kwamba Chama cha Mapinduzi hakina mchezo katika kutekeleza Ilani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja moja ambayo ningependa tu labda nitapata ufafanuzi, *either* ni *typing error* au ni makosa gani hayo: Mwanza – Shinyanga *Border*, *Rehabilitation*, kuna shilingi milioni 200. Shilingi milioni 200 kwa kweli kidogo imenishitua! Ni fedha ambazo kwa kweli ni kidogo mno, maana matengenezo ya lami kuanzia *Border* ya Shinyanga kwenda Mwanza wala siyo viraka, sasa hivi kilomita moja utasema kiraka? Kwa hiyo, inatakiwa hapa wataalamu wajaribu kuiangalia kama ni kweli hii shilingi milioni 200 haitoshi! Sehemu za Ilula kule barabara imekwisha, panatakiwa matengenezo ya hali ya juu. Unakuta kilomita mbili zimefumka zote zile. Sasa ifike mahala wataalamu wetu wa fedha waangalie kuona kwamba fedha hii ni kidogo na haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumzia barabara ya Usagara–Geita mpaka kule Kamyola. Kwa kweli tulipiga piga kelele sana. Lakini, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu safari hii imeona kilio hicho kwamba kisiendelee, imetenga shilingi bilioni 40 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Kwa kweli hapa sina hoja. Ninachotaka nielezwe tu ni kwamba hizi shilingi bilioni 40 zitaanza kufanya kazi lini na ni kazi zipi ambazo zitafanyika ili angalau wananchi waweze kuelewa kwamba kuna nini kinachoendelea katika shilingi bilioni 40 hizo kwa kipindi hiki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ufungue Jiji la Mwanza, ni vyema magari yanayotoka Kenya yaje mpaka pale Kisesa yakate kona zake, halafu yanyooshe kuja Usagara moja kwa moja mpaka Burundi , inaitwa Nyanguge – Musoma *Bypass*. Hapa imenichanganya! Unakuta kuna shilingi bilioni 1.4, sasa hii ni lami kweli utatengeneza hapo Usagara kwenda Fera -Bujingwa-Kisesa, bado uende mpaka kule Nyanguge, uende mpaka Musoma! Fedha hazitoshi! Nitahitaji ufafanuzi tu, watu wa Miundombinu watatueleza ni kazi zipi zitakazofanywa? Shughuli zinaendelea, wako wapembuzi wanaweka mambo na nini…wanaonekana! Sasa tuelezwe kazi zitakazofanyika ili watu wajipange, kama watapata fidia ili waweze kuanza na shughuli zingine wapishe ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nijielekeze kwenye suala la mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga. Labda nianze tu kwanza kumpongeza Waziri Mkuu tena kwamba yeye ndiye mwanzilishi wa mradi huo na kwa kweli anastahili kupongezwa kwa aina ya pekee kwa wananchi wa Kahama, Shinyanga na Vijiji 54 ambavyo vitafaidika na maji yatakayowafikia hivi karibuni. Shughuli zinaendelea. Mwaka wa jana nilizungumzia juu ya vijiji ambavyo vilisahaulika, viko ndani ya kilomita tano. Kwa kweli Imefika mahala wataalamu labda tuwape nafasi, wamedai kwamba awamu ya pili watavihusisha vijiji vingi zaidi, na mimi nimeona kwamba basi hilo tuliache, tusubiri awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, ule mradi ni wa mabilioni ya pesa na ni muhimu sana kwa wananchi wa Kahama na Shinyanga, cha msingi, huko porini barabara ya kwenda kule haitamaniki. Mheshimiwa Waziri wa Maji juzi juzi amefika kule, wakati wa kurudi alibadilisha njia. Sasa niiombe Serikali ijaribu kuona kwamba suala hili ni la msingi, umeweka mradi wa mabilioni mahala fulani na ni muhimu sana kwa wananchi watakaotumia maji hayo, barabara ile ipandishwe hadhi, itoke kuhudumiwa na Halmashauri iwe ya Mkoa. Itahusisha vijiji vya Buhingo, Seke, Nyamainza, Mbalama, Isesa mpaka Nyangomango ambako wengine wanaita Ihelele. Ihelele ni kitongoji, lakini kijiji ni Mangomango, ni vyema rekodi zikaingia vizuri ili angalau muelewe hivyo. Kwa hiyo, naomba hiyo barabara ipandishwe hadhi iwe kwenye hadhi ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwashukuru hawa Wakandarasi wanaojenga, wameziba mashimo, lakini hawajaikarabati *(reform)* ile barabara kwa maana ya kwamba pawe na mitaro ya kumwaga maji. Wameziba vizuri, tunawapongeza. Lakini, cha msingi barabara irudi kwa wenyewe kwa maana irudi ihudumiwe na Serikali upande wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bila kuzungumzia maji ya Misungwi, nitakuwa sijatenda haki. Maji ya Misungwi, karibu viongozi wote wa Kitaifa wamezungumzia. Rais wa Awamu ya Tatu ameyazungumzia, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi alifika pale, akazungumzia, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Shein alifika akazungumzia, Mheshimiwa Rais mwenyewe amefika pale akiomba kura, akayazungumzia na amerudi tarehe 8 Mei, akawahakikishia wananchi wa maeneo hayo wataopata maji kupitia *MCC*.

Wakati anatoa ahadi hiyo, bahati ya pekee, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Ofisi ya Umma, Mheshimiwa Anthony Diallo na Mheshimiwa Mohamed Seif, walikuwepo. Sasa nina mashahidi watatu kwenye Baraza la Mawaziri, kwa hiyo, nina imani kabisa itakapofika hoja ya kugawanya *MCC*, nadhani Misungwi itakuwa imepewa heshima ya pekee kutokana na sauti ya Mheshimiwa Rais ambayo kwa kweli ni ya aina ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano huo mambo mengi yalijitokeza. Rais alipata fursa ya kutembelea hospitali yetu ya Wilaya ambayo unaweza kusema ni Kituo cha Afya – jina ni Hospitali ya Wilaya! Alifurahishwa na jinsi watumishi walivyoweza kutoa chanjo karibu kwa asilimia mia moja na zaidi, akaahidi, *Ultra Sound* itafika Misungwi na Hospitali ya Wilaya ya Misungwi itakuwa kwenye hadhi ya kiwilaya, kwamba "nimefika hapa mimi Mheshimiwa Rais hospitali hii nadhani na yenyewe inapaswa ipanuliwe ifikie kwenye hadhi yake". Sasa hebu wahusika nijaribu kuwauliza imekuwaje hapa sijaona fedha za upanuzi wa Hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa watumishi, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, katika mkutano wa hadhara aliahidi kwamba angeliongeza watumishi. Naomba nimwarifu kwamba mpaka sasa kutokana na kasi yake ilivyo, watumishi 53

amekwishawapangia kuja Misungwi na 12 tayari wamekwisharipoti na wameanza kufanya kazi. Hongera sana Mama yetu kwa kazi nzuri unayoifanya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pembejeo: Sehemu nyingi wananchi wanasumbuka na pembjeo. Sisi watu wa Kanda ya Ziwa, tunahitaji ruzuku kwenye dawa za pamba. Tuna matatizo makubwa kweli, zao la pamba bila kunyunyuzia zaidi ya mara sita, hutapata zao lolote. Tunaomba tufikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za Mkoa: naipongeza sana Serikali, barabara ya Fulo - Nyambiti ilitengewa pesa kidogo, naomba safari hii itengewe pesa za kutosha.

Mheshimiwa Ndassa ni shahidi kwa Mkutano wa *RCC*, tulivutana kutokana na shilingi karibu milioni 40, safari hii barabara ya Fulo Nyambiti itengenezwe hususan kwenye daraja la mto Kanyerere pana matatizo kweli. Sasa shilingi milioni 80 utatengeneza nini? Nadhani ifike mahali tuangalie barabara hiyo.

Serikali za Mitaa tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwafikiria Waheshimiwa Madiwani. Shilingi 60,000 si haba kwa kuanzia, lakini labda ingetamkwa kwa maana kwamba waanzie shilingi 60,000 halafu kikubwa, naomba kama inawezekana wakopeshwe vyombo vya usafiri. Wanahangaika kweli, watalipa, wana uwezo, jamani wapeni vyombo vya kusafiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo basi mimi niseme tu kwamba mambo mengine tutaendelea kufuatilia kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia 100. Ahsanteni sana! (*Makofi*)

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini nianzie na pole, tumepata msiba, sasa hivi ndugu yetu Peter Matagulwa, Mwenyekiti wetu wa *SHIRECU* Shinyanga amefariki. Nichukue nafasi hii kuwapa pole familia na wananchi wa Shinyanga kwa sababu anatuhusu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipindi hiki tumepata ajali nyingi na Waheshimiwa Wabunge, tumeendelea kutoa pole. Lakini hili basi la *Mohamed Trans* ni basi la Shinyanga na ndio mabasi yetu tunayoyaamini, tumesikitishwa sana. Lakini kwa vile Mkuu wa Mkoa yupo tutaenda kuwaweka sawa, wasije wakawamaliza wananchi kwa sababu ndiyo mabasi ambayo tunayaamini. (*Makofi*)

Lakini nichukua nafasi hii kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Singida, amefanya kazi kubwa na wananchi , viongozi wa kule na Wabunge wa Mkoa wa Singida. Wamewazika ndugu zetu. Kwa kweli basi lile wananchi wa Shinyanga na Mwanza ndiyo walikuwemo wengi. Tunachukua nafasi hii kuwashukuru sana tunasema ninyi ni ndugu zetu mmewazika ndugu zetu, Mungu awajalie na atawazidishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pole hizo mimi niende moja kwa moja katika suala la elimu. Katika elimu kwanza tunashukuru bajeti yetu tumepewa asilimia 18 lakini kwa Mkoa wa Shinyanga tunashukuru zaidi, kwani tulikuwa na shule 78 lakini mpaka sasa tumejenga shule 264. Nimesema hili kwa kumshukuru sana Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru ulituita Mkoa wa Shinyanga, viongozi wote na ukatuagiza na kusema kwamba haiwezekani Mkoa mkubwa ukawa na shule 78, ukasema tujitahidi na sisi kweli tulijitahidi, tunamshukuru Mkuu wa Mkoa na hivi ni afande ulipomwambia aliseme ndiyo afande akaenda kutekeleza kazi.

Tunamshukuru amefanya kazi hiyo na nachukua nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wa Mkoa wa Shinyanga wa Chama na Serikali na wananchi wote kwa kuchangia, mpaka sasa tuna shule 264 na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu ametupa walimu na walimu hao wapo wanakula raha mstarehe Shinyanga ni safi, walimu karibuni Shinyanga mje kula raha Shinyanga! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mimi nilikuwa nasema hapa Wabunge wanawake ukituangalia na Waheshimiwa Mawaziri, wengi tumesomea shule za bweni. Sasa hivi watoto wetu wanasoma shule za kwenda na kurudi nyumbani, kwa kweli hatuwatendei haki. Katika Mkoa wa Shinyanga tuna zile ngoma zetu, zamani mlikuwa mnaona zinaitwa *Chagulaga* si mnazijua!

Sasa hivi tuna minada, watoto wanapofika miaka 13 na 14 wanaibukia wasichana wazuri, mnawajua wanapendeza, wanapofika pale wanawekewa kigingi na wavulana hakuna kupita, mtoto atapitia wapi? Lakini akiwa katika shule ya bweni mtoto atakaa shule atasoma safi, ataweka vitabu mambo yatakuwa safi. Tunaomba shule za bweni kwa wanafunzi wa shule zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, naomba ukae chonjo maana zaidi ya shule 300 wakati sisi tuna 264. Mheshimiwa Balele hapo anakutazama kwa jicho la upande karibu tunakufikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Elimu. Shinyanga tulikuwa tunalilia Chuo cha Elimu kiwe wapi, wapi tutapata! Lakini sasa tumepata Chuo cha Elimu *SHYCOM* na wamesema kuwa walimu wanaanza kuja mwezi wa Julai. Kwa niaba ya Mkoa wa Shinyanga nikiwa Mbunge wa Mkoa ule, natoa shukrani nyingi. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri kwa taarifa ambazo tumepata Chuo hicho watakuwa wanafundishwa mambo ya biashara. (*Makofi*)

Lakini tunasema shule hizi 264 ni nyingi nao walimu hawatafundisha Shinyanga tu watakwenda mikoa tofauti, tunaomba basi mchanganye michepuo yote iwe ya biashara, iwe ya Sayansi na *Arts* kwa kadri mtakavyoona inafaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika elimu, baada ya kuona asilimia 18 imefika kuna watu wanasuuza midomo sasa hivi tayari kwa kula hizo fedha. Sasa tunasema fedha za MMEM haziliki, mnaona hapa Bungeni tunavyohangaika

kuzungumza. Kama mnaanza kusuuza midomo yenu tayari kwa kula hizo hela tunasema hizo hela haziliki na jasho litawatoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema yafuatayo: Majuzi hapa mmeleta *JK Boys,* wamekuja ndani tumewapongeza, kipindi kile tena mkaleta wanafunzi wa shule hapa tukawapongeza waliofanya mitihani vizuri. Hivi kwa nini walaji hela wazuri sana tusiwalete hapa na sisi tuwazomee waonekane kwenye runinga? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hizi fedha Mheshimiwa Waziri wa Elimu aziangalie, mambo ya elimu anaweza akasema kuhusu madarasa lakini naomba waangalie mambo yafuatayo: Kwanza, kuna fedha za chakula katika shule za bweni. Watoto wanakula chakula kibaya, maharage yameoza, ugali una wadudu, kwa nini wanakula chakula hicho wakati hela zinatoka? Ukiona shule nzuri watoto wanakula vizuri hakuna migogoro katika zile shule za Sekondari ujue mwalimu mkuu wa shule ile anaongea na viranja wa shule ndiyo wanapanga chakula wale chakula cha aina gani kwa wiki. Kwa hiyo, mimi natoa wito kwamba naomba viranja wakuu wa shule kuweni macho na hela hizi , hakikisheni wanafunzi wenzenu wanakula chakula kizuri kama kande, kande safi na siyo kande zilizooza. Mahindi yapo mengi hapa, huko Rukwa mahindi mengi, kwa nini tule kande zilizooza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalonitia wasiwasi ni zile fedha wanazotoa kwa wale watoto wenye familia maskini na watoto yatima. Watoto wanaosomeshwa nchini hapa wako si chini ya 45,000 lakini mtoto yule anaambiwa saini hapa, kazi yake kusaini, hajui kapewa shati na kaptura, shati na sketi au na kitu gani, basi kieleweke huyo mtoto anapewa kitu hicho kwa ajili ya nini na nini siyo unamsainisha bila kujua utaratibu, naomba utaratibu huo uwe wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo, nimeshasema *Taifa Star, JK Boys* tuliifurahia hapa. Lakini nasema michezo ipo mingi , mwingine Mbunge amesema kuna ngumi, kuna *netball*, kuna *handball,* mimi kama mwanamke nasemea *netball* ipo wapi sasa hivi? Tulikuwa tunaisikia *netball*. Gerezani pale watu walikuwa wanajumuika kutoka kazini kwenda kuangalia wasichana wanavyoruka namna hii, hamna sasa hivi! *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nauliza, na sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri Bendera yupo, nataka nimuulize Mheshimiwa Bendera, hivi *netball* viongozi waliochaguliwa wapo? Kweli wanafanyakazi? Kuna mama mmoja alikuwa anaitwa mama Ana Kibila, alikuwa anafanya shughuli kweli kweli, mara leo watu wanakutana Mara, mara kesho Mbeya, sasa timu zimelala hatuelewi chochote kinachoendelea. Hivi Mheshimiwa Bendera unafanya nini? (*Makofi*)

Leo tunasema Rais amemleta *Maximo* na sisi tungeletewa *Maximo* wa kike, *Maximo* wa kike naye angekuja kutufundisha *netball*, yuko wapi? Viongozi wa *netball* mmelala naomba muamke! Viongozi sisi Wabunge wanawake tunakasirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi nataka niwaulize hawa watu *football* akina Mzee Tenga, *football* inachezwa na wanaume na wanawake, wapo wasichana wanacheza *football,* wanaume na wanawake.

Wapo wasichana wanacheza *football,* na *netball* wanacheza wanawake na wanaume, sasa mimi nimuulize Mheshimiwa Tenga, jamani na Mheshimiwa Naibu Waziri, huyo *Maximo* kwa nini asifike huku na akaenda akawafundisha wasichana wanaocheza *netball, fifty fifty,* mwanangu haipo! *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho, katika michezo fedha za maendeleo, sijui kama zipo itakapofika michezo katika Wizara ya Utamaduni na Michezo, ituambie maana sasa baada ya Kiwanja cha Dar es Salaam, kuwa kinafanyiwa matengenezo sasa tumehamia Mwanza, Mwanza tunasema hii michezo ipo sehemu nyingi, viwanja viko popote, tunaomba mtusaidie na sisi Shinyanga wapo na Dodoma hapa tungekuja kuangalia. Tunaomba vitengenezwe hivyo viwanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya tuna bonde la ufa limekuja. Bonde la ufa hapa tumehangaika, tukasema hapa Watanzania tutakufa. Lakini tunashukuru, tumeambiwa tusile nyama, wote tukaacha, uongo wote tumeacha kula nyama! Sasa huu UKIMWI kama ungekuwa upo hapa aah! tungepona lakini sasa bahati mbaya mnajua wenyewe! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 35 na 50 mimi umenifurahisha sana. Kwanza, umenifurahisha kwa sababu amesema katika hospitali 11 Shinyanga imo katika ukarabati, kwa niaba ya Mkoa nachukua nafasi hii sana kukushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia afya, nasema Ukimwi tunakwenda kupimwa bure pamoja na *TB,* dawa tunapewa bure, lakini mnasema malaria inaua sana, kama inaua sana kwa nini tusipime malaria bure na kupewa dawa bure? Tupewe *Alu* bure, na kweli malaria inaua kuliko UKIMWI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja mpaka kwenye hotuba aliyosoma Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba tarehe 14 mwezi Julai ni siku ya kitaifa katika kupimwa virusi vya Ukimwi duniani. Nimshukuru sana Rais, mimi nasema twendeni tukapime wananchi, na Wabunge basi tuwe wa kwanza kupima. Lakini nivyojiuliza je, huko kupimwa kutakuwa ni kupimwa endelevu au ni mwaka huu tu? Je, vitendea kazi viko katika Wilaya? Je, watalaamu wapo? Maana yake tusije tukafika kule tutakuta watu hawapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisisitizia ni suala letu la kilimo. Tumekwishazungumzia Shinyanga, mnajua Mkoa wetu ni mkame na sisi kwa kweli akili yetu yote tunajua kwamba wenzetu wanatusaidia tupate kilimo cha umwagiliaji. Mipango tumekwishaifanya, lakini sasa bajeti ya kilimo nimeona kama ni ndogo. Sasa swali, hivi umwagiliaji utakuwepo kweli Shinyanga jamani? Hebu tusaidiane kwa mfano, Kishapu tu tuna mto Tungu na Mto Mangu, miwili tu inaweza

kufanya kazi hiyo, kwa maana ya Wilaya hiyo. Lakini vilevile maofisa Kilimo wa Kata tunaomba basi muwakopeshe angalau usafiri na hapo hapo muwajengee nyumba ili watusaidie vizuri katika kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Kwetu sisi Shinyanga hatuna ofisi ya Wabunge wa Viti Maalum. Kwa vile Mkuu wa Mkoa yupo na hoja hapa imetoka, tunaomba hizo hela jamani mpeni na sisi tupate ofisi kwani tunafanyia kazi nyumbani! Lakini mwenzetu Mbunge wetu wa Kisesa kwa kweli jimbo lake lipo mbali, lipo Mwandoa, ni kilomita 60 kutoka mjini Meatu. Tunaomba mumpe naye ofisi kwa sababu anafanya kazi katika ofisi ya Watendaji wa Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo nachukua nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Meghji, Waziri wa Fedha. Kwa kweli umeweka maneno mama tumekusikia, na Wabunge tulikuwa na jambo tumelikataa wote, na wewe na jopo lako ukasema unatuunga mkono. Umekataa mafuta ya taa, bei itakuwa ile ile, nasema hongera sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa wito kwa wapiga kura wangu wa Mkoa wa Shinyanga ambao wamenipa kura za kutosha, nasema ndugu zangu tarehe 14 Julai, 2007, tusiogope, twendeni tukapimwe mkoa mzima tujue mbivu na mbichi. Maana ukijua wewe unao una uhakika wa kuishi maisha marefu, una uhakika wa kuwaweka vizuri watoto wako wawe na wewe mwenyewe kujiweka vizuri. Utaendelea na zoezi, vidonge, utakunywa, utaishi usiwe na tabu. Kapimwe na usiusambaze na usiseme kwamba ukipimwa kama kijana basi hutaoa, unamchukua mwenzako ulioathirika naye unafunga ndoa nzuri na mimi nitakuchangia tu, utameremeta na kuishi maisha ya raha mustarehe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii kukushukuru tena, na nasema nimeiunga mkono hoja hii asilimia mia. Ahsanteni sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Huyo ndiyo Joyce Masunga, Mbunge wa Viti Maalumu kutoka Mkoa wa Shinyanga. Tunashukuru Mheshimiwa Joyce.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda nimpongeze yeye mwenyewe binafsi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu tafadhali tumsikilize sasa Mheshimiwa Telele!

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye binafsi kwa hotuba yake nzuri. Niwapongeze Mawaziri walioko katika Ofisi yake, watalaamu mbalimbali kwa kutuandalia hotuba nzuri sana na mimi mwenyewe huenda mwishoni huko nikasahau, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ya kuchangia kwanza kuhusu suala zima la ulinzi na usalama. Suala hili limetajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 37 na 38. Lakini napenda kunukuu sehemu fupi, "kwamba majeshi yetu katika kipindi hiki yalijijengea utayari na utimamu ili kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa nchi, watu na mali zao". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ulinzi na usalama ni jukumu la kikatiba la Serikali yoyote na hasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi kule Ngorongoro tumeathiriwa sana na Wasomali. Wasomali siyo watu wazuri hata kidogo, ni watu ambao wanalipiza kisasi sana. Nimesoma juzi katika magazeti kwamba kuna Wasomali wamepewa uraia wa Tanzania, pengine taratibu zimefuatwa, lakini bado ningependa pia kuiomba Serikali iwaangalie watu hawa kwa makini sana, vyombo vinavyohusika wafanye uchujaji kuhusu watu hawa kwa makini sana. (*Makofi*)

Maeneo ya vijiji vya Pinyinyi kule Moniki, Angaleselo, Masusu, Malambo, Maloni, Arashi, Olbalbal na Yobi, ni maeneo ambayo yameathirika sana kutokana na tatizo la Wasomali. Hayo ni maeneo ambayo yanakaliwa na Watanzania wa jamii ya Kimasai. Watu hawa wana silaha duni, wana Sime, mikuki na rungu, silaha ambazo kwa kweli hawawezi kuzitumia kukabiliana na Wasomali ambao wanatumia silaha za moto. Wanatumia *SMG*, *AK47* hata silaha za *Section* kama silaha kubwa ya *LMG*. Kwa kweli katika kipindi fulani wametuua, wametuumiza sana sisi wananchi wa vijiji hivi. Wanapoingia mmoja mmoja au wawili au watatu wanaingia kwenye maboma na kuwaua watu, wanabaka wanawake, ilifika mahali kwa kweli mpaka jeuri yao ikawa kubwa wakamuua *ODC* wa Wilaya ya Ngorongoro mwaka 2001. Ilipofikia hatua hiyo kwa kweli hasira ya Serikali iliungana na hasira ya Wamasai. Wasomali walikuwa na tabia ya kuingia kwenye boma, wanaangalia mbuzi au dume. Msomali anamchukua mbuzi kwenye boma na kwenda kumchinja huku akimwacha Mmasai hana la kufanya kwa sababu ukipambana naye atakulipua kwa risasi.

Naishukuru sana Serikali, baadaye mwaka 2001 ilifanya operesheni ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kuwaua watu hao na kutokomea kabisa. Lakini kama ninavyosema ni watu ambao wanaangalia hali ikoje. Wamekwenda, wamerudi tena juzi juzi hapa wamekuja na kuwaumiza wananchi katika vijiji hivi na Serikali kwa mara nyingine tena ikaweka operesheni ya polisi na askari wa *game* wa mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro pamoja na wa *TANAPA,* wamewasaka na kuwapata wachache lakini wengi wao wametokomea na kuingia nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii nao katika hili la Wasomali hawako salama. Kwa sababu juzi tu mwezi Mei kule *Olbalbal* waliwateka nyara watalii na taarifa zilipelekwa polisi, lakini polisi mpaka watoke Arusha kilomita 430. Kule barabara hakuna, kuna barabara mbili tu, za kwenda Loliondo ama unapita Karatu unaingia lango kuu la Ngorongoro unakwenda *Oldvai Gorge* unakatisha mbugani, unafuata mwelekeo tu, hakuna tena barabara ya kwenda Loliondo. Barabara nyingine ni hii ambayo inatoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mto wa Mbu pale kupitia Ngaluka kwenda mpaka Ngaleselo na kupandisha kwenda Loliondo.

Barabara zote mbili ni mbaya sana. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu tarehe 23/3 Mheshimiwa Rais alifanya ziara katika Wilaya ya Ngorongoro. Nimshukuru pia Mkuu wa Mkoa , watu wa Usalama wa Taifa walikuwa wana shida sana, walisita sana kumpitisha Rais katika barabara hiyo kutokana na ubovu. Lakini Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Kanali Samwel Ndomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli walimshawishi na yeye mwenyewe Rais wetu kwa sababu ni askari vile vile hakuona kama kuna tatizo la kwenda Loliondo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amepita ile barabara inayopitia Ngaleselo na kujionea mwenyewe, akalala Loliondo mjini wakati wa kurudi akapita ile ya Mbungani ambayo hakuna barabara unafuata mwelekeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Rais, amepata picha nzuri sana ya huko Loliondo, ni Wilaya ambayo imejifunga kwa muda mrefu sana. Hakuna mawasiliano ya barabara, mawasiliano ya simu, umeme, hakuna kitu chochote na ndiyo maana katika mpaka wa Kenya na Tanzania kuna njia nyingi sana za panya ambazo hawa Wasomali wanapita na ndiyo inakuwa shida sana kuwadhibiti. Ndiyo sababu nataka nipendekeze mambo yafuatayo kwa upande wa ulinzi na usalama. Kwanza, mafunzo ya mgambo yaimarishwe katika maeneo ambayo ama ni mapito ya Wasomali au ni maeneo ya watalii. Mafunzo haya kwa kweli ya mgambo yaimarishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo tunaweza kutumia kukabiliana na suala hili ni taratibu za kuomba silaha. Kuna zile silaha zinazomilikiwa na raia, urasimu wake ni mkubwa sana na vilevile urasimu huu siyo mbaya sana kwa sababu kwa kweli masuala ya silaha nayo ukilipua yana matatizo yake. Lakini tunaomba vikao vile vya kuangalia nani anastahili kupata silaha na nani hastahili vifanyike kwa mujibu wa ratiba na haraka zaidi,vikao vya wilaya, mkoa na makao makuu ya Polisi, ili wenye uwezo wa kununua na kumiliki silaha waweze kuzipata ili wenyewe watumie kujilinda na kulinda mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda pia nipendekeze kwamba kwa kuwa jirani zetu wako tu pale na hatuna namna ya kutengana nao ila kukaa nao tu vizuri, nataka nishauri kwamba kwa usalama wa nchi yetu Serikali ifike mahali ifikirie uwezekano wa kupata *detach* ya kudumu ya jeshi la Wananchi katika maeneo yale. Hili lingeweza kutusaidia sana kwa sababu suala la ulinzi na usalama ni jukumu la Serikali wakisaidiana na wananchi wenyewe. *Detach* hii kama itakubalika iwekwe kule kijiji cha Sali kwa sababu ni katikati ya vijiji ambavyo vinaathirika kama nilivyokuwa nimeelezea. Lakini jambo lingine ni kwamba vituo pia vya polisi viweze kuimarishwa kule mpakani kwa kuwaongezea askari, silaha na usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme, nimeshasema ni tatizo la barabara. Najua Mheshimiwa Rais, alipofanya ziara kule Ngorongoro aliwaahidi wananchi wa Ngorongoro kwamba barabara nayo inayotokea Mto wa Mbu kupitia Engaluka na kwenda mpaka Ngalesolo Loliondo itajengwa kwa kiwango cha lami.

Alitutamkia na mimi namshukuru sana, najua kwamba taratibu zinaendelea lakini akasema kwamba wakati hizo taratibu za lami zinaendelea hii barabara ya kutokea lango la Ngorongoro kupita Mbungani na hii barabara ya kutokea Engaleselo kwenda Loliondo ziimarishwe ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao zisiendelee kukwama wakati tunasubiri mipango ya Serikali ikamilike kwa ajili ya barabara ya lami. Naiomba sana Serikali barabara hizo kwa mujibu wa ahadi za Rais iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kuhusu suala la mawasiliano, simu za mikononi. Napenda niwapongeze watu wa *Vodacom* na *Celtel,* wameingia Loliondo hivi karibuni na kutufanyia kazi nzuri sana.

Nawapongeza sana na wameniambia kwamba ziko *site* zingine kama kule Samunge, Ngaleselo, Soisambu, Malambo na Inokonoka Sendu, Ihenduli, Kakesyo na Ndutu wamekusudia pia kuweka minara ili kuendelea kupanua kuifanya Wilaya ya Ngorongoro nayo iendelee kufahamika katika Tanzania na Ulimwengu wote. Nawapongeza sana na naomba watekeleze haya ambayo wametuahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya Mto wa Mbu kupitia Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia kwangu kule, ina fursa nyingi sana za uchumi.

Kule kuna Engaruka Luinsi, watalii watakwenda wataangalia, kule kuna Shimo la Mungu, kuna mlima Lengai, kuna *Engalesolo Water falls,* kuna *escarpment* ya *rift valley*, kuna *lake Natron,* kwa kweli ni eneo ambalo tukipata barabara ya uhakika, hiyo barabara itatuongezea mapato kutokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa kwenye kijiji cha Pinyinyi, ni *boarder* kabisa kilomita chache tu kutoka *boarder* ya Kenya. Kuna *lodge* wanaita *Shombole Lodge.*

Nilipokuwa nakaribia ile *Lodge* nikakuta kuna kibao kikubwa kimeandikwa *welcome to Shombole Lodge, Lake Natron drive day and night*. Na *lake Natron* lipo kwetu moja kwa moja. Ni sehemu ndogo sana iko Kenya na haina *flamingo* ambao hawa watalii wanakwenda kuwaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana wanaingia, wanawaangalia *flamingo* Kijiji cha Pinyinyi ambacho hakinufaiki na chochote katika utalii huo.

Hata wanatuibia ningeomba Wizara inayohusika pengine nitachangia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, waweke *gate* ya kuweza kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la umeme. Mheshimiwa Rais pia kwa tarehe hiyo alituahidi kutupatia umeme.

Lakini alisema wakati utaratibu wa umeme wa *hydro* tunaendelea kushughulikia aliiagiza *TANESCO* kwamba umeme wa *generator* upelekwe katika Wilaya ya

Ngorongoro. Nimeshafuatilia kwa Naibu Waziri amenipa matumaini na nategemea kwamba hili litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu naona muda umekwenda na mimi huwa sipendi kugongewa kengele, zipo sheria ambazo kwa kweli zina matatizo kwa tarafa ya Ngorongoro ambayo pia ni hifadhi.

Kuna Sheria ya Vijiji ya Mwaka 1975, kuna sheria *Local Government Authorities* ya mwaka 1982, kuna *Village Land Act,* na *Land Act,* (Sheria Namba 4 na 5) za Mwaka 1999 na kuna Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, sheria zote hizi zinakanganya. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana . (*Makofi*)

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda kutoa pole kwa watu wote wale ambao wamepata ajali iliyotokea Mbeya, Arusha na Singida, naomba Mwenyezi Mungu awape afya mapema na wale waliopoteza uhai wao naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitazungumzia hali ya usafiri na hali ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ukurasa wa 21 ametusaidia sana watu wa Jiji la Dar es Salaam kwa kutupa fedha ambayo itatengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba Jiji la Dar es Salaam ndiyo Jiji kuu sasa hivi nchini Tanzania na ndiyo Jiji ambalo lina magari mengi katika nchi hii ya Tanzania. Kwa kutoa tu pesa kwa ajili ya kutengeneza barabara za changarawe katika jiji la Dar es Salaam kwa sasa hivi kwa kweli haifai kutokana na msongamano mwingi sana ambao umejitokeza. Pamoja na utaratibu huu ambao umefanywa na ma-*traffic* sasa hivi umesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza msongamano lakini bado kuna tatizo zima ambalo watu wa Mkoa wa Dar es Salaam na wananchi wa Mkoa ule wanakutana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tunaijua vizuri, kuna njia ambazo Serikali inaweza ikazitengeneza ikapunguza kabisa msongamano pamoja na hizi alizozitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano barabara ya Uhuru barabara ambayo Viongozi wengi wa Serikali na Viongozi wengi wanaotoka nje ya nchi wanapita, inawatia aibu kubwa. Ina mashimo, kama si mashimo basi ni mahandaki. Lakini barabara ya Uhuru inaweza ikatengenezewa barabara nyingine ambayo inaweza kupita Lindi kwa kiwango cha lami ikatokea Buguruni Hosteli na kupunguza msongamano katika barabara ya Uhuru. *(Makofi)*

Vile vile kuna barabara ambayo inaweza kutengenezwa kutoka Bomani ikatokea Ilala Shamba na pia kutokea Gereji ikapunguza msongamano katika Barabara ya Uhuru. Vile vile ukitazama Kinondoni, kuna barabara ambayo inapitia Hospitali kupita Kijitonyama, kutokea Sayansi ikitengenezwa kwa kiwango cha lami, inapunguza msongamano na barabara nyingi tu ambazo zipo, zinaweza kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara inayohusika na masuala yote ya barabara za Mkoa wa Dar es Salaam basi ituchukue sisi watoto wa Dar es Salaam tusaidie kutoa mawazo yetu katika barabara ambazo zipo. Kuna Mitaa ya Dar es Salaam mpaka Mitaa inaitwa Punda. Lakini Wabunge hapa ukiwauliza Mitaa ya Punda unaijua? Hawaijui. Tutaisaidia Serikali katika suala hilo la kuondoa msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuiomba sana Serikali, iangalie sana barabara ambazo zina *traffic lights*. Sasa hivi kuna mtindo ambao umetokea katika Jiji la Dar es Salaam, madreva wanapita katika taa nyekundu. Hii ni hatari kubwa na inasababisha ajali nyingi sana. Tunaomba *traffic* sasa hivi pengine mtu anapita na *traffic* yupo pembeni, wachukue namba za magari kisha wawawajibishe madreva ambao wanafanya matokeo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuiomba Serikali hili ni jambo *special,* naomba kwa niaba ya wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ndiyo kiongozi wetu wa Serikali. Jiji la Dar es Salaam lisichukuliwe tu kwamba ndiyo la Dar es Salaam, alichukue kama jiji kuu la nchi hii ambalo linapata wageni wengi na watalii wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba afanye *special programme* ambayo itasaidia kujenga barabara za *frame over* za juu, magari yapite juu. Kwa mfano, katika ukurasa wake wa 21 kuna barabara ambayo itatoka Twiga kwenda Jangwani pale, inaweza ikatengenezwa barabara hizo za juu zikatoka Twiga kwenda Kinondoni na ikatoka Kariakoo vile vile Twiga kwenda Kigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba sasa hivi, wakati umefika wa kututengenezea barababara za kisasa. Pamoja na hayo jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni la afya. Jiji la Dar es Salaam lina watu wengi sana takriban watu milioni tatu mpaka nne na jiji la Dar es Salaam linategemea hospitali ya Mwananyamala, Kinondoni na Ilala pamoja na hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Tukubaliane kwamba mpaka sasa hivi bado suala zima la huduma katika hospitali hizi pamoja na kukarabatiwa tunashukuru, pamoja na kuongezwa tunashukuru. Lakini bado wagonjwa wanalala chini hadi leo. Tunazungumzia habari ya miaka 45 ya uhuru bado Watanzania tunawalaza chini katika hospitali ndogo ndogo za Wilaya. Tunaomba hospitali ambayo Mheshimiwa Waziri alisema kwamba tutajengewa hospitali ya Mkoa, basi hospitali hiyo ijengwe mapema sana ili kupunguza msongamano katika hospitali hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kupunguza uwezekano wa watu kuendelea kulala chini kwa muda mrefu. Pamoja na kuyasema haya, kuna tatizo kubwa la msingi katika Wizara ya Afya ambayo wafanyakazi, wahudumu na madaktari baadhi yao

wamepata vyeo zaidi ya mara tatu, lakini Serikali bado haijawaongezea mishahara. Hili suala kwa kweli tunaomba Serikali ilisimamie suala. Haya ni maombi rasmi yamekuja ili tuwasilishe, Serikali iangalie, wale ambao wamepata vyeo zaidi ya mara tatu au mara mbili lakini mishahara yao ni ile ile, kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni kuhusu Jimbo la Kigamboni. Jimbo la Kigamboni sasa hivi Serikali imetoa viwanja vingi sana katika Jimbo la Kigamboni na viwanja hivyo vitawasaidia wananchi katika kujenga makazi yao. Lakini naiomba Serikali, Kigamboni itakuwa ni sehemu ya kimataifa na ramani ya Kigamboni ukiiona, nafikiri haipo katika Afrika. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kitu kimoja, naomba Kigamboni iangaliwe katika masuala muhimu, kwanza zitengenezwe barabara ambazo zitasaidia wananchi kufika maeneo ambayo wanataka kujenga kwa urahisi na vile vile ipelekewe maji. Kwa muda mrefu Kigamboni maji ya mabomba imekuwa kama kitendawili. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kwa kuwa Serikali imeamua kwa dhati kabisa kupeleka wananchi kuishi huko watengeneze mabomba ya maji na vile vile wasogeze umeme, pamoja na daraja pamoja na kivuko. Tunashukuru kivuko Aprili tumeahidiwa kwamba kinakuja kipya ambacho kitasaidia wakazi wa Kigamboni. Lakini pamoja na hayo yote kutokana na viwanja vya miradi ya 20,000 vile tunahitaji mambo haya yasimamiwe na panuzi za barabara ziwe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la wazee. Tulikubaliana kwamba wazee watatibiwa bure katika nchi hii ambao wamefikia miaka 55 na kuendelea. Lakini mpaka leo ni kitendawili. Ni wazee wachache tu ambao ndiyo wanatapata huduma mpaka upitie kwenye Kata au kwenye Serikali ya Mitaa. Hivi kweli mzee wa miaka 70 akiumwa atoke nyumbani kwanza amtafute Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ampe hiyo barua ndiyo aende akapate huduma? Lakini Serikali ilisema hapa hapa Bungeni kwamba itatengeneza vitambulisho.

Sasa ndiyo nataka nipate kusikia wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama aseme kwamba wazee wangapi wameshapata hivyo vitambulisho au bado utaratibu ule ule unaendelea? Hata hivyo wazee hao hao wakienda hospitali wanadai kwamba wanaandikiwa dawa wakanunue. Sasa Waziri Mkuu atueleze ni maradhi gani ambayo wazee wanaweza kutibiwa, kwa vile wazee wana sukari, wana presha na madawa haya ni ghali sana. Sasa aeleze jamii hapa kwamba ni magonjwa yapi ambayo wazee wanahitaji wapate huduma katika hospitali za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, sasa nizungumzie suala zima la Mahakama. Kumekuwa na zogo kubwa na msongamano mkubwa katika Mahakama za Wilaya yetu ya Ilala. Unakumbuka hapa niliuliza swali la nyongeza, nikaambiwa nimezungumza sio mahali pake? Sasa leo huu ndiyo uwanja wangu. Sasa hivi Mahakama ya Wilaya ambayo ilikuwa zamani Samora, imehamishwa imeletwa katika Mahakama ya Kariakoo ambayo ndiyo ina mahabusu wanakaa ndani ya magari. Tunakuwa tunawatesa mahabusu kwa kuwaweka ndani ya magari kwa masaa yote,

wakati wao wanahukumiwa kabla ya hukumu kufika. Hili suala liangaliwe vizuri Jiji la Dar es Salaam lina watu wengi. Ziongezwe Mahakama ziwe nyingi ili ziwahudumie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa nazungumzia Halmashauri. Bunge hili sisi sote Wabunge tulioko hapa ni Madiwani katika Halmashauri, lakini ni jambo la kusikitisha na la aibu kabisa kuona kwamba huu ni mwaka wa pili baadhi ya Wabunge wa Viti Maalum bado hawashiriki katika Halmashauri pamoja na Rais kutia saini sheria ile pamoja na kupeleka Waraka ambao unawaelekeza kwamba watupokee tuingie katika Halmashauri, lakini bado kuna kitendawili. Kuna Madiwani wa Viti Maalum kwa Dar es Salaam hawaingii katika Halmashauri: Je, tutakwenda kutetea wapi wananchi wetu? Tutakuwa kila tukija hapa kwenye Bunge ndiyo tunatetea? Hii sio haki. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe tamko katika Bunge hili kwamba Wabunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Dar es Salaam sasa wanaruhusiwa kuingia katika Halmashauri na wale Wakuu wa Halmashauri ambao hawataki kusikia wakishamsikia *boss* wetu amesema, basi nafikiri Wabunge wote wa Viti Maalum tutatekeleza wajibu wetu kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kugongewa kengele, ila nina jambo moja nataka kulisema. Katika ukurasa wa sita, Waziri Mkuu alizungumzia hali ya kisiasa. Alizungumzia vizuri sana nchi hii amani na utulivu na kila kitu, lakini sio kweli. Siku za uchaguzi, Vyama vingine vya siasa vinapata taabu sana, watu wanapigwa hata katika uchaguzi mdogo tu wa Serikali ya Mtaa au Serikali ya Kijiji. Watu wanaadhiriwa, wanapigwa na haki yao hawapati. Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya Waziri Mkuu naomba demokrasia ifanyike, sasa iwe demokrasia ya kweli kama tunavyofanyiwa sisi Wabunge katika Bunge hili. Tunahitaji demokrasia hiyo ishuke mpaka kwenye Vijiji vyetu na Matawi yetu Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sipendi kugongewa kengele ya pili. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza naomba nianze kwa kutoa pole kwa wafiwa ndugu na jamaa wa Marehemu kwa msiba uliotupata Watanzania kwa kuondokewa Watanzania wenzetu wapatao 54 ndani ya kipindi cha siku 11. Nawapa pole na Mungu azilaze pema roho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kuzungumzia suala la elimu. Elimu ndiyo msingi mkuu wa maisha ya mwanadamu. Tunavyodhani ni kwamba huwezi kujenga nyumba ambayo itakuwa madhubuti bila ya kuwa na msingi madhubuti. Elimu ya msingi ndiyo msingi wa elimu kwa Mtanzania na mtu yeyote ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu iliyo bora ndiyo elimu ambayo itamkomboa Mtanzania. Elimu tunaithamini sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kitabu chake

hiki alichotoa ametoa takwimu na jinsi gani ambavyo watoto wa Kitanzania wanaandikishwa mashuleni ili kupata elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa wanafunzi hautathmini ubora wa elimu. Watoto wa Kitanzania tunahitaji tuwape elimu iliyo bora. Ni metegemeo yetu kwamba wanafunzi hao au vijana hao ndiyo watakaokuwa viongozi baada ya kuondoka sisi. Lazima tuwape elimu yenye thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa Kitanzania ambaye anaondoka nyumbani asubuhi, anakwenda shuleni kupata elimu, lakini anapofika barabarani anakwenda kusubiri daladala pengine inafika saa 4 .00 au saa 5.00 hajafika darasani. Mwanafunzi huyo anapofika darasani mwalimu hasikii Kiswahili chochote na mifano inaonekana katika televisheni, tunaonyeshwa kila siku jinsi mtoto wa Kitanzania anavyodhalilika anavyoingia darasani.

Hivyo ningembona Mheshimiwa Waziri Mkuu, Seikali basi iandae utaratibu wa kuwajali watoto wale angalau kuandaa utaratibu wa kuweka magari ambayo watoto wale wataweza kupata huduma za kuwafikisha shuleni kwa wakati hata kama ni kwa gharama nafuu, basi mtoto anaweza kuchangia hiyo nauli ili aweze kufika shuleni kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanapata shida sana. Wewe kama ni mzazi unapoingia kwenye daladala na ukamwona mtoto anavyosukumwa na mzazi mwenzako, usipande daladala ile, mbali kwamba anasukumwa na kondakta wa daladala, lakini hata mzazi wakati mwingine hajali kwa sababu pengine mtoto yule sio mtoto wake wa kumzaa yule. Kwa hiyo, anamsukuma asiingie kwenye gari. Mtoto yule anadhalilika. Kama wewe ni mzazi na unahisi kwamba una mtoto wako kama yule anakwenda shuleni ukakiona kile kitendo, basi wewe mzazi machozi yatakutoka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tungeandaa utaratibu wa kuweka magari ambayo wazazi au wanafunzi wale wachangie gharama fulani ili mwanafunzi anapotoka nyumbani awe na uhakika kwamba anakwenda kituo fulani anakwenda kupanda gari hili ili inifikishe shuleni. Nadhani ungekuwa utaratibu mzuri ambao ungewasaidia watoto wetu ili waweze kupata elimu iliyo bora kwa wakati unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana kuwa na idadi nzuri ya vijana ambao wamesomeshwa vizuri kuliko kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamepita tu shuleni. Sasa watoto wetu ni vizuri sana Mheshimiwa Masunga kaichangia sana hoja ya kwamba tuna haja ya kuweka mabweni shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabweni ni suala la msingi na la muhimu. Linamkomboa kijana, kwanza kijana anajifunza kutokana na maisha anayoishi na watu tofauti, anajifunza tabia tofauti, anajifunza kuweza kuishi popote na watu wa aina zote. Kwa hiyo, unaanza kumjenga mwanafunzi pale, kijana yule akikua, anakua katika mazingira mazuri. Baadaye kijana yule, atakuwa kijana nzuri sana ambaye tumemwandaa huku chini, kuliko mtoto yule kutoka akienda nyumbani akirudi hapati muda mzuri wa kujifunza, mtoto anapokuwepo nyumbani, wewe mzazi akirudi tayari umeshamtegemea. Kanunue chumvi, kama mwanamke kakune nazi, nenda kafue, nenda

kafanye hivi, kwa hiyo, muda wake unapotea, lakini mwanafunzi ukimweka pale kwenye bweni anapata masomo pale, anakwenda nyumbani wakati wa mapumziko tu ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili aliangalie kwa makini sana. Bado nipo hapo hapo kwenye suala la elimu. Mwalimu bora ndiye atakayetoa mwanafunzi bora. Kwa hiyo, tunapaswa kuwaandaa walimu wetu vizuri. Tunapaswa kuandaa mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba shule tunazozijenga tunazipatia walimu walio bora, wanaokidhi mahitaji ya shule ile na mwalimu ambaye ana muda mzuri wa kufundisha vizuri mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule tunazozijenga tuhakikishe kwamba tunajenga na nyumba za walimu. Ni muhimu sana kuweka nyumba za walimu, ni muhimu sana kumboresha mwalimu kwa mafao yake ili aweze kujali kazi yake. Mwalimu ambaye humtoshelezi kimahitaji hawezi kuithamini kazi yake. Mwalimu kama haithamini kazi yake, matunda hayatakuwa mazuri. Naomba tuliangalie kwa makini sana ili suala hili la kumfanya Mwalimu awe ni Mwalimu kweli ili tuweze kutoa matunda mazuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni wanafunzi au ni vijana ambao tunawaandaa kuja kushika madaraka katika nchi yetu. Kwa hiyo, Taifa lililo bora litajengwa na sisi ambao tuko sasa hivi ili tuweze kutoa matunda yaliyo bora na Taifa lilo bora liendelee kwa kutoa vijana wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika sehemu ya afya. Bado kunaonekana kuna matatizo ya akina mama kujifungulia majumbani. Tatizo ambalo linawasababishia akina mama wengi kupoteza maisha yao au kupoteza maisha ya watoto, bado kuna tatizo la baadhi ya mahospitali kuwatoza gharama akina mama wanapokwenda kujifungua. Ni tatizo sugu, ni tatizo ambalo linapaswa kupigiwa kelele sana na kufuatiliwa kwa makini sana ili kuhakikisha akina mama wanahudhuria kliniki na wanahudhuria hospitali wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi sana wana maisha duni sana. Wakati mwingine hata akina baba wanakuwa hawajali mama anapokuwa mjamzito kushughulika kwamba huyu sasa hivi ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba namwandaa kwa ajili ya kujifungua. Hamthamini, hamjali, anamtelekeza bila kujali ile afya yake ambayo pengine *source* ni Mwenyezi Mungu na Mtume na yeye. Kwa hiyo, mama yule kama baba hayuko pamoja naye na Serikali anapokwenda Hospitalini pia naye inakwenda kumtoza gharama ambayo pengine hana uwezo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tatizo sugu. Kwa hiyo naomba bado Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili aendelee kulipigia kelele kwamba akina mama hawa basi wasitozwe hizo gharama kutokana na hali zao na afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapo hapo kwenye suala la afya. Hospitali ya *Ocean Road* ni hospitali kubwa ambayo inashughulikia wagonjwa wa kansa. Tatizo la kansa limekuwa sugu katika nchi yetu. Kansa imetuandama, magonjwa mengi, watu

wengi wanateseka na matatizo haya, hospitali yetu ambayo tunayo ni moja tu, ambayo nasema kwamba haikidhi haja. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hospitali ile ahakikishe inajengwa siyo kukarabatiwa. Tuijenge upya, tuweke vifaa ambavyo vinahitaji na vinatosheleza kwa ajili ya kuwashughulikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kansa ni tatizo sugu sana. Lingine nije kwenye usalama wa raia. Raia wa Tanzania maisha yao yanasumbuliwa sana na suala la ujambazi. Ndani ya maeneo mengi sasa hivi kumeanzishwa polisi jamii. Polisi jamii inasaidia sana. Kuna baadhi ya mambo ambayo huwa yanataka kujitokeza lakini Polisi Jamii wanasaidia kwa kiasi fulani. Lakini Polisi Jamii ambaye ana kirungu, Polisi Jamii ambaye ana jiwe labda Polisi Jamii pengine hathubutu hata kutembea na kisu. Polisi Jamii kashirikishwa na askari mmoja tu ambaye hana silaha yoyote.

Kwa hiyo, linapotokea tatizo, hata yule askari ambaye ana mafunzo kamili, basi hawezi kupambana nalo. Kwa hiyo, tunaomba hawa Polisi Jamii wapewe *training* ya kutosha na pia yule askari ambaye anaongozana naye, basi awe na silaha panapotokea tatizo aweze kusaidiana nao wale. Lakini kumpeleka askari mikono mitupu wa Polisi Jamii akapambane na majambazi ni tatizo.

Wale majambazi wana silaha za kutosha, hawatoki kwenda kufanya ujambazi bila ya kuwa na silaha kamili. Ingawaje Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kitabu chake kumetolewa na taarifa kwamba kuna silaha ambazo zinamilikiwa kinyume cha sheria nyingi tu zimekamatwa, wamenyang’anywa lakini bado silaha nyingi zimo mikononi kinyume cha sheria. Naomba hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa usalama wa raia, narudi hapa hapa kwamba bado tunahitaji *training* ya kutosha kwa vijana wanawake ili waweze kutusaidia sisi wanawake wenzao. Askari wa kike na Mheshimiwa Waziri Mkuu nimeshamwambia ni kidogo sana. Tunahitaji mafunzo yatolewe zaidi au ajira zitolewe zaidi kwa vijana wa kike ili tupate askari wanawake waweze kufanya kazi kwa niaba ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa tunaelekea kwenye Muungano yaani Jumuiya ya Wanachama watano, wakiwemo jirani zetu. Jirani zetu tunawajua wana matatizo sana. Leo tunakwenda kujikaribisha na sisi kwenye matatizo. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuangalie sana hawa wenzetu ni jirani zetu, ni marafiki zetu, lakini ni watu ambao kidogo wana matatizo na siyo kidogo, labda niseme sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki raha ya kuwa wamoja ni watu ambao tunalingana kimila, tabia na silka na utamaduni. Tamaduni zetu ni tofauti na tabia zetu ni tofauti. Sisi Watanzania ni watu ambao tunaishi kwa amani na utulivu. Wenzetu ni watu ambao wana migogoro isiyokwisha ndani ya nchi yao. Sisi kama tunayo ni midogo midogo na matatizo ambayo tunayo, Mheshimiwa Rais kasimama kidete kuhakikisha kwamba matatizo yanaondoka.

Kwa hiyo, tuna matumaini makubwa kwamba hili litamalizika. Lakini je, jirani zetu ambao tunawakaribisha na sasa tunaelekea kwenye Shirikisho: Je, hili Mheshimiwa Waziri Mkuu utatuambiaje? Utatuhakikishiaje Watanzania usalama wetu na kujiunga na hawa wenzetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Jumuiya ya Afrika Mashariki, au kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki, sisi Jamhuri ya Muungano ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Zanzibar inaelekea kukosa nafasi mara mbili zaidi tunapoelekea huko. Je, nafasi ya Zanzibar iko wapi katika Shirikisho hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana na hasa kwa kuwakumbusha akina baba kuwalea akina mama vizuri hasa wanapokuwa wajawazito. Tunakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini pia nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake pamoja na Watendaji waliopo katika Ofisi yake bila ya kuwasahau Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao wanafanya nao kazi kwa ukaribu zaidi.

Pili, nami napenda kutoa rambi rambi zangu kwa wale wote ambao waliokuwa wamepata matatizo na wale waliondokewa na wapendwa wao nawapa pole Mwenyezi Mungu atawapa imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichangie, kwanza TAMISEMI. TAMISEMI nachangia kwa sababu watendaji ndiyo ambao wana dhamana kubwa. Lakini utaona sasa hivi kuna vyeti ambavyo ni vichafu, kuna vyeti safi, vyeti vya kati. Vyeti hivi vinatolewa kwa Halmashauri mbalimbali kutokana na mahesabu yao wanavyoyapanga. Wale wanapata cheti kichafu hawapati pesa za maendeleo. Sasa hapa mimi najiuliza sana kama hawapati pesa za maendeleo pesa hizi wanawanyima watendaji, au pesa hizi wanawanyima wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama watendaji ndiyo waandaaji na watendaji ndiyo wasimamizi, mnapowanyima wananchi pesa za maendeleo na mnahitaji wawe na maendeleo, maendeleo haya hayataweza kupatikana. Lakini bado tatizo likionekana kwa mtendaji, mtendaji yule anatolewa kituo kimoja na kupelekwa kituo kingine. Bado zile zilizopotea ukichanganya na zile ambazo anazopewa za uhamisho, basi inakuwa ni raha tu. Kwa sababu yeye anakuwa hana tatizo anapata pesa za uhamisho na nyingine zimepotea na anakwenda kwenye kituo kingine.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tulizingatie suala hili la watendaji wenye sifa ndio waweze kuajiriwa kwenye Halmashauri mbalimbali na tuweze kuangalia kwa mfano Halmshauri ya Tabora ilifikisha karibu miaka miwili hawapati pesa za maendeleo, lakini watu wanaweza wakasema Tabora yoyote lakini watapataje maendeleo wakati kuna baadhi ya pesa wao hawazipati kwenye Halmashauri zao. Kwa hiyo, mimi nilikuwa

naomba, ni kweli pesa hizi ni za wafadhili na wafadhili wao wameweka utaratibu huu na kama wameweka utaratibu na watendaji ni wa kwetu sisi wao walikuwa na maana ya kutuambia sisi tuwadhibiti watendaji wetu ndiyo maana yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa na imani ataweza kulizingatia ingawa alishawaita na kukaa na kuongea nao, lakini juzi mimi nilishiriki kwenye Kamati ya *LAAC* na nimeliona mambo jinsi yanavyokwenda. Nilikuwa naomba sana pesa za maendeleo kwa wananchi ziweze kuzingatiwa, watendaji waweze kuandika mahesabu vizuri ili waweze kupelekewa pesa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Zahanati, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati yuko katika utaratibu wa kueleza tuanzishe zahanati kwenye kila kijiji au Wilaya lakini aelewe kuwa ziko Wilaya ambazo tayari zimeshajenga zahanati kwa kushirikiana na nguvu za wananchi. Mfano Tabora tuna miaka sita zahanati Wilaya ya Urambo zimeshajengwa na zipo lakini mle sasa hivi mchwa wanakula zile mbao na hakuna watendaji na wala hazijafunguliwa. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo inayowasababisha wananchi waweze kuvunjika moyo wa kuleta maendeleo au kuchangia na wao pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mojawapo ambayo tukubali tunapoanzisha jambo tulianzishe sio kwa mlipuko, tulianzishe tukiwa tumeshajiandaa. Suala ardhi mimi naliongelea kwa uchungu sana. Bunge lililopita katika Wizara ya Ardhi, nyumba zile za Serikali zilipouziwa wale Mawaziri waliokuwa wakikaa kwenye nyumba zile, wote walipewa hati zao. Lakini wale wananchi walionunua zile nyumba za *National Housing,* mpaka leo ninavyosema bado hawajapewa hati zao, lakini Waziri alipokuwa akinijibu hapa wakati nimeshika vifungu vya Wizara yake akaniambia ninatoa mwezi mmoja watakuwa wameshapata hati zao wote. Lakini sasa nashangaa mpaka leo ni mwaka mmoja umefika, kauli hizi tunazozitoa humu ndani, tuweze kuzizingatia na kuona kuwa wananchi wanazisikia na hati ni haki yao.

Lakini bado wanasema kuna mwananchi mmoja aliuliza kwenye *TV* wakati Waziri anahojiwa akasema, ukiona wanakucheleweshea wapeleke Mahakamani. Lakini mimi ushauri wangu kwa uchungu wa kodi ya wananchi, nasema mimi nitaendelea kujitahidi kuwaombea waweze kupata hati zao wasiende Mahakamani. Wakienda Mahakamani atakayepata hasara ni Serikali, sio mtu.

Mtu ana uwezo wa kusema nenda Mahakamani kwa sababu anajua hana fungu lake ambalo atalitoa katika mfuko wake, ni fungu la wananchi na kodi ya wananchi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba wananchi hawa waweze kupewa hati zao kadri iwezekanavyo kwa sababu ni haki yao wanaweza wakakopa sehemu yoyote, anaweza akapoteza maisha yake hata watoto wake wanashindwa kwenda kutafuta hati zao. Kwa hiyo, lazima tukubali kuangalia haki za binadamu na wao wana haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu ni suala ambalo kwa mimi mwenyewe na Wabunge wa Tabora tuna nafasi kubwa ya kuweza kuisemea *TRC.* Tunaishukuru Serikali kuweza kupata mwekezaji na pia kuingia katika asilimia 49,

wanazo, na wawekezaji wakiwa na asilimia 51. Hii inatia moyo na inaleta faraja. Lakini bado Mheshimiwa Kaboyonga aliuliza swali, katika swali lake mimi ni bahati nzuri namshukuru Mheshimiwa Spika alinipa swali la nyongeza. Nilipouliza swali la nyongeza kwanini treni limeanzia hapa na mwezi wa sita tuliambiwa kuwa treni zitakwenda moja kwa moja kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza? Akasema, tatizo kubwa ni mwekezaji.

Lakini pia ninakumbuka mwezi wa sita kama huu tuliambiwa tatizo sio mwekezaji, tatizo ni reli hapa katikati zimesumbua. Sasa juzi nilipojibiwa vile nikasema kumbe tatizo lilikuwa ni reli sio mwekezaji. Kwa hiyo, tumekubali kufanya Dodoma ni Dubai kusudi wale wananchi wahangaike kuja mpaka Dodoma, wakishafika Dodoma waanze kugawanyika wenye kwenda huku kila mtu sehemu yake. Maana watu tumeshafika Dubai tunaangalia pale watu wanavyogawanyika, sasa tunaichukua Dodoma tena inakuwa Dubai. Lakini bado tukubali kuwa tunawatesa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, treni inaharibika, wananchi wanalala hapa, wengine wanakuwa na watoto wadogo wanalala na kuna baridi, wakati huo kila mmoja anaelewa, lakini mwingine anakuwa na pesa ndogo, anasafiri kwa utaratibu gani? Kwa hiyo, bado tunawatesa watu, tukubali kuangalia taratibu tunapozipanga tuwafikirie kwanza wananchi wanaathirika kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, hii barabara nisipoisemea wale wanawake walionichagua kule wala hawawezi kunielewa. Nimechanguliwa na wanawake wa *UWT* Mkoa wa Tabora, sina budi kwa kweli kulisemea. Lakini nilimwomba Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote wa Tabora tukimaliza Bunge wala asiende na treni, sisi na yeye tufanye msafara mmoja wa kupita barabara hii mpaka Tabora na akifika pale Tabora afanye mkutano wa hadhara kuwaeleze mikakati kabambe ambayo imeandaliwa na Serikali kwa ajili ya barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaelewa kuwa mikakati kabambe ipo ambayo imeandaliwa na ni mizuri, lakini wananchi tukiwaambia bado hawaelewi. Juzi Mheshimiwa Saidi amesafiri kwenye basi, wanamwambia yaani umeamua sasa kupanda basi kusudi kuja kuhakikisha utaratibu huo barabara hii haiendelei kutengenezwa? Kwa hiyo, alijikuta watu wote wanamlaumu yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Wabunge wa Tabora tunasema, sisi hatuwezi kuilaumu sana Serikali, Serikali Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aondoke sisi tupite barabara hii twende mpaka Tabora, tena sisi tutakuwa tunam-*escort* twende afanye Mkutano wa Hadhara. Moja, itajenga heshima ya kuona kuwa Serikali imewasikia na wao wameieleza Serikali tatizo gani ambalo linaendelea au mikakati gani mizuri ambayo imeandaliwa na Serikali kuweza kutengeneza barabara hii. Kwa sababu ni wasikivu na wanaielewa na ndiyo maana wakaichagua Serikali kwa kura nyingi zaidi na wao watawasikia na watakuwa wavumilivu katika maandalizi ya mikakati kabambe hiyo ambayo inayoandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi hivi itakuwa ni mbaya, shida sana. Kibaya zaidi ambacho kinatupa shida, sisi kwetu tuna Mawaziri, tuna Spika ambaye anatoka

Tabora, wao wanasema yaani tuna Spika, bado tuna Mawaziri lakini barabara wala haitegemei.

Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ambayo na sisi wengine inatutia uchungu, ndiyo maana ya kumwomba Waziri aende kule akafanye mkutano na wananchi watamsikiliza vizuri sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sema sema!

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo, mimi nilikuwa nasema tukubali kuwa mikopo tumeitoa lakini bado tulikuwa hatujajiandaa wala benki zilikuwa hazijajiandaa. Tunasema kuhusu *SACCOS,* hatujachukua muda mrefu pesa zimeshakwenda benki wale wananchi, hata hizo *SACCOS* hawajaanza kuziunda, ndio kwanza tunakwenda kuwaambia anzisheni *SACCOS* pesa inaingia Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfanyabiashara yeyote anaangalia ile siku ambayo ile fedha imeingia na inaanza kuzunguka muda sio mrefu. Kwa hiyo, huu muda hawa watu wanajiandaa kuanzish *SACCOS,* vikundi waanze kuelekezwa sijui *SACCOS* zikozeje, hela tayari zimekwenda, zimezungumza na faida imeshapatikana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu sasa hivi wanapata shida ya hizi *SACCOS* na wanajikusanya kwa kipato chao kidogo wanapata hizo pesa, wakienda kutokana na masharti wanaambiwa bado hamjafikia malengo na kama bado hamjafikia malengo pesa iko benki inazunguka na kama pesa inazunguka uelewe kuwa huyu mwananchi mpaka aje apate mkopo anakuwa ameshakata tamaa. Wengine tu juzi nyumbani, mimi nikiwa Tabora wananifuata wanasema nyinyi ndio mnaokopa na nyinyi mnaozitumia, lakini mnatumia vyombo tu hivi bali kuweza kujitangaza kuwa mikopo ipo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inabidi ukae nao uanze kuwaeleza mpaka wakuelewe au wakati mwingine unamwambia panda kwenye gari twendeni benki. Kwa hiyo, mnafika benki unamwambia Meneja, samahani naomba uanze kuwapa elimu. Kwa hiyo, wanaanza kupewa elimu. Mimi nilikuwa naona sijui utumike utaratibu gani au hizo pesa nyingine za kuongeza kwanza zisipelekwe benki mpaka wananchi waelewe utaratibu huu ambao uliokuwepo, au waelewe kwanza namna ya *SACCOS* au utaratibu uweze kubadilishwa ukae katika hali nzuri mwananchi ajue kuwa mimi ninakwenda kukopa benki, nakwenda kwa dhamana fulani, ndio kama hizi hati nilizosema. Aende na hati yake akachukue mkopo atapewa, kuliko kutegemea huu wa *SACCOS* ambao bado unazidi kuzungusha na unatuletea shida sana kwenye Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Madiwani, ni kweli tunasema, lakini hicho kipengele cha kusema kama itawezekana kwenye Halmashauri, zipo Halmashauri nyingine kuna uwezekano lakini watendaji tu wanakwambia uwezekano huu haupo, lakini bado waambiwe wapeleke utaratibu ule ulioletwa wapeleke kwa Madiwani kwenye *full council* waweze kukubali au kukataa. Lakini bado wengine hata kwa Madiwani

hawajapeleka, Halmashauri yetu ya Tabora wamepeleka na tumekubali, lakini bado hata mimi nilikuwa nasema bado ni ndogo, waweze kufikiriwa kuongezwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea kuhusu suala la kuweza kukopeshwa vyombo vya usafiri, Madiwani na wao wana hizo Sh. 30,000/= au kama wakiongezwa zitawezekana kufikia Sh. 60,000/=. Ndio maana nasema bora zifikie Sh. 100,000/=, lakini kwenye ile ile pesa yake ambayo anaipata na posho yake, Diwani ana uwezo wa kukopa pikipiki na hata mtendaji ana uwezo wa kukopa pikipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Serikali iandae utaratibu wa kuwawezesha kukopa pikipiki. Mwisho ya yote, hata kiinua mgongo chake anakatwa zile pesa kama zitakuwa hazijafikia. Kwa sababu tuangalie sehemu ambazo wanafanyia kazi, ni sehemu kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukubali na wao kusaidiwa angalau waweze kupata pikipiki pamoja na Watendaji kwa sababu Watendaji wa Kata na Madiwani wote wanafanyakazi sehemu moja, basi tuweze kuwafikiria kwa vitendea kazi vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono, lakini kusema kuhusu suala la hati zile ziweze kupatikana, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nami nianze kwa kutoa mkono wa rambirambi kwa Marehemu wetu wote waliopoteza maisha katika ajali zile tatu za Mbeya, Singida na Arusha, Mwenyezi Mungu awepe raha ya milele. Amina!

Lakini pili napenda niwatakie afya njema wagonjwa wetu, Wabunge wenzetu, wa kwanza nimtakie kupona haraka sana Mbunge mwenzangu wa Mbinga Mashariki, Naibu Waziri wa Mipango - Mheshimiwa Gaudence Kayombo ili arudi tena katika Bunge hili. Nimtakie tena kupona haraka Mheshimiwa Amina Chifupa na mwenzake Mheshimiwa Mwalyosi - Mbunge wa Ludewa waweze kurudi vizuri katika Bunge hili.

Sasa na mimi pia nipongeze hotuba nzuri ya Waziri Mkuu ambayo imeelezwa kwa kina na kwa kweli inatekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kikamilifu kabisa. Labda ningetoa ombi tu kwamba nilikuwa naomba kwa Wabunge hasa Majimbo toka CCM mpaka Wapinzani nilikuwa nasema ni vizuri tukisimama hapa kwa sababu Serikali imeshatoa mwelekeo wake ilishatoa ilichofanya huko nyuma na sisi Wabunge tuweze kusema huko kwenye Majimbo yetu Serikali ya CCM imefanya nini ili wananchi wa Tanzania waweze kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema, kwa kweli yako mambo ambayo mwaka jana nimeyalalamikia hapa, lakini kwa dhati ya moyo wangu napenda kuishukuru Serikali ya CCM hasa awamu hii ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu, suala la umeme Mji wa Mbiga, awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu nataka niwaambie kwamba mwezi ujao umeme unawashwa Mbiga kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumehangaika sana na zao la kahawa mpaka mwaka jana tulikuwa tunapata kilo moja Sh. 400/= lakini kwa nguvu ya Serikali yetu na upeo wa Halmashauri zetu, leo wananchi wa Mbinga tunapata pesa kilo moja Sh. 2,000/=. *(Makofi)*

Lingine ni mawasiliano, nimshukuru sana Mheshimiwa Maua Daftari, mwaka jana nimelalamika kweli Jimbo langu halina mawasiliano ya simu hata moja. Lakini leo hii kuna minara 18 katika Jimbo langu tu ya *CELTEL, VODACOM,* na *TIGO*, na hii yote ni kasi mpya, nguvu mpya ya Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa nimelalamika pia mwaka jana kwamba ziwa letu Nyasa wavuvi ni maskini hawana uwezo wa kujiendeleza, hawajui uvuvi wa kisasa. Nishukuru sana Wizara ya Maliasili na Utalii kumtuma Naibu Waziri Mama Zaberi Mhita, nasema zimefanyika kwa ukamilifu na wananchi wameona kasi mpya, wamepata semina na sasa uvuvi unakwenda bambam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana pia nilikuwa nimelalamika, nimekuja kusema kwamba hospitali, hasa Zahanati zetu za mipakani kutoka mpakani mpaka Makao Makuu ya Wilaya ni karibu kilomita 160 hakuna usafiri wa akina mama wanajifungulia njiani, watu wanakufa, nikaomba hapa *ambulance* kwa nguvu mpya, kasi mpya, nikushukuru Waziri Mkuu kupitia Serikali za Mitaa TAMISEMI, magari matatu *ambulance* tumepata ahsante sana. Hiyo ndiyo kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Lakini pia niishukuru Serikali barabara ya kutoka Mtwara, Masasi, Tunduru, Songea Mbabay ilikuwa ni kitendawili, lakini sasa wananchi wanajua kabisa kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha barabara ile inaanza kutengenezwa na kwa kweli wanategemea watafanikiwa na mazao yetu yatasafirishwa na sasa tunaweza kutoka Dar es Salaam mpaka Capetown kwa lami, hizo ni juhudi za chama cha Mapinduzi nashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini yako mambo ambayo pengine niliyasema wakati ule na bado naendelea kuwepo mpaka sasa. Sasa haya ndiyo maombi tu kuhusu uwanja wa ndege wa Songea. Katika viwanja vya ndege vya Tanzania, Songea ni moja ya viwanja vizuri sana, kwa sababu ni kiwanja cha lami kuanzia mwanzo mpaka mwisho, lakini ndege hazitui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege zinakwenda Mtwara zinarudi, labda nipake maelezo kupitia Wizara ya Miundombinu, kuna nini? Hatuna fedha, tumesema kahawa sasa ni Sh. 2,000/= tuna pesa, tuna mahindi, tuna samaki, kwanini ndege haziendi Songea? Wananchi wanauliza, pesa wanashindwa kutumia toka Songea, kutoka Mbambabay mpaka Dar es Salaam ni kilomita 1200 sasa anataka atumie pesa yake kwa ndege akifika Songea apange ndege aje Dar es Salaam aende Mwanza, wapi ndege. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Miundombinu itusaidie ndege. *(Makofi)*

Lipo tatizo la mpaka wetu wa Tanzania. Mwaka jana nilisema kwamba jamani liko tatizo wenzetu wanadai kwamba mpaka wao ni kando kando ya Ziwa Nyasa, kwa

maana hata mimi Mbunge ni mtu wao, yaani ni Mbunge niko huku lakini ni Mmalawi, ndicho wanachodai, ndio msingi wa vita ile ya mwaka 1964 na kuthibitisha hilo wenzetu sasa wanavua mpaka kando kando ya ziwa letu kando kando kabisa wanafika na boti, wenzetu uvuvi uko mbali kidogo kuliko sisi. Kwa hiyo, wanakuja na boti, wanakuja na meli wanavua samaki wanafika mpaka kwetu na ukiwauliza wanakwambia huu ndiyo mpaka wetu, lakini kwa sababu ulinzi kule kwetu hakuna.

Kuanzia *Itungi port* mpaka unakwenda Chiwindi hakuna ulinzi kamili wa mipaka. Kwa hiyo, tunaomba kupitia ofisi hii ya Waziri Mkuu tupatiwe hata *detachments* za Jeshi hata *Feed Force, FFU* ama za ulinzi wowote ule ambao utasaidia ulinzi ambao na wananchi wakawa wanaishi kwa amani na raha. Lakini sasa hivi utakuta watu wetu wakivuka kidogo tu katikati ya ziwa wanakamatwa na Malawi na meli za Malawi, lakini wao wakija huku wanatamba tu. Kwa hiyo, jambo litiliwe maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kivuko kati ya Jimbo la Mbinga Magharibi na Jimbo la Peramiho. Wananchi wa kule usafiri wao ni duni kabisa, kuelekea Mikulu ni usafiri duni kabisa, wanatumia magamba ya miti kutengeneza mitumbwi ili waweze kuvuka. Sasa mfikirie, wakati mvua zinanyesha, mto umejaa, mama mjamzito anatarajia kujifungua anakwenda kwa mtumbwi wa magamba ya miti!

Sasa mimi naomba nipendekeze kwamba Serikali juzi hapa wakati anajibu swali Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alisema kuna kivuko kimezama mto Luhuhu, lakini kuna kivuko kipya kimeletwa mto Luhuhu. Ushauri wangu ni kwamba kile kilichozama kiopolewe na kikishaopolewa kipeleke mitomoni kifungwe ili wananchi wale waondokane na adha hii, maana ni wananchi wa Jimbo hilo hilo, wale walioletewa kivuko kipya, ni wananchi wa Jimbo na wale ambao wanavuka kwa magamba ya miti ni wananchi wa Jimbo lile. Kwa hiyo, tunaomba kivuko kiopolewe na kiende kule kikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Bandari ya *Bambabay.* Mwaka jana tulipiga kelele Serikali ikatenga shilingi milioni 100, lakini tumefuatilia shilingi milioni 100 hatujaziona, bandari haijatengenezwa, bajeti ya mwaka huu tumeletewa shilingi milioni 50. Sasa unatoka kwenye mia moja unarudi 50, mwaka itakuwa 25, mwaka mwingine sifuri, mwaka mwingine Mtwara *Corridor* imekufa. Kwa hiyo, naomba sana kama tuko *serious* na tuko *serious* kwa kweli, najua kazi ni kubwa, nchi ni kubwa uwezo ni mdogo, lakini keki hii ndogo tugawane na bandari ya *Bambabay* iweze kupewa pesa za kujenga bandari ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mchango mwingi lakini naipongeza Serikali yetu kwa kutusaidia yale tuliyoyaomba na sasa hivi Mbinga tunakwenda mbele, inshallah mwaka haya niliyosema yatakuwa yametatuliwa na awamu ya nne na idumu. Naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Capt. Komba na hasa kwa kuzingatia ujirani mwema kati ya Mwenyekiti anayeongoza kikao saa hizi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya hotuba nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa, napenda kutoa pole kwa ndugu yetu Peter Mtagulwa pamoja na waliofiwa kwa ajali mbalimbali za basi wiki hii iliyopita, Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Solwa, nasema niko hapa kuongea kwa yale waliyonituma. Mimi naanza na barabara. Kwanza, niipongeze Serikali kwa juhudi zake zote za kuona kwamba barabara nchini zinaweza kupitika vizuri lakini hasa ukizingatia Mkoa wa Shinyanga na Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongolea kwa mfano hai wa mwaka 2006 katika fedha tulizopata, ukipata barabara ya Pandakichiza na 'B' ambayo ilitakiwa tupate shilingi milioni 175 tulipata milioni 17.7. Ukitazama barabara ya Dudia - Solwa yenye urefu wa kilometa 54 pamoja na *emergence,* fedha za *emergence* kwa ajili ya ukarabati kutokana na mvua kubwa ile iliyonyesha, naishukuru sana ile mvua kwa sababu tuliongezewa fedha hapo angalau tumeweza kupata shilingi milioni 96, lakini mahitaji hasa ni shilingi milioni 300. Ukitazama barabara ya Ishandibula Ndimenya ina urefu wa kilometa 42, tumepata shilingi milioni 20 tu badala ya shilingi milioni 160. Katika barabara hizi za Wilaya, tuna barabara sita katika Jimbo la Solwa ikiwepo Solwa Mwakitolio kilometa 35 Mwawaze Selamagazi kilomita 35 na Mshipe ya Bukande kilometa 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema hapa ni kwamba ardhi ya Jimbo la Solwa ni mbuga kweli kweli kwa maana ya kwamba fedha hizi unazotupa kwanza tunaishukuru Serikali inafanya juhudi ni kwa nia njema tu ya kuondoa tatizo la barabara. Lakini kwa Mkoa wa Shinyanga na Jimbo la Solwa hizi fedha hazitoshi kabisa.

Napenda kusisitiza kwamba katika barabara ya Dubia - Solwa tumepata shilingi milioni 96, imetengenezwa kutoka Kata ya Dubia mpaka ya Bukande - Paliyamigati shilingi milioni 96. Makaravati zaidi ya 20 kilomita 25, makaravati zaidi ya 20 ardhi ni mbuga. Yaani hapa ninachojaribu kusema ni kwamba, Serikali izingatie kuona kwamba ninachoongea hapa ni kwamba tuzingatiwe kwa tatizo la ardhi, ni mbuga, tuongozewe fedha angalau basi kwa asilimia 60 badala ya asilimia 100. *(Makofi)*

Nilipokuwa katika ziara yangu kule, wananchi wengi sana walikuwa wanalalamika na barabara, wengine bei ya mazao, wengine ni nini. Lakini huwezi kuongelea masuala yoyote katika maendeleo zaidi ya barabara, ndiyo maana mimi nimeanza barabara kwanza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, mwaka jana pale Samuye yalitokea mafuriko na tulikuwa na ndege moja na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Marehemu Mheshimiwa Akukweti. Tulifika pale Masengo lakini Mheshimiwa Rais kwa nia njema na huruma ya wananchi wakataka kwenda kuona

wananchi pale Ikonda jinsi walivyoathirika, tukaamua kuondoka. Lakini hatukuondoka hata dakika mbili tu ile barabara yeye iliturudisha kule tulikotoka na Mheshimiwa Rais akasema, basi turudi.

Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda naye ni shahidi kwa haya ninayoongea kwamba barabara za Jimbo la Solwa na Mkoa wa Shinyanga ni mbuga, tunaomba fedha nyingi za kutosha tuzingatiwe kwa hilo, kinyume na hapo yote haya tutakayokuwa tunayaongelea lakini mwisho uchumi, mazao, bei chini na kadhalika yanasababishwa na barabara tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine, hii ya *Old Shinyanga – Sarawe* ni barabara kubwa mno na ni barabara ya *TANROADS.* Nashukuru sana Serikali inaifanyia kazi vizuri sana. Lakini nipende tu kusema, vilevile na Serikali ijue kwamba katika huu mradi wa maji wa Ziwa Victoria kuja Shinyanga, malori makubwa na mazito yalipita pale na yaliharibu sana ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu mno katika kuunganisha Mkoa wa Shinyanga na Mwanza kupitia biashara ya vijijini na wakulima wa vijijini kati ya Jimbo la Solwa na Jimbo la Misungwi Mkoa wa Shinyanga, imeharibika sana. Ningeomba Serikali ifikirie mara mbili. Ninachotaka kusema na ninachoomba hasa hapa Serikali ituongezee kwa kuzingatia ardhi yetu ni mbuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ananisikiliza vizuri sana, amewahi kuishi Shinyanga, anauelewa sana Mkoa wa Shinyanga ulivyo na ombi langu sasa kama nilivyoomba hapo awali.

Ombi la pili ni hii barabara ya Didiya – Solwa, ni barabara kubwa mno, ipo nje ya uwezo wa Halmashauri na kuna barabara nyingine ya Imenya kupitia Usule – Mawale – Shinyabuland, ni kubwa mno iko nje ya uwezo wa Halmashauri. Kwa hiyo, ningeiomba Wizara izichukue hizi barabara isipandishe hadhi kuwa barabara za Mkoa kupunguza mzigo kwenye Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitafurahi sana kama maombi yangu haya yatasikilizwa na kwa kweli ni kwa muda mrefu sana matatizo haya ya barabara katika Jimbo la Solwa yamekuwepo. Kuna Methali moja inayosema Mficha maradhi hufichuliwa na kifo. Sasa mimi hapa naomba kuyaongea haya na nifichue maradhi ili tupate tiba sasa ya barabara zetu katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie sasa kwenye shule zetu za sekondari. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi kubwa mno tena sana kutoka sekondari 78 mpaka 294. Natoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Solwa, kufikia mwezi wa Nane tutakuwa na shule 27 za sekondari lakini vilevile naupongeza Mpango wa *MMES,* fedha zote zilizotoka mwaka jana zimefanya kazi kama zilivyokusudiwa na mwaka huu

asilimia 18 ya bajeti inalenga kwenye Sekondari. Naipongeza sana Serikali kwa kazi hii kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Ni kwa sababu sasa hivi tunakwenda kwenye hatua ya ujenzi wa Zanahati na Vituo vya Afya. Sasa nilipokuwa kwenye ziara yangu nilipambana na maswali, lakini nikasema hapana hili nitalipeleka Bungeni. Waliniambia sisi tunafurahia sana maendeleo na tuko tayari kuchanga na kuendelea na ujenzi, lakini sasa tunafanya yote kwa pamoja kwa maana ujenzi wa Sekondari uwe ujenzi endelevu na wakati huo huo uendelee na ujenzi wa Zahanati? Nikamwambia hapana, mimi...

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ooh! naona *time* zinakwenda haraka sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema mimi nalipeleka hili lakini naomba kwamba ujenzi wa Zahanati na kwa sababu Serikali imetoa kipaumbele sana iuchukue ujenzi wa sekondari moja kwa moja katika mpango huu wa *MMES* kwa sababu sasa hivi katika Mkoa wa Shinyanga Jimbo la Solwa sekondari zilipofikia ni pazuri. Kwa hiyo, ujenzi endelevu kwa maana ya Serikali kama italichukua itakuwa ni mwaka hadi mwaka kupitia mpango wa *MMES* ili sasa tutoe nafasi kwa wananchi katika michango yao na tujikite vizuri hasa katika ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ombi hilo au naomba tu nipate mwongozo wa Serikali kuhusu haya yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kidogo kwenye kilimo. Katika Jimbo la Solwa tuna miradi ya umwagiliaji. Katika Kata ya Tinde kuna miradi ya Nsalala, Itwangi, Midabutini na Nduguti na sehemu hii ya Masengwa hata Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kutembelea. Lakini miradi hii imekaa kama mfereji tu, yaani mvua ikikatika yenyewe haina kazi, lakini mvua ikinyesha ndiyo inanyoosha maji kwenda kwenye mashamba.

Kwa hiyo, kinachohitajika hapa ni kupata mabwawa yatakayovuna yale maji ili yaweze kufanya kazi vizuri kwa maana ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tarehe 23 Juni, 2006 niliwahi kumwandikia barua Waziri wakati huo akiwa Mheshimiwa Joseph James Mungai kuhusu suala zima la maeneo muhimu ya umwagiliaji katika Jimbo la Solwa. Katika Jimbo la Solwa nilimweleza kwamba kuna maeneo mazuri sana katika Mbuga ya Solwa, inayoelekea na Mwakituryo ambayo inakwenda mpaka kule Bukene – Ilola hadi Didiya eneo ni kubwa lina urefu wa kilomita zaidi ya 45. Ikinyesha mvua eneo lile halipitiki. Nikaiomba *Irrigation Scheme* kanda ya Ziwa pale wakaja wakazungukia wakasema hivi tumeshaandika barua ndugu yangu, huyu Karumuna katika Kanda ya Ziwa kule akasema nimeshaandika barua Wizarani na tumeomba fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kwamba hiyo barua na maombi hayo yamefanyiwa kazi? Vilevile katika Kata ya Samwea kuna mto fulani unaitwa Mto Manonga, ni mkubwa kwelikweli na ndiyo uliosababisha mafuriko yote haya yatokee.

Ningependa vilevile Wizara ya Kilimo ichukulie hii kuona kwamba pale pia panafaa mno katika kilimo cha umwagiliaji. Ningeiomba sana Serikali ifanyie kazi maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mifuko ya Pembejeo, wananchi wa Jimbo la Solwa wengi mno wanataka trekta. Mimi nilishawahi kukutana na Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dr. Christopher Kajoro Chiza, lakini masharti yale yale ya kibenki na mambo mengi tu kama dhamana, mimi nasema kwa mtindo huu wale walengwa hawawezi wakafaidika. Hasa ninachoomba ni trekta kwa sababu kilio kikubwa cha wananchi wa Solwa na wakulima wakubwa wanataka mikopo wapate matrekta.

Sasa naiomba Serikali au nitoe ushauri kwamba ihusishe Halmashauri kama mkulima anataka mkopo adhaminiwe na Halmashauri trekta hili libaki kwa jina la Halmashauri mpaka pale atakapomaliza deni na jina linahamishwa kwa jina la yule aliyekopa labda hiyo ndiyo itakuwa njia fupi kwa ajili ya kuwawezesha watakaotaka mikopo ya trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na hapo, mfuko wa pembejeo hautalenga na hautaleta tija ya kilimo katika jamii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona *time* zinakwenda narukaruka *point* lakini nataka niongelee mifugo. Kwanza namsifu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa sana anayoifanya karibu sana na Wizara hii ya mifugo na nitakayoongea hapa yeye anaelewa vizuri sana kwani ni mfugaji mzuri mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa iliyofanya kwa kutafuta mwekezaji ambaye tumepata sasa hivi kiwanda cha nyama cha Shinyanga kitafanya kazi. Sasa soko la mifugo yetu litapatikana na uzuri wa hiyo ni kwamba bei itakuwa nzuri, ng'ombe watauzwa kwa kilo badala ya kichwa na itapunguza usumbufu wa ng'ombe kwenda Dar es Salaam ambapo ng'ombe karibu asilimia 25 wanakwenda Dar es Salaam. Hili ndiyo soko la uhakika, tukishakuwa na viwanda katika Mkoa wa Shinyanga ndiyo soko.

Kwa maana hiyo, Mkoa wa Shinyanga una ng'ombe milioni tatu, Jimbo la Solwa lina ng'ombe 3,344,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Benedict Kiroya Losurutia, na ninaomba Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae kama muda utaturuhusu.

**MHE. BENEDICT KIROYA LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kwanza nitoe shukrani kubwa kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, wala sina la kusema, hotuba hii ni nzuri sana, nina uzoefu kabisa katika jumba hili, natimiza sasa karibu miaka 20 inakwenda sijawahi kuona hotuba nzuri kama

hii. Haina maneno mengi. Ukishaona watu wanarudiarudia maneno ni kwamba hotuba ni nzuri na kwamba wamejaribu kutekeleza yale yote na hii inatokana na kuwa mkweli na kufanya kazi. Hayo ndiyo matunda yake. *(Makofi)*

Kwanza nashukuru sana wale Wasaidizi wake, Mawaziri pamoja na wataalamu kwa kuweza kutengeneza hotuba nzuri yenye mwelekeo ambayo tutakwenda kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi nina machache ambayo ni muhimu nianze kuyatanguliza. La kwanza, tuna mradi wa maji wa *World Bank* na ambaye sasa hivi ni Waziri Mkuu alianzisha akiwa katika Wizara ya Maji na sisi tulikuwa kwenye *pilot area*, kulikuwa na Wilaya nyingi tu kama 10 na zaidi. Mpaka sasa miradi hiyo yote haijatekelezwa. Shida fedha zote zimeletwa, hapa Wizara ya Maji kuna urasimu mkubwa, wamepewa jukumu la kununua pampu hawanunui, basi visima vimekaa tu. Hatujaingia awamu ya pili ambayo nchi nzima inatakiwa itekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, fedha tayari *World Bank* imesha-*release,* zipo Tanzania, tatizo ni urasimu, nani anunue pampu? Sasa ukishasikia urasimu wa namna hiyo, basi tunakuwa na fikra kubwa sana. Tunaomba sana ukavalie njuga wananchi, wamechoka kuangalia visima kila siku, vimejengwa, maji hakuna na pampu hakuna. Sasa mpango gani huu? Tusisifiane bure, tuwe na kitu ambacho tunaonyesha wananchi.

La pili, tunaomba sekondari. Nina hakika katika Jimbo langu tulikuwa katika hali mbaya, lakini sasa hivi tunakwenda vizuri, tumepata makada ambao wanafanya kazi, tuna hakika ulitembelea tulikuwa na sekondari mbili na sasa tuna hakika ya sekondari nane mwakani na zinajengwa. Ila nataka ni–*register* kitu kimoja, katika hizi Wilaya za wafugaji tumeanza sisi kupeleka watoto bweni wakiwa katika *Primary School,* tunapokuja *Secondary School* Taifa linapata kigugumizi kama unapeleka mtoto akiwa *Primary School* na kumpleka bweni kwa sababu hana mahali pa kukaa katika *Primary School,* anapokwenda Sekondari si ndiyo inakuwa mbaya zaidi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana shule zetu za Sekondari ziwe shule za bweni. Tunaziomba sana, sisemi mahali gani, lakini shule zote za wafugaji ziwe katika bweni. Sio upendeleo! Kama mnataka kutuacha, kwa nini msituambie tu kwamba mkachunge ng'ombe kuliko kutubabaisha tu!

Kuna watu ambao tumewatupa kama Watindiga na Wandorobo, pia wanaokota matunda, sisi tupo hapa katika jumba jekundu, tuna makoti mekundu tumewaacha tu, ni vizuri kusema wazi. Mimi pale kwangu Kiteto tumetenga vijiji vya Wandorobo, Wamasai wanataka kuingia pale, nawaambia hapana, hivi ni vijiji vya Wandorobo na shule Wandorobo msiwaingize watoto na ninawatunza kwa sababu ninaona mbali baadaye watatupa taabu nchi hii. Lazima nitawapeleka shule, niwajengee hospitali na kitu chochote ninachopata hapa niwapelekee. Mimi ndiye nawatunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania wengine sasa hivi hawalimi mabonde na wengine wanatangatanga huko na huko, nani atawapelekea chakula cha kula

bila sisi? Nani? Unamsubiri Mzungu ampelekee Marekani! Wanatusubiri sisi tuwapeleke shule na tuwajengee kwa sababu ndiyo sisi tumeona mbali, ndiyo maana tunahangaika kusema kwamba tupeni shule za bweni.

Rais Mstaafu - Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa alikuja akaahidi kujenga Sekondari katika kila Wilaya, amekwenda na ahadi yake, ameondoka. Hawa wamesema mahali pagumu tutapeleka, watamaliza muda wao wataondoka, hivi nani huyu atakayetuonea huruma? Nani? Sasa shule tumeshajenga, tunaomba sasa shule za bweni kwa wote. Wengine wako Hanang Wabarbaig wanatembea, wengine Wahadzabe wanaondoka, siyo Wamasai tu, wapo wengi sana, wako *minority* wengi sana katika nchi hii na kuna watu wanakula rehema tu. Hii keki tunagawana tunaangalia kabisa wanavyokula na wanavyomega tunawaangalia! Kwa hiyo tunaomba kabisa ifanyike. *(Makofi)*

Hata sisi Manyara tumeungana na Wairaki pale, tuna vitu wanatuambia kwamba ninyi bado kidogo, chukueni hiki kiti kikubwa ili muweze kutuendesha. Huo ndiyo utaratibu.

Kitu kingine ninachotaka kuzungumza ni barabara. Tumeungana na Manyara na Babati. Katika barabara, tumeambiwa msiende Arusha, nendeni Manyara, kwa nini? Tukasema hatuna barabara, Serikali ikatoa ahadi kwamba tutawatengenezeeni barabara kutoka Babati mpaka Kibaya mpaka Orukesiment.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeungana na wenzetu wa Manyara wakatuacha hewa, hakuna barabara. Sasa kama wameshindwa, turudi Arusha ahadi yetu ilikuwa barabara, njia fupi, wamefika wakasema mpaka miaka 30 ndiyo barabara iwe tayari, alah! Miaka 30! Keshokutwa kama mtaweza kutengeneza barabara njia ya Arusha nyeupee turudi, ya nini kuhangaika? Ahadi hawajatekeleza wao wenyewe, sisi tumekubali, sisi turudi na sasa tuseme tutekelezeni ahadi za wenzetu ili yale waliyokuwa wanafikiria, basi itakuwa ni mbaya sana kama Mzee unafariki halafu boma lako linaingiliwa na kila kitu, mbaya sana. Inatakiwa kama unafariki, yale uliyoanzisha yanafanyika na kuendelezwa, lakini huu utaratibu wa sasa hivi unafariki unakwenda na vyombo vyako vyote, hii ni mbaya sana. *(Kicheko)*

La mwisho, madogo madogo haya ni kuhusu Ofisi ya Bunge. Tangu mimi nichaguliwe sijui ofisi. Nyumbani, barabarani na popote, sijui. Mnatenga hela lakini Mbunge miaka 20 hana Ofisi jamani hii ni kazi mpya kabisa, hana ofisi. 30 years uko Barabara unadunda tu, hizi pesa mmepata kidogo kabla mimi sijaacha basi tutengeneze pale Kiteto twende zetu tukajenge ionekane hata Ofisi ya Mbunge kwamba ndiyo hii. Mimi naonekana njiani ndiyo ofisi na ndiyo karatasi nimeshatengeneza mema hapa naandika barabarani, kwisha! Complimentary basi imekwisha mimi ofisi yangu imekamilika. Kwa hiyo, tunaomba sasa kama kuna ofisi basi tunaomba mara moja hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Lingine la mwisho ni suala la Kata na Vijiji. Wengine mambo ya Kata na Vijiji walimaliza miaka 10 na 15 iliyopita, lakini sasa hivi ndiyo tunazinduka. Kwa wenzetu Kata moja ni sawasawa na Wilaya mbili za kwao. Ndiyo! Sisi hatukuwa na habari

kwamba kukatakata Wilaya ndiyo maendeleo, tulifikiri ukubwa wa Wilaya ndiyo maendeleo sasa hivi tumekuja kugutuka loh! Ndiyo maendeleo. Tena tuliombwa wakati ule kwamba tukate Wilaya tukasema aaah! Usitupunguze! Sasa hivi kwenda Makao Makuu ya Kata ni kilomita 70 mpaka 80 kufanya kitu kinachoitwa *ODC* kwetu ni ndoto, mpaka kuendesha gari uende *ODC*.

Rais wetu Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa alikuja kutembelea kule akatupa Kata saba kwa haraka haraka, kumbe hakupitisha kwenye gazeti la Serikali, Sheria ikatubana. Wakati ule Waziri akiwa ni Mheshimiwa Kingunge-Ngombale Mwiru tukabanwa tukaachwa hivyo. Kwa kutuonea huruma tu, tunaomba sasa mje kwetu, nadhani Mheshimwia Waziri atakuja kututembelea. Nikikwambia Makami Kata yenyewe kijiji kimoja kilomita 80 au 60 njoo utembelee uone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa hatuombi Wilaya, angalau Kata na Vijiji, hiyo tunaomba tupate Kata kama 20, Vijini 30 ukikata kijiji ukamwambia Mmasai atakwambia na michango tutafanyaje? Kijiji kitatakiwa kiwe na watu kama 40,000 au 20,000 ndiyo michango inakuwa shilingi kumi kumi ndiyo inatakiwa. Sasa mnawaambia hapa kila kitongoji kiwe kijiji, wakakubali shule, lakini bado tunaomba vijiji na tunaomba Kata tutakuletea orodha yetu na utukubalie kwani tumehangaika sana. Tukikosa safari hii ndiyo basi, mwisho na tutashangaa!

Mimi naomba sasa nije kwenye agenda ambayo nimesimamia, hayo mengine yalikuwa ni rasharasha tu. Yaliyonifanya mimi nisimame ni *operation* ya kuwaondoa wavamizi katika eneo la Ngweleiya Mutagosi na maeneo ya hifadhi. *Operation* hii kabla haijafanyika, iliundwa Tume na Mkuu wa Mkoa ambapo iliagizwa na Mawaziri wawili wa TAMISEMI na Mazingira wakatoa amri kwa Mkuu waunde Tume. Lile eneo lilishaandikishwa na kadhalika likavamiwa kama lile la Ihefu, lakini hawa ni wakulima na wale ni wafugaji. Walipohamia wakavamia wakafyeka, wakachoma na wakawa sasa wamekaa wanalima, lakini siyo wakazi wa Kiteto tunahangaika nao miaka mingi sana mpaka wananchi wakalalamika ikawa maandanamo, akina mama na hata wazee wakafanya maandamano mpaka Serikali ikasikia ikasemekana kwamba wahame.

Baadaye Tume ile ikafanya uchunguzi wake mzuri sana ikabainika kwamba kweli kuna wavamizi waliingia katika maeneo ya hifadhi katika Msitu wa Solodo ambao umeshatuletea sifa ya *Equator Initiative* ya dunia ambayo inamilikiwa na vijiji saba na hii ya *Musangos* ya Maliasili ikafanyiwa *operation*.

Lakini kulikuwa na watu ambao Tume ilibaini kwamba washikwe, ni wenyeji ndiyo wanauza. Kuna viongozi wa Vijiji wameifanya misitu ya hifadhi kwamba ni mali yao na wanauzia watu kutoka nje. Yupo William Kaula, ni Diwani yuko Soledo anauza, yupo Lapunyati - Diwani wa Kata yangu anauza. Tume imebaini kwamba huyu anauza na vijiji vimebaini lakini leo wakaachiwa wanatembea.

Serikali ikafanya *operation* ikawaondoa watu 17,000, nina hakika ulikwenda kuwatembelea akina mama wanafanya maandamano. Wale Madiwani pamoja na wale waliouza wamewarudishia tena watu katika maeneo yale kusema haya ni nguvu ya soda

tu, ninachoomba Serikali iwe Serikali. Huwezi kufanya mapinduzi hata siku moja nje ya mapambano. Huyu yupo ndani ya msitu, ndiye anazuia mapinduzi haya, ninachoomba washikwe, kama huwezi kuwafukuza, basi simamisheni uongozi ili Serikali ifanye kazi. Hilo ni moja katika kuleta mafanikio.

La pili nataka niseme kwamba juzi kulikuwa na *CC* gari ya Mkuu wa Wilaya pamoja na gari ya Mkurugenzi wamekwenda katika eneo hilo kwa ajili ya kuangalia tu ikapigwa mawe na wale wavamizi pia wakavunja vioo wakakimbia. Wamekaa wiki tatu, karibu ya nne ndiyo wanakwenda kushughulikia kupigwa gari ya Serikali, gari ya Polisi inakwenda pale inashangiliwa, hiyo ndiyo Serikali! Gari ya *DC* inapigwa mawe, gari ya Polisi inapita pale inashangiliwa, kuna nini hapo? Duniani gari ya Mkurugenzi inapigwa mawe, gari ya Polisi inavishwa khanga, kuna nini hapo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Losurutia, naomba uunge mkono hoja muda umetimia.

**MHE. BENEDICT KIROYA LOSURUTIA:** Kweli eeh! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba Serikali ishughulikie haraka sana iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba umalizie.

**MHE. BENEDICT KIROYA LOSURUTIA:** Naomba sasa nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Benedict Losurutia na tunamshukuru Mungu kwamba kwa kweli leo umeonyesha kwamba afya yako sasa imerejea kisawasawa kabisa kwa asilimia mia moja na ninaamini wapiga kura wako wamekusikia na kukushuhudia jinsi ulivyo na afya muafaka kabisa sasa.

Waheshimiwa Wabunge naomba sasa nimwite Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na ninafikiri atakuwa ndiye msemaji wetu wa mwisho siku hii ya leo.

**MHE. LUHAGA JOELSON MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu, hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu zetu ambao wametutoka, Ndugu yetu Peter Matagurwa Mwenyekiti wa *SHIRECU* (Shinyanga), lakini vilevile nitoe salamu za rambirambi kwa Mwenyekiti wangu wa Kata ya Kisesa Mheshimiwa Edward Ndibato, Mwanamapinduzi ambaye kwa kweli alikuwa mpiganaji wa Chama Cha Mapinduzi naye katangulia mbele za haki, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa spika yangu ya mwanzao ilikuwa haina sauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niendelee kuwashukuru kwa kweli wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa kwa kuniwezesha mimi kusimama Bungeni hapa na kwa kutambua kazi ngumu waliyoifanya kunitoa toka kwenye Uenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wilaya hadi Ubunge. Ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue muda mfupi kutoa salamu za pongezi toka kwa wapiga kura wangu kwa Serikali ambao wamenituma niseme wana-Kisesa tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali kutenga fedha za ujenzi wa daraja la mto Simiyu. Daraja hilo limemaliza wananchi wengi, limemeza ndugu zetu wengi, lakini Mheshimiwa Rais wetu amekubali na fedha zimetengwa na sasa hivi harakati za ujenzi ziko karibu kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kunipa mimi heshima na Halmashauri yangu kutekeleza mradi huo wa ujenzi wa daraja la Simiyu ambalo ni la Muungano. Wapiga kura wangu wamenituma nitoe shukrani za pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika mwaka jana.

Nilisimama hapa Bungeni nikatoa kilio kikubwa sana juu ya mawasiliano Jimboni kwangu, kaka yangu Mheshimiwa Andrew Chenge aliniambia mdogo wangu tulia, kazi nitaifanya. Zilipita siku saba tu, gari lilikwenda lenye vifaa vyote na mnara ukajengwa ukakamilika Kisesa sasa mawasiliano yapo sawasawa na hiyo ndiyo kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamenituma pia nishukuru kwamba madaraja ya Igobe, Tindabuligi na Sakasaka ambayo kwa kweli yamemaliza watu wengi kwa kuchukuliwa na maji na wengine kuliwa na mamba na viboko sasa yanajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo, basi nianze kwa kuchangia. Matatizo yanatofautiana eneo na eneo. Napenda nizungumzie juu ya tatizo la barabara za vijijini. Kuhusu barabara za vijijini, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha shilingi bilioni 65.5 kwa ajili ya Mfuko wa *Road Fund* katika Halmashauri zetu. Mfuko huu ndiyo unaotumika kutengeneza barabara zetu ambazo tayari zimechongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nishukuru baada ya kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeona ule mpango wa usafiri wa Serikali za Mitaa, *Local Government Transport Programme* kwa ajili ya kufanya matengenezo makubwa na kuchonga barabara mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimewahi kufika katika baadhi ya maeneo. Niliwahi kutembelea Tunduru katika ziara isiyo rasmi. Nikatembelea eneo la kutoka Lukumbule kwenda Makande, hata kwa usafiri wa baiskeli huwezi kupita. Meatu, Jimbo la Kisesa, barabara inayotoka Tindabuligi kwenda Longaloniga, Longaloniga - Mwamhongo, Mwamhongo - Mwasengela hata kama unakwenda kwa miguu inabidi uwe

unaangalia tu mahali ambapo hakuna miti ndiyo unapita, hakuna barabara. Barabara inayotoka Mwabulutagu kwenda Lingeka na kwenda Malwilo haipitiki. Barabara inayotoka Lubiga kwenda Mwanduitinje kwenda Mwabusalu, haipitiki na daraja linalounganisha Jimbo la Kisesa na Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu, daraja la Lubiga nalo halipitiki**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya kuna matatizo makubwa sana. Akinamama wajawazito, watoto na wagonjwa wengine hufa bila kupata matibabu. Hata shule za msingi na sekondari tunazozijenga walimu wanazikimbia. Shughuli za kiuchumi nazo ni ngumu sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na *Local Government Transport Programme,* ili barabara zetu za vijijini ziweze kuchongwa na kufanyiwa matengenezo makubwa. Lakini nilivyochunguza kwenye makabrasha nikakuta kwamba fedha zilizotengwa katika mpango huo ni shilingi bilioni 2.2 tu kwa nchi nzima. Pale ndipo nilipoanza kukosa raha. Lakini labda Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani atanipa raha wakati atakapokuwa anahitimisha hoja yake kwa kusema kwamba maeneo ambayo nimeyazungumza yatapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kila mwaka. Bajeti mwaka 2005/2006 zilitengwa fedha kwa ajili ya kununua magari 22, nadhani yalinunuliwa. Mwaka 2006/2007 zilitengwa fedha kwa ajili ya kununua magari 35, nadhani nayo yamenunuliwa. Lakini wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anawasilisha hoja yake sijaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya kununua magari kwa mwaka 2007/2008. Lakini nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu alisahau, wakati anafanya majumuisho naomba ataje ni magari mangapi? Je, Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mwandoya ambacho kiko umbali wa kilomita 60 kutoka hospitali ya Wilaya? Watu wengi wanakufa bila kupata matibabu kwa sababu ni mbali sana, kilomita 60. Wanatozwa fedha nyingi sana kutoka kwenye kituo cha Afya kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya, siyo chini ya Sh. 150,000/= mpaka Sh. 200,000/=. Kwa mwananchi wa kawaida hizo ni fedha nyingi sana, hawezi wakahimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisemea vizuri sana akiwaagiza Watendaji wa Umma kwamba wafanye kila linalowezekana kutunza fedha na raslimali za umma.

Mimi wakati nachambua ile hotuba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali niliona kwamba katika Wizara na katika Idara na katika Mawakala wa Serikali kuna mabadiliko na mabadiliko hayo yanaonekana kwamba hati safi zimeongezeka kutoka 23 mpaka hati safi 40. Hati zenye shaka zimepungua kutoka 43 mpaka 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni jitihada ambazo kwa kweli ni za kupongeza. Ni mabadiliko makubwa ambayo yanahitaji pongezi. Tatizo lililopo sasa ni kwenye

Halmashauri zetu za Wilaya ndizo zenye matatizo. Watendaji wetu wa Halmashauri hawataki kubadilika, hoja ni zile zile kila mwaka. *Dat*a zinasema badala ya hati safi kuongezeka zimekuwa zikipungua kutoka 62 mpaka 53. Hati zenye shaka zimeongezeka kutoka 51 mpaka 67. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utagundua kwamba kuna Halmashauri ambazo zilipata hati safi mwaka 2004/2005, lakini mwaka 2006/2007 zimepata hati zenye shaka. Pia kuna Halmashauri ambazo zinapata hati yenye shaka kila mwaka.

Ina maana kwamba maelekezo na ushauri unaotolewa na *CAG* kila mwaka hauzingatiwi. Maelekezo na ushauri unaotolewa na Kamati ya *LAAC* nao hauzingatiwi. Kwa maana hiyo sasa, Kamati ya *LAAC* imeendelea kuhoji matatizo yale yale, kasoro zile zile kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Sheria na kanuni za za Fedha za Umma pamoja na Manunuzi zinakiukwa kila mwaka. Hata mwaka jana Waheshimiwa Wabunge walisimama hapa kuzungumza juu ya fedha zinavyotumika vibaya kwenye Halmashauri. Tulisema sana na tukasisitiza kwamba tunataka sasa mahesabu ya Halmashauri yarekebishwe ili yawe mazuri. Lakini hakuna mabadiliko.

Ukiangalia hoja za Wakaguzi, utagundua kuwa zinasababishwa na uzembe, wizi, udanganyifu hata rushwa. Mfano, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakaguzi walishindwa kuletewa vitabu vya risiti vya maduhuli vitabu 27. Halmashauri ya Igunga vitabu 24. Sasa katika utaratibu wa kawaida na mimi nimekaa kwenye Halmashauri na nilikuwa Mhasibu, vitabu hivyo vinatunzwa *strong room.* Sasa mtu akikueleza kwamba havikuwasilishwa kwenye ukaguzi, maana yake nini? Fedha zimetumika zina nyaraka pungufu. Mbeya fedha zimetumika shilingi milioni 205.3 bila nyaraka. Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imetumia shilingi milioni 331.4 bila nyaraka, hakuna *supporting documents*. Ifahamike kuwa, Afisa Mhasibu ndiye anayeamua aidha upatikanaji wa hati inayoridhisha, yenye shaka au hati chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi ndiye anayesaini malipo yote baada ya kujiridhisha kwamba malipo hayo ni halali na kwamba viambatanisho vyote vipo. Sasa ukikuta mtu amesaini mpaka shilingi milioni 205, amesaini mpka shilingi milioni 331 zote zimeidhinishwa, bila viambatanisho. Ni wizi. Hao watu lazima wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda unakwenda haraka, labda nitoe ushauri wangu kabla sijagongewa kengele. Kwanza, ningeomba ifanyike *special audit investigation* katika Halmashauri ambazo zimepata hati chafu na hati zenye shaka Wakuu wetu wa Mikoa wanaweza kuzifanya hizo kazi mkiwakabidhi kusimamia mpiganaji kama *Brig. General* Balele, *RC* Shinyanga akimkabidhi afanye hiyo kazi, tutapata hati safi nyingi sana. Mwaka jana aliwaita Wakurugenzi kwenye Kikao cha *RCC* akaambiwa kwamba kama Halmashauri itakosa fedha za mradi kwa mahesabu mabaya, Mkurugenzi aandike barua ya kujiuzulu. Kipindi hiki Shinyanga tumepata hati safi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna sababu ya kuendelea kuwa na Wakurugenzi dhaifu, wenye uwezo mdogo wakati tunao watu wachapakazi wazuri, waondolewe madarakani tuwaweke wachapakazi ili tuweze kuendana na Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi hao katika utaratibu ule wa kusaini Mkataba wa kazi, basi moja ya kipengele iwe ni pamoja na kusaini Mkataba wa Halmashauri yake kupata hati safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilikuwa katika Meza yetu, sasa tumezimaliza kwa siku ya leo baada ya kuwasikia wachangiaji ambao wamepata nafasi ya kuchangia hoja zao kwa kipindi hiki cha jioni. Ninaomba niwataje wasemaji watakaochangia mwanzo kwa siku ya kesho kusudi wapate nafasi nzuri ya kujiandaa na kuwa karibu kipindi hicho kitakapofika. Tutaanza na Mheshimiwa Ali Said Salim halafu atafuatia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na atafuatia Mheshimiwa Ramadhani Maneno. Hao ndiyo watakuwa wasemaji wetu watatu wa mwanzo na wale wengine watapangwa kulingana na utaratibu kadri ya orodha yetu inavyotuelekeza tulivyoiacha leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa ushirikiano katika kipindi cha leo cha jioni na kwa kuwa sasa muda wetu umefika, ninaomba sasa niahirishwe Bunge mpaka Kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 27 Juni, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*